## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR








## RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

## KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UKARABATI WA UWANJA WA MICHEZO GOMBANI CHAKE CHAKE PEMBA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UKARABATI WA UWANJA WA MICHEZO GOMBANI CHAKE CHAKE PEMBA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**
2 Mtaa wa Tume, 71125 Kilimani Zanzibar, S.L.P 258
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

**MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4** **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

**MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**AFISI YA RAIS IKULU,**
**S.L.P. 437,**
**ZANZIBAR, TANZANIA.**

**KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UKARABATI WA UWANJA WA MICHEZO GOMBANI CHAKECHAKE PEMBA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

---

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Chake Chake Pemba kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

.......................................
**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR.**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

## Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

## Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

## MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu**
Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.

2. **Uadilifu**
Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

3. **Kuwa Huru**
Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.

4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi**
Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

5. **Kutunza Siri**
Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

6. **Uwazi na Uwajibikaji**
Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

# YALIYOMO

YALIYOMO ....................................................................................III
ORODHA YA MAJADWELI.........................................................................VII
ORODHA YA PICHA ...............................................................................IX
VIFUPISHO ........................................................................................ X
DIBAJI..............................................................................................XII
**SURA YA KWANZA** ............................................................................ 1
1.0 UTANGULIZI................................................................................. 1
1.1 CHIMBUKO LA UKAGUZI ................................................................ 1
1.2 UBUNIFU WA UKAGUZI (DESIGN OF THE AUDIT).......................... 3
1.2.1 MALENGO YA UKAGUZI.............................................................. 3
1.2.2 VIGEZO VYA TATHMINI................................................................ 3
1.3 UPEO WA UKAGUZI......................................................................... 6
1.4 MBINU ZA UKUSANYAJI NA UCHAMBUZI WA TAARIFA .................. 7
1.4.1 MBINU ZA UKUSANYAJI WA TAARIFA......................................... 7
1.4.2 MBINU ZA UCHAMBUZI WA TAARIFA .........................................11
1.5 MCHAKATO WA UTHIBITISHAJI WA TAARIFA...............................11
1.6 VIWANGO VYA UKAGUZI VILIVYOTUMIKA ...................................11
1.7 MUUNDO WA RIPOTI .....................................................................12
**SURA YA PILI**....................................................................................14
2.0 MFUMO WA UKARABATI WA UWANJA WA GOMBANI.......................14
2.1 TAARIFA YA AWALI........................................................................14
2.2 SHERIA ZINAZOTUMIKA KWA KUSIMAMIA UKARABATI WA UWANJA...........................................................................................14
2.3 MAJUKUMU NA WAJIBU WA WAHUSIKA WAKUU ..........................15
2.3.1 WAJIBU WA WATENDAJI WAKUU KATIKA UTEKELEZAJI WA UKARABATI WA MIRADI ....................................................................15

2.3.2 FEDHA KWA AJILI YA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA UWANJA WA MICHEZO (KUFANYA UKARABATI NA UBORESHAJI WA UWANJA WA GOMBANI) PEMBA ................16

2.3.3 MAJUKUMU YA WAHUSIKA WENGINE KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UKARABATI WA UWANJA .............................17

2.4 MCHAKATO WA UTEKELEZAJI WA MRADI ...................................18

2.4.1 MCHAKATO WA UTEKELEZAJI WA MRADI ULIYOKAGULIWA ...18

2.5 TAARIFA NA MAELEZO YA MIRADI...........................................20

2.5.1 TAARIFA YA MRADI.......................................................20

**SURA YA TATU** ...............................................................25

3.0 MATOKEO YA UKAGUZI ....................................................25

3.1 UTANGULIZI .....................................................................25

3.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UANZISHWAJI NA MIPANGO..............................................................25

3.2.1 HATUA YA UANZISHWAJI NA UPANGAJI WA MRADI ..............25

3.3 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UNUNUZI.......................30

3.3.1 MCHAKATO WA MANUNUZI KUHUSU UPATIKANAJI WA MKANDARASI..........................................................31

3.3.2 MCHAKATO WA KUMPATA MSHAURI ELEKEZI .......................39

3.4 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA...............................................................43

3.4.1 USIMAMIZI WA MKATABA WA KAZI......................................43

3.4.2 KUCHELEWA KUANZA KWA MRADI .....................................50

3.5 USIMAMIZI WA TOFAUTI ZINAZOJITOKEZA KWENYE ONGEZEKO LA FEDHA (ADDENDUM) .................................................59

3.5.1 MALIPO YA ZIADA YA SHILINGI 266,717,200 YALIYOPITISHWA NA MSHAURI ELEKEZI BILA YA KUIDHINISHWA NA WIZARA...........................................................59

3.5.2 MALIPO YA ZIADA YA SHILINGI 411,657,100 YALIYOPITISHWA TENA NA MSHAURI ELEKEZI BILA YA KUIDHINISHWA NA WIZARA..............................................59

3.5.3 USIMAMIZI WA MKATABA WA HUDUMA YA USHAURI............60

3.6 MAHITAJI YA TAARIFA.........................................................63

3.6.1 RIPOTI YA UANZISHWAJI WA MRADI (INCEPTION REPORT) ..63

3.7 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA MRADI NA UDHIBITI WA NDANI (UDHIBITI WA GHARAMA)...........68

3.7.1 MATAYARISHO YASIOJITOSHELEZA YA MAKISIO YA GHARAMA ZA UJENZI (BOQ)..............................................69

3.7.2 KUJITOKEZA KWA DOSARI KATIKA KAZI ZA ZIADA ZILIZOIDHINISHWA.......................................................79

3.7.3 KUJUMUISHWA KAZI ZINAZOPASWA KUFANYWA NA MSHAURI ELEKEZI KATIKA KAZI ZA ZIADA ZA WAKANDARASI...............81

3.7.4 KUTOJUMUISHWA KWA BAADHI YA KAZI MUHIMU KATIKA BOQ YA MKATABA WA KAZI ZA UKARABATI...........................82

3.7.5 TOZO YA BIDHAA ZA AINA MOJA, AMBAYO HUTUMIA VIFAA SAWA NA UKUBWA SAWA LAKINI IMEBAINISHWA KUWA NA KIWANGO TOFAUTI KATIKA BOQ ZA MKATABA......................84

3.7.6 UPUNGUFU WA VIPIMO KWA VIFAA VILIVYOMO KWENYE BOQ ZA MKATABA.......................................................85

3.7.7 KUKOSEKANA KWA USHAHIDI WA KUWASILISHWA KWA HATI YA DHAMANA YA UTENDAJI KAZI (PERFORMANCE SECURITY)..............................................86

3.7.8 KUKOSEKANA KWA MAANDALIZI MAZURI YA HATI ZA MALIPO YA MUDA (IPCS)...............................................87

3.7.9 KULIPA KAMPUNI YA USHAURI SHILINGI 70,000,000 MBALI NA KUTOTEKELEZA MAJUKUMU YAKE KWA MUJIBU WA MKATABA WA HUDUMA YA USHAURI...................................87

3.7.10 KUIDHINISHA MALIPO YA ZIADA KWA MKANDARASI, WIZARA NA MSHAURI ELEKEZI..........................................88

3.8 VIPENGELE VYA KIUFUNDI (UKAGUZI WA UBORA, UPIMAJI WA KAZI, NA UPIMAJI WA VIFAA) - USIMAMIZI WA VIPENGELE VYA UBORA WA MRADI....................................................................90

3.8.1 UHAMASISHAJI HAFIFU WA MKANDARASI ............................90

3.8.2 UHAMASISHAJI MDOGO (MOBILIZATION) WA WAFANYAKAZI MUHIMU WA MSHAURI ....................................................94

3.8.3 UZOEFU USIORIDHISHA WA KAMPUNI KATIKA UNUNUZI WA UTOAJI HUDUMA ZA USHAURI KWA UWANJA WA GOMBANI...97

3.8.4 UKOSEFU WA USHAHIDI JUU YA SIFA ZA WATAALAM WA MSHAURI....................................................................101

3.8.5 TATHMINI YA UBORA WA VIFAA VILIVYOTUMIKA KUKIDHI VIGEZO.......................................................................101

3.8.6 KUFANYIKA KWA UKARABATI WA MNARA BILA YA KUWEPO KWA MICHORO YA MNARA NA RIPOTI YA UCHAMBUZI WA MIUNDO YA MNARA........................................................104

3.9 UKAMILISHAJI NA UFUNGAJI WA MRADI....................................105

3.9.1 MAANDALIZI YA TAARIFA ZA FEDHA ZA MRADI (FINAL ACCOUNT).....................................................105

3.9.2 USIMAMIZI WA MAZINGIRA (MASUALA YA USALAMA NA KIJAMII), NA MASUALA YA AFYA NA USALAMA WA KAZI.........105

3.9.3 UKOSEFU WA UTOAJI WA MASUALA YA AFYA NA USALAMA....106

3.9.4 UKOSEFU WA PROGRAMU ZA UHAMASISHAJI JUU YA VVU/UKIMWI.....................................................................108

3.9.5 UTUNZAJI DUNI WA MAZINGIRA........................................108

3.9.6 KUKOSEKANA KWA MAENEO RASMI YA UTUPAJI WA TAKA.....126

3.9.7 UKOSEFU WA USHIRIKI WA WAFANYAKAZI MUHIMU WA USALAMA NA WATAALAM WA MATIBABU KATIKA MRADI........111

3.9.8 KUMALIZA KWA MUDA WA MATUMIZI KWA VIFAA VYA KUZIMIA MOTO (FIRE EXTENGUISHERS).............................111

**4.0 MAREJEO** ......................................................................113

**VIAMBATISHO** ..................................................................115

# ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Nambari 1: Mgawanyo wa Bajeti kwa mwaka 2020/21 - 2022/23 .16
Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Majukumu ya Wahusika wengineo........17
Jadweli Nambari 3: Mchakato wa utekelezaji wa mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani..............................................19
Jadweli Nambari 4: Taarifa ya Mradi kuhusu Mkataba wa Mshauri Elekezi .21
Jadweli Nambari 5: Taarifa ya Mkataba wa Kazi ya Mradi.........................21
Jadweli Nambari 6: Taarifa za Mkataba wa Usimamizi wa mradi kati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA)..........................22
Jadweli Nambari 7: Majina na Anwani ya Wazabuni ambao walibainishwa na kupewa Hati za Zabuni kulingana na Ripoti ya Tathmini ........................................................33
Jadweli Nambari 8: Majina na Anwani ya Wazabuni ambao walipewa Hati za Zabuni kulingana na Fomu ya Utoaji wa Zabuni .....34
Jadweli Nambari 9: Maelezo ya Usajili chini ya ZCRB na CRB ...................37
Jadweli Nambari 10: Kupingana na Masharti Maalum ya Mkataba na Majadiliano katika Mkataba Na. SMZ / SO1/W/ RCB/2021-22/20.................................................44
Jadweli Nambari 11: Maelezo kuhusu Ombi la Kuongezwa Muda uliowasilishwa Wizarani na Mkandarasi kupitia Mshauri .....................................................52
Jadweli Nambari 12: Malipo yaliyofanywa kwa Mkandarasi hadi sasa........66
Jadweli Nambari 13: Muhtasari wa Tathmini ya Thamani ya Kazi zilizofanywa hadi sasa dhidi ya Kazi za Mkataba kulingana na Mkataba wa hati za makisio ya gharama za ujenzi...................................................67
Jadweli Nambari 14: Gharama za Ujenzi Makadirio BoQ kwa Mradi ..........69
Jadweli Nambari 15: Utoaji usiotosheleza wa Vipimo katika BoQ iliyotumika katika Hati ya Zabuni kwa Awamu ya Kwanza ya Ununuzi na katika BoQ na Njia ya Kawaida ya Vipimo (SMM) ......................................................71

Jadweli Nambari 16: Vitu vilivyotolewa katika BoQ vilivyotumika katika hati ya zabuni kwa Awamu ya Kwanza ya Ununuzi wa Vifaa.....73
Jadweli Nambari 17: Muhtasari wa Vifaa vya kazi za ziada kwa Kazi isizozidi 15% ya Jumla ya Mkataba kulingana na BoQ.....75
Jadweli Nambari 18: Muhtasari wa Kazi ambazo zilitozwa malipo mara mbili katika Mkataba mmoja.....77
Jadweli Nambari 19: Uchambuzi wa BoQ kwa kazi za ziada zilizowasilishwa na Mshauri.....80
Jadweli Nambari 20: Uchambuzi wa BoQ kwa Kazi za Ziada zilizowasilishwa na Mshauri.....81
Jadweli Nambari 21: Vitu muhimu ambavyo havijajumuishwa katika BoQ za Mkataba na katika BoQ kwa kazi ya ziada.....83
Jadweli Nambari 22: Uchambuzi wa BoQ za Mkataba.....84
Jadweli Nambari 23: Uchambuzi wa BoQ ya Mkataba.....85
Jadweli Nambari 24: Malipo kwa Mkandarasi Baada Wizara ya Fedha kutoa maombi ya Malipo yaliyoombwa na Mteja dhidi ya Kiasi cha Mkataba.....89
Jadweli Nambari 25: Wafanyakazi muhimu waliohamasishwa dhidi ya Wafanyakazi Waliopo kwenye eneo la mradi.....91
Jadweli Nambari 26: Orodha ya Wafanyakazi Muhimu wa Mkandarasi na Sifa zinazohitajika.....93
Jadweli Nambari 27: Muundo wa wafanyakazi wa kampuni ya Mshauri Elekezi.....95
Jadweli Nambari 28: Maelezo ya Mahitaji ya Usajili na Leseni.....96
Jadweli Nambari 29: Sifa za Wafanyakazi muhimu wa Mshauri aliyeorodheshwa katika Ripoti za Maendeleo ya Kila Mwezi (Januari hadi Juni 2023).....98
Jadweli Nambari 30: Maelezo kulingana na vyeti vya Elimu na Utaalamu.....100
Jadweli Nambari 31: Matokeo ya majaribio yaliyofanyika juu ya Nguvu ya Zege ya Rebound Hammer.....102

# ORODHA YA PICHA

Picha Nambari 1 : Sheria na Viwango vinavyotumika katika kusimamia utekelezaji wa miradi ....14

Picha Nambari 2: Muhtasari wa Mahusiano kati ya wahusika wakuu ....18

Picha Nambari 3: Ukarabati wa Uwanja wa Gombani....20

Picha Nambari 4: Kituo cha Transforma iliyowekwa juu ya kibanda kwa ajili ya matumizi ya Uwanja....49

Picha Nambari 5: Mabaki ya uchafu kutoka Msingi ulioondolewa kwenye njia ya Riadha ....126

Picha Nambari 6: Kifaa cha kuzimia moto kilichokosa kufanyiwa service .112

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AG | : | Mwanasheria Mkuu |
| AO | : | Afisa Masuuli |
| APP | : | Mpango wa Ununuzi wa Mwaka |
| BoQ | : | Makisio ya Gharama za Ujenzi |
| C25 | : | Daraja la 25 |
| CQS | : | Ushauri wa Uteuzi wa Ubora |
| EIA | : | Tathmini ya Athari za Mazingira |
| EMP | : | Mpango wa Usimamizi wa Mazingira |
| ESMP | : | Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii |
| GCC | : | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| GN | : | Government Notice |
| HSMP | : | Mpango wa Usimamizi wa Afya na Usalama |
| ICT | : | Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari |
| IPCs | : | Cheti cha Malipo ya Muda |
| ITB | : | Maagizo kwa Bidders |
| JV | : | Mradi wa Pamoja |
| kN/mm2 | : | Kilo Newton kwa Milimetres ya mraba |
| $M^2$ | : | Mita za Mraba |
| MDAs | : | Wizara, Idara na Mashirika |
| NEMC | : | Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira |
| OCAGZ | : | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar |
| PPR | : | Kanuni za Ununuzi wa Umma |
| Qty | : | Kiasi |
| R.E | : | Toleo lililorekebishwa |
| SCC | : | Masharti Maalum ya Mkataba |
| SMZ | : | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| ToR | : | Hadidu Rejea |

| | | |
|---|---|---|
| TRA | : | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TZS | : | Shilingi ya Tanzania |
| VAT | : | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| VO's | : | Variation Orders |
| ZAEQRB | : | Bodi ya Usajili ya Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji wa Majengo Zanzibar |
| ZBA | : | Wakala wa Majengo Zanzibar |
| ZCRB | : | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar |
| ZPPDA | : | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| ZRA | : | Mamlaka ya Mapato Zanzibar |
| ISSAIs | : | Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi wa Juu |
| INTOSAIs | : | Shirika la Kimataifa la Taasisi za Ukaguzi |

## DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo wa Gombani Chake Chake Pemba kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka.

Ripoti hii imejumuisha mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi ambapo matokeo, athari na mapendekezo ya ukaguzi yameelekezwa kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wangu ambapo nilifanya tathmini kwa kuangalia taarifa za fedha pamoja na nyaraka mbalimbali zinazohusiana na Mradi huo, taratibu za michakato ya manunuzi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni mbali mbali.

Napenda kuchukuwa fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wangu kwa kujitolea kufanya kazi ya Ukaguzi pamoja na Uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kutoa ushirikiano wao mzuri ambao umewezesha kukamilisha Ripoti hii kwa wakati.

..............................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**

# SURA YA KWANZA



# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Chimbuko la Ukaguzi

Matengenezo ya miundombinu ya Viwanja vya Michezo (Renovation and Remodeling) ni moja kati ya maeneo muhimu ya uwekezaji yanayofanywa na Serikali kupitia Taasisi zake ili kuweza kuzalisha mapato na hatimae kutoa gawio kwa Serikali.

Aidha, ukarabati wa viwanja vya michezo unahakikisha kwamba Wizara, Idara, na Wakala wa Serikali zinakua na hali nzuri katika viwanja vya michezo kwa kuwepo nafasi ya kutosha, vifaa sahihi vya michezo pamoja na mazingira mazuri ya kuwezesha kutekeleza majukumu yao kwa shughuli za michezo na vile vile kuimarisha afya za wananchi. Miundombinu ya Viwanja vya Michezo inawezesha kufanyika kwa matukio mbalimbali ya kiserikali na matukio ya mikusanyiko ya kisiasa.

Sekta ya ujenzi yenye ufanisi ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania. Katika miongo mitatu iliyopita, ujenzi umekuwa sekta kubwa katika mipango ya uwekezaji nchini inayochangia asilimia 50 ya jumla ya uundaji wa mtaji. Lengo kuu la Serikali ni kuendeleza sekta ya ujenzi inayojitegemea ambayo ina uwezo wa kukidhi mahitaji mbalimbali ya ujenzi, ukarabati, na matengenezo ya kazi zote za ujenzi na za kiraia kwa ufanisi na tija.

Udhibiti wa gharama katika ujenzi/ ukarabati ni utaratibu wa udhibiti kulingana na vigezo vya kudhibiti gharama kwa mlinganisho unaotokana na uhusiano wa kiuchumi kati ya gharama, ubora na matumizi ili kuhakikisha vipimo vinavyohitajika vinaendana na gharama halisi ya mradi kwa lengo la kupatikana kwa ufanisi kati ya utendaji halisi na utendaji uliopangwa kwa mazingatio ya thamani halisi ya fedha

Hata hivyo, kuongezeka kwa gharama za ujenzi ni changamoto za kawaida katika miradi ya ujenzi wa umma hapa Zanzibar. Kuna sababu nyingi zinazosababisha gharama kubwa katika majengo ya Serikali na miradi ya ukarabati, miongoni mwa sababu hizo ni kama vile matatizo ya upatikanaji wa fedha kwa wakati, ucheleweshwaji wa malipo kwa wakandarasi, usimamizi duni wa mikataba inayopelekea kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa malipo, uhaba wa vifaa, mabadiliko katika hali ya eneo la mradi, mabadiliko ya usanifu, makosa na tofauti katika nyaraka za mkataba, kushuka kwa bei, makadirio yasiyo sahihi, ucheleweshaji wa kumalizika kwa kazi kwa wakati, kujitokeza kwa kazi za ziada zilizokuwa hazikupangwa katika nyaraka za makisio ya gharama, kufupisha vipindi vya Mikataba, vitendo vya udanganyifu na rushwa.

Dosari zilizotajwa katika ukarabati wa majengo ya Serikali Zanzibar zilipelekea kufanyika kwa ukaguzi wa kiufundi juu ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani na kupendekeza maeneo ya kuboresha katika miradi ya ukarabati na ujenzi inayotekelezwa na Serikali.

Uamuzi wa kufanya Ukaguzi huu wa ufundi ulihamasishwa kutokana na mambo makuu mawili ambayo ni kiwango kikubwa cha gharama kwa mujibu wa fedha zilizotumika pamoja na dosari za kiutendaji zilizoripotiwa zinazohusiana na gharama za juu kwa kulinganisha na ubora wa kazi za ukarabati zilizofanyika katika mradi. Maelezo ya taarifa hizo ni kama inavyoonekana hapo chini: -

- **Kiwango kikubwa cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Pemba**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (Chini ya Idara ya Michezo) imekuwa ikitenga bajeti ya shilingi Bilioni 7 kila mwaka kwa ajili ya kuendeleza viwanja vya michezo. Bajeti hiyo inajumuisha fedha kwa ajili ya ukarabati na maboresho ya uwanja wa Gombani ikiwemo kufanya marekebisho ya miundombinu ya uwanja huo. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba fedha hizo zisimamiwe vizuri ili kutambua thamani ya fedha kwa mujibu wa fedha zilizotengwa na kutumika.

- **Kuripotiwa kwa dosari katika Utekelezaji wa Miradi kuhusiana na Gharama kubwa za usimamizi pamoja na kubainika udhaifu wa ubora wa miradi**

Ukaguzi wa Kiufundi ulihamasishwa na hitaji la kutenga kiasi cha ziada cha fedha kutokana na tofauti za mkataba pamoja na mkataba wa awali wa kazi unaofikia shilingi Bilioni 2.8 kwa kazi za ukarabati. Vile vile, kulikuwa na dosari za kiutendaji zilizojitokeza kuhusiana na ubora wa shughuli za ukarabati wa uwanja. Dosari hizo zilihusishwa hasa na usimamizi duni wa mradi na usimamizi wa mkataba, udhibiti wa ubora, kutofuata sheria na kanuni za ununuzi pamoja na mipango duni na usanifu wa mradi.

Kufuatia dosari za kiutendaji zilizotajwa hapo juu imepelekea kufanya ukaguzi maalum wa kiufundi kuhusu ukarabati wa miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba ili kutathmini kiwango kinachowezekana kutumika kwa uhalisia na kulinganisha na tofauti ya gharama za mradi zilizojitokeza pamoja na kupima ubora wa miundombinu ya uwanja iliyowekwa.

## 1.2 Ubunifu wa Ukaguzi (Design of the Audit)

### 1.2.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi ni kutathmini ikiwa ukarabati wa Uwanja wa Gombani Chake Chake Pemba ulifanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia muda, gharama, upeo na ubora ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa ya mradi.

Ili kufikia lengo kuu la ukaguzi, malengo sita maalum ya ukaguzi yalitumika. Malengo haya maalum ya ukaguzi yalikuwa ni kutathmini ikiwa:

(i) Uanzishwaji na upangaji wa ukarabati wa uwanja ulifanyika vya kutosha ili kuweza kufikia malengo ya mradi;

(ii) Michakato ya ununuzi na mikataba ya wakandarasi, washauri elekezi, bidhaa na huduma za mradi ilifanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za ununuzi;

(iii) Makisio, utoaji na matumizi ya fedha za mradi ulifanyika kwa mujibu wa miongozo ya kifedha;

(iv) Ukarabati wa uwanja ulifanyika kwa ufanisi ili kuweza kukamilika katika muda uliopangwa, gharama, na ubora kwa kulingana na vipengele na masharti ya mkataba;

(v) Uwanja uliokarabatiwa unakidhi ubora na viwango vilivyokusudiwa; na

(vi) Vihatarishi vinavyohusiana na mazingira, usalama na athari za kijamii wakati wa utekelezaji wa mradi vilitambuliwa na kushughulikiwa kulingana na mahitaji ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sheria ya Afya na Usalama wa Kazi na vipengele na masharti ya mikataba.

### 1.2.2 Vigezo vya Tathmini

Ili kutathmini utoshelevu wakati wa utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa Uwanja wa Gombani Pemba, vigezo vya tathmini vilitolewa kutoka vyanzo mbalimbali kama vile Sheria, Kanuni, Masharti Maalum ya Mkataba, Masharti ya Jumla ya Mkataba, Maelezo ya Mikataba, Mipango Mkakati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mipango ya Ununuzi wa Mwaka na Bajeti za Wizara, miongozo, viwango kubalifu na nyaraka za mkataba, miongozo ya kifedha, Mkataba wa Makubaliano, na Hati ya Ubunifu wa Mradi. Vifuatavyo ni vigezo vya tathmini vilivyotumika kwa kila lengo la ukaguzi:

- Utoshelevu wa kupanga na kubuni miradi kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili kuwezesha kufanikisha malengo ya mradi

Kanuni nambari 43(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2021 inahitaji manunuzi yoyote yatakayofanywa na Taasisi kuidhinishwa na Afisa Masuuli. Hii ni pamoja na kuanzisha mipango ya ununuzi katika hatua ya ubunifu wa mradi. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar inahitaji utafiti wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhiliwa kwa mradi.

Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Zanzibar inaitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira baada ya kuchunguza muhtasari wa mradi, kumtaka msimamizi wa mradi au kufanya utafiti wa Tathmini ya Athari za Mazingira na kuandaa Taarifa ya Athari za Mazingira ambayo itawasilishwa kwa Mamlaka kwa ajili ya ukaguzi.

- Kukubaliana na mchakato wa ununuzi wa bidhaa na huduma kulingana na mkataba wa wakandarasi, washauri elekezi kwa kuzingatia Sheria na kanuni husika za ununuzi
- Utoshelevu wa makisio, malipo, na matumizi ya fedha za mradi kwa mujibu wa miongozo ya kifedha.
- Ufanisi wa utekelezaji wa miradi ili kufikia muda wa kukamilika kwa mradi, gharama, na ubora unaotarajiwa kulingana na masharti ya mkataba.

Kifungu nambari 45.1(c) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kwamba Mteja atafanya malipo ndani ya siku 60. Kifungu nambari 46.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza zaidi kwamba ikiwa Mteja amecheleweshа malipo zaidi ya siku kumi na tano (15) baada ya tarehe ya mwisho adhabu itawekwa.

Kifungu nambari 13.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kwamba Mkandarasi atatoa, kwa majina ya pamoja ya Mwajiri na Mkandarasi, bima kuanzia tarehe ya kuanza hadi mwisho wa Kipindi cha mpito cha uangalizi wa mradi (Defects Liability Period), kwa kiasi na makato yaliyotajwa katika Masharti Maalum ya Mkataba kwa matukio yatokanayo na vihatarishi vinavyotokana na kazi za Mkandarasi.

Aidha, Kifungu nambari 23 cha Masharti Maalum ya Mkataba kilibainisha kuwa kiasi cha malipo ya awali kitakuwa asilimia 20 ya bei ya mkataba bila ya kujumuisha gharama za ziada (provisional sum). Mkandarasi atalipwa malipo ya awali mara baada ya kuingia mkataba na baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali (advance payment guarantee).

Baada ya malipo kwa Mkandarasi, Kifungu nambari 46.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kuwa malipo yatarekebishwa kwa makato ya dhamana ya malipo ya awali na zuio la fedha (advance payments and retention money). Kifungu nambari 45.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kuwa Mwajiri atamlipa Mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na Msimamizi wa Mradi ndani ya siku 28 baada ya kupokea kwa ajili ya malipo.

- Utoshelevu wa miradi iliyojengwa katika kukidhi ubora na viwango vilivyokusudiwa

Sehemu ya 3.2.1 ya BS EN 1997-1: 2004 [Geo technical Design] inaeleza kuwa uchunguzi wa ubunifu wa kiufundi wa kijografia (geo technical Design) utatoa taarifa za kutosha kuhusu ardhi na hali ya maji ya ardhi ndani na karibu na eneo la ujenzi kwa maelezo sahihi ya vitu vilivyomo katika ardhi ya ujenzi na tathmini ya kuaminika ya kuangalia tabia ya vigezo vya ardhi kutumika katika kufanya mahesabu.

Sehemu ya 3.2.3 ya BS EN 1997-1: 2004 [Geo technical Design] inaeleza kwamba, ili kuhakikisha kuwa uchunguzi wa kubuni unashughulikia maeneo yote ya ardhi, tahadhari inayoweza kujitokeza inapaswa kupewa vipaumbele vifuatavyo vya kijiolojia: wasifu wa ardhi; mashimo ya asili au ya kibinadamu; uharibifu wa miamba, udongo, au vifaa vya kujaza; madhara ya unyevu unyevu wa maji "hydrogeological" ; kasoro, viungio na nyinginezo; udongo unaotawanyika na wingi wa miamba; udongo na miamba inayopanuka na yenye kubomoka; na uwepo wa taka au vifaa vilivyotengenezwa na mwanadamu.

- Utoshelevu wa miradi iliyotekelezwa kuhusiana na hatari zilizotambuliwa zinazohusiana na mazingira, usalama, na athari za kijamii kulingana na mahitaji ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sheria ya Afya na Usalama wa Kazi, na Masharti ya Mikataba.

Kifungu nambari 21.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kuwa Mkandarasi atazingatia sheria zote za kazi zinazotumika Zanzibar, ikiwa ni pamoja na sheria zinazohusiana na ajira za wafanyakazi, saa za kazi, afya, usalama, ustawi, na uhamiaji, na kuwaruhusu haki zao zote za kisheria.

Kifungu nambari 21.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza zaidi kwamba Mkandarasi atahitaji wafanyakazi wake kutii sheria zote husika, ikiwa ni pamoja na zile zinazohusu usalama kazini. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba vifaa vya huduma ya kwanza vinapatikana wakati wote kwenye sehemu ya kazi na kwamba mipango inayofaa inafanywa kwa mahitaji yote muhimu ya ustawi na usafi na kuzuia magonjwa ya mripuko.

Kifungu nambari 20.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kuwa Mkandarasi atachukua hatua zote za busara kulinda mazingira na kupunguza uharibifu na kero kwa watu na mali inayotokana na uchafuzi wa mazingira, kelele, na matokeo mengine ya shughuli zake.

## 1.3 Upeo wa Ukaguzi

Ukaguzi wa kiufundi umefanyika kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Zanzibar, ambapo ulifanyika kwa kuzingatia mwenendo wa usimamizi wa mradi kuhusu mambo yanayohusiana na mipango, usanifu, fedha, manunuzi, usimamizi wa mkataba, mambo ya kiufundi, mazingira, usalama, na kijamii.

Ukaguzi huo ulihusisha kukagua na kutathmini michakato ya jinsi mradi ulivyopangwa, ulivyoundwa, utaratibu wa manunuzi, hatua za utekelezaji, ukamilishaji wa mradi na hatua ya kufungwa kwa mradi. Ukaguzi pia ulithibitisha viwango vya muundo vilivyotumiwa, vipimo, ubora wa kazi kwa maeneo yanayokarabatiwa ya mradi, hali halisi ya hatua ya utekelezaji pamoja na utendaji wa wafanyakazi wa mradi.

Katika kipengele cha usimamizi wa kifedha, ukaguzi ulifanya tathmini juu ya uwepo wa ufanisi katika utoaji wa fedha zilizopangwa na kuidhinishwa kwa matumizi ya mradi, ufanisi wa udhibiti wa ndani wa kifedha, na kuzingatia kanuni za kifedha zinazoongoza na hali ya malipo kama ilivyoonyeshwa katika hati za mradi husika. Uchunguzi wa taarifa za hesabu za mwisho za mradi ikiwa ni pamoja na udhibiti wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na pamoja na kuzingatia malalamiko yanayotokana na madai ya mradi.

Kipengele cha usimamizi wa manunuzi kinahusisha tathmini ya uzingatiaji wa taratibu za manunuzi na taratibu za uingiaji wa mikataba kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake; au sheria yoyote husika au miongozo kama ilivyoonyeshwa katika nyaraka za mradi husika. Shughuli kama vile bajeti ya ununuzi na upangaji wa ununuzi, utoshelevu wa maandalizi ya nyaraka za zabuni, mchakato wa zabuni, tathmini ya zabuni, na utoaji wa mkataba kwa wakandarasi na washauri ikiwa ni pamoja na kusainiwa kwa mikataba itapimwa.

Kipengele cha kiufundi, kilihusisha kufanya tathmini ya ubora na wingi wa matokeo ya mradi na vifaa vilivyotumika, kwa kutathmini usawa na usahihi wa kupanga, kubuni, kufuata viwango vilivyokusudiwa, ubora wa kazi, na utendaji. Wakaguzi pia walitathmini utoshelevu na uzingatiaji wa kuhakiki ubora na mfumo wa udhibiti wa miradi.

Kwa kufanya hivyo, Wakaguzi wa Ufundi walifanya ukaguzi kwa kutembelea maeneo ya kazi zilipotekelezwa na kukagua matokeo ya kazi zilizofanyika, kuhakiki matokeo ya majaribio ya uchunguzi uliofanyika katika maabara ya vifaa na sehemu za kazi zilizokamilishwa. Kama sehemu ya kipengele cha kiufundi, Ukaguzi pia ulifanya vipimo visivyo vya uharibifu wa kazi (non destructive test) na miundo iliyojengwa.

Kuhusu kipengele cha usimamizi wa mkataba, Ukaguzi ulitathmini utoshelevu wa mfumo na michakato ya kusimamia utoaji wa mradi kama vile wakati, gharama, na ubora ambapo ilijumuisha tathmini ya mipango ya utekelezaji wa mradi kama vile tathmini ya mradi, upembuzi yakinifu, taarifa za uanzishwaji wa mradi, usanifu wa mradi, muda na makadirio ya gharama, na vipengele vya kuanzishwa kwa mradi. Vipengele vya usimamizi wa mkataba vinavyoainisha usimamizi na ufuatiliaji wa wakandarasi na washauri, kufungwa kwa mradi, na ufunguzi wa mradi pia vilipimwa. Vile vile, Ukaguzi wa Ufundi uliangalia ikiwa Wizara ilizingatia kipengele cha shughuli za kujenga uwezo kwa mafundi wa ndani, Wajibu wa Taasisi kwa Jamii na uhusiano wa kufanya kazi kati ya pande zote zinazohusika katika mradi huo.

Aidha, Ukaguzi wa Ufundi ulitathmini upatikanaji na utoshelevu wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Tathmini ya Athari za Mazingira. Pia ulichunguza kiwango cha uzingatiaji/ utekelezaji wa hatua za kupunguza hatari zinazohusiana na mazingira, afya na usalama wa kazi, na athari za kijamii. Vipengele vikuu ambavyo vilifanyiwa tathmini ni pamoja na masuala ya usalama kwa wafanyakazi, utunzaji wa udongo na taka ambazo zitazalishwa, na kupunguza mmong'onyoko wa udongo.

## 1.4 Mbinu za Ukusanyaji na Uchambuzi wa Taarifa

### 1.4.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Taarifa

Njia tatu za ukusanyaji wa taarifa zilitumiwa na timu ya Ukaguzi wa Kiufundi. Njia hizi ni pamoja na Mapitio ya Nyaraka za Mradi, Mahojiano, na kutembelea eneo la utekelezaji wa mradi katika sehemu zilizokamilika na zinazoendelea kwenye Ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Chakechake Pemba kama ilivyofafanuliwa hapa chini:

### a) Mahojiano

Katika kupata uelewa mpana wa mradi na kutambua changamoto zilizopo za kiufundi, Ukaguzi ulifanya mahojiano na majadiliano na maafisa mbalimbali. Mahojiano hayo pia yalifanyika kwa lengo la kupatikana taarifa za ziada zinazohusiana na utekelezaji wa mradi huo ili kufafanua na kupata uelewa juu ya taarifa zilizopatikana kutoka kwenye nyaraka zilizopitiwa na maeneo ya kazi yaliyohakikiwa. Baadhi ya maafisa muhimu waliohojiwa ni pamoja na Mratibu wa mradi, Meneja wa Mradi, Mhasibu Mkuu/ Mhasibu Mkuu wa Mradi huo, Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, Mshauri Elekezi, Mhandisi Mkaazi na Mkandarasi. Taarifa za maafisa waliohojiwa zimebainishwa katika **Kiambatisho Nambari 1**.

### b) Mapitio ya Nyaraka

Ukaguzi ulipitia nyaraka mbalimbali ili kupata uelewa wa mradi na kutathmini utoshelevu wa mipango/uhitaji wa tathmini, utekelezaji na ufuatiliaji wa mradi. Hii pia ilifanyika ili kutambua hatari zinazoweza kujitokeza katika utendaji au sababu za msingi za matatizo ya utendaji ili kuwezesha ukaguzi kusaidia kuja na matokeo na mapendekezo ya maboresho zaidi. Taarifa zilizokusanywa kupitia nyaraka zilizopitiwa pia zilitumika kuthibitisha taarifa zilizopatikana kutokana na mahojiano ya maafisa wanaohusika na utekelezaji wa mradi.

Nyaraka zilizopitiwa za mwaka 2022/2023 hadi Septemba, 2023 ambazo zinazohusiana na upangaji wa miradi, kumbukumbu za fedha za manunuzi, nyaraka zinazohusiana na na masuala ya mazingira.

Nyaraka zilizopitiwa kutokana na kazi zilizokaguliwa zilijumuisha: -

#### i. Nyaraka za kuanzisha na kupanga mradi

Ripoti ya Tathmini ya Mahitaji, Ripoti ya Uchunguzi wa Eneo la kazi na Udongo (jiolojia, mazingira, zoolojia), Uchambuzi wa Kiufundi / Ripoti ya Uanzishwaji wa Mradi, Ripoti ya Makadirio ya awali ya Wahandisi, Ripoti za Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii, Ripoti za Usanifu, Kuidhinishwa kwa Miundo ya Usanifu, Michoro ya kina ya Mradi, Maelezo ya Mradi ya kiufundi, Mpango wa mtiririko wa Fedha za Mradi na Bajeti.

### ii. Nyaraka zinazohusiana na Ununuzi

Mpango wa Ununuzi wa Mwaka na Bajeti, Nyaraka za Zabuni, Makadirio ya Mhandisi, nyaraka zote za hadidu rejea za Bodi ya zabuni, Barua za Uteuzi wa Kamati ya Tathmini na Timu ya Majadiliano, Ripoti za kiufundi za tathmini ya Zabuni, kumbukumbu za vikao vya mazungumzo ya mapatano, kumbukumbu za idhini ya Bodi ya zabuni, taarifa ya Afisa Masuuli juu ya Uamuzi wa Bodi ya zabuni, tangazo la nia ya zabuni iliyotolewa kwa makampuni yote yaliyoshiriki katika zabuni, barua ya tuzo ya zabuni, uhakiki wa nyaraka za mkataba wa rasimu kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hati ya kiapo, Idhini ya njia za manunuzi, matangazo ya zabuni na nyaraka za zabuni, Uthibitisho wa fedha, Kipengele cha Bajeti za sampuli za Zabuni, kumbukumbu za vikao vya Bodi ya zabuni kuidhinisha Hati za zabuni kwa zabuni ya sampuli, Tangazo la Zabuni , Nyaraka za zabuni zilizouzwa kwa wazabuni kwa zabuni za sampuli na Hati za Mkataba (Fomu ya Mkataba, Barua ya Tuzo ya Zabuni, Masharti Maalum ya Mkataba, Masharti ya Jumla ya Mkataba, Maelezo ya Jumla, Maelezo Maalum, Michoro, Gharama za makisio ya ujenzi na Mazungumzo ya kupatana Kabla ya Mkataba).

### iii. Kumbukumbu za Fedha

Hati ya malipo ya muda, Hati ya kukabidhi kazi (Hati ya awamu ya kazi na Hati ya mwisho kukamilika kwa kazi), na Taarifa ya hesabu za mradi (kufungwa kwa mkataba, kurejeshwa kwa dhamana ya fedha, na kurejeshwa kwa zuio la fedha).

### iv. Nyaraka zinazohusiana na Usimamizi wa Mkataba

Mpango kazi uliyosahihishwa au uliyorekebishwa, Ripoti za Maendeleo, Rekodi za Malipo/Vyeti, maelekezo ya eneo la kazi, hadidu rejea za mikutano ya kusimamia maeneo ya kazi, na Maagizo ya Tofauti (VOs).

### v. Nyaraka za kukamilisha na kufunga miradi

Hati ya mwisho, Hati ya kukamilika kwa vitendo, taarifa ya hesabu za mradi, Hati ya hesabu za mradi, michoro ya Ujenzi, Utendaji na Mpango wa matengenezo ya majengo.

### vi. Nyaraka zinazohusiana na Usimamizi wa Mazingira

Ripoti za Tathmini ya Athari za Mazingira, Mpango wa Usimamizi wa Mazingira, Mpango wa Usimamizi wa Athari za Kijamii na Ripoti za Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira.

### c) Uhakiki wa eneo la Mradi

Ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea kwenye eneo ambapo mradi ulitekelezwa ili kukagua na kuthibitisha kazi halisi iliyofanywa na kufanya uhakiki wa ubora wa kazi zilizotekelezwa. Kupitia ziara hiyo, ukaguzi uliangalia ikiwa kazi zilizotekelezwa zilikubaliana na vipimo, michoro, Makisio ya gharama za ujenzi (BoQ), na masharti yoyote yaliyotolewa katika hati za mkataba na nyaraka za usanifu wa mradi.

Katika ziara hiyo ukaguzi ulizingatia na kupima ubora wa kazi zilizokamilishwa, kuhakiki maeneo ya kazi zilizokamilishwa kwa kulinganisha na vitu vilivyoonyeshwa katika Taarifa ya gharama za makisio ya ujenzi, Vipimo vya hali halisi ya kazi zilizotekelezwa ikilinganishwa na vipimo vilivyooneshwa katika taarifa za makisio ya gharama za ujenzi (BoQ), na uhakikisho wa usalama wa maeneo ya kazi, mazingira na afya kama ilivyoelezwa katika nyaraka za mradi.

Aidha, ukaguzi ulitembelea katika maeneo ya kazi kwa kuzingatia mambo yafuatayo: Hali halisi ya ukamilikaji wa mradi, kasi ya utekelezaji wa mradi ikiwa inakwenda kulingana na mpango wa kazi, Ubora wa vifaa vilivyotumika katika ujenzi, Ubora wa kazi zilizokamilishwa, na Usimamizi wa Mradi (Upatikanaji wa wafanyakazi muhimu, Upatikanaji wa zana zinazohitajika na vifaa ama Mashine na Uthibitishaji wa Kazi).

### d) Mikutano ya kabla ya kumalizika kwa kazi ya Ukaguzi

Kabla ya kumaliza kazi ya ukaguzi na kufanya kikao cha kumaliza kazi ya ukaguzi katika Makao Makuu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Ukaguzi ulifanya mikutano ya awali na maafisa wa Wizara baada ya kumaliza uhakiki katika maeneo ya kazi.

Kikao hicho kilifanyika tarehe 1 Agosti, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 5:00 Asubuhi ambapo madhumuni ya kikao hicho ni kutoa shukurani kwa ushirikiano mkubwa uliotolewa na ufafanuzi mzuri kwa baadhi ya nyaraka ambazo zilihitaji ufafanuzi.

Kwa baadhi ya nyaraka zilizokosekana maafisa wa Wizara waliahidi kuzileta nyaraka hizo kuanzia siku inayofuata (2 Agosti, 2023). Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha nyaraka ambazo hazijakaguliwa ilikuwa ni tarehe 4 Agosti, 2023.

### 1.4.2 Mbinu za Uchambuzi wa Taarifa

Taarifa zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mbinu zote za ubora na kiasi (qualitative and quantitative methods) ili kupata ukweli na taarifa za kutosha kuhusu utendaji wa jumla wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika kusimamia ukarabati wa Uwanja wa Michezo wa Gombani kwa kuzingatia muda, gharama, na ubora.

Katika uchambuzi huo mbinu mbali mbali ziliweza kutumika ikiwemo kuchambua taarifa zenye ubora kwa kutambua dhana tofauti na ukweli unaotokana na mahojiano au nyaraka zilizopitiwa na kuziainisha kulingana na madai yao.

Hata hivyo, maelezo ya kiasi na matukio mengine yaliwekwa kwenye jadweli ili kuendeleza taarifa za uhakika au taarifa ya mfululizo wa wakati na ukweli husika uliotokana na taarifa zilizopatikana.

## 1.5 Mchakato wa Uthibitishaji wa Taarifa

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilipewa fursa ya kufafanua baadhi ya masuala yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi na walipewa muda wa kuwasilisha nyaraka zilizokosekana. Wizara ilithibitisha usahihi wa takwimu na taarifa zilizowasilishwa katika ripoti ya ukaguzi. Pia, Wizara ilitoa uthibitisho wa takwimu wakati wa ukusanyaji wa taarifa.

## 1.6 Viwango vya Ukaguzi vilivyotumika

Ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) juu ya ukaguzi wa utendaji uliotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Ukaguzi kwenye Taasisi za Umma (INTOSAI). Viwango hivyo vinahitaji kwamba ukaguzi upangwe na kufanywa ili kupata ushahidi wa kutosha na usahihi wa ukaguzi kwa lengo la kutoa msingi mzuri wa matokeo ya ukaguzi na hitimisho kulingana na malengo ya ukaguzi.

## 1.7 Muundo wa Ripoti

- **Sura ya Kwanza**: • Utangulizi
- **Sura ya Pili**: •Mfumo wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo wa Gombani
- **Sura ya Tatu**: •Matokeo ya Ukaguzi
- **Sura ya Nne**: •Mapendekezo ya Ukaguzi
- **Sura ya Tano**: •Hitimisho

# SURA YA PILI


STANDARDS
COMPLIANCE
POLICIES
RULES
TRANSPARENCY
REGULATIONS
REQUIREMENTS
CONTROL
LAW



# 2.0 MFUMO WA UKARABATI WA UWANJA WA GOMBANI

## 2.1 Taarifa ya Awali

Sura hii inaelezea mfumo wa Matengenezo ya Miundombinu ya Uwanja wa Michezo (Ukarabati na uboreshaji wa Uwanja wa Gombani) Pemba ikiwemo mfumo wa kisheria, wajibu na majukumu ya watendaji wakuu, michakato ya mradi, mgawanyo wa fedha za mradi na rasilimali watu kwa utekelezaji wa miradi.

## 2.2 Sheria zinazotumika kwa kusimamia Ukarabati wa Uwanja

Matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani yamesimamiwa na kufanyika kwa mujibu wa Sheria, Miongozo, Mikakati, Viwango, na Maelezo kama inavyoonyeshwa katika picha hapa chini.

**Picha Nambari 1 : Sheria na viwango vinavyotumika katika kusimamia utekelezaji wa miradi**




*Chanzo: Uchambuzi wa Sheria, Muongozo na Viwango vya Upimaji wa Kazi za Ujenzi kwa Afrika Mashariki toleo la kwanza la 1970 uliofanywa na wakaguzi, 2023*

## 2.3 Majukumu na Wajibu wa Wahusika Wakuu

### 2.3.1 Wajibu wa watendaji wakuu katika utekelezaji wa ukarabati wa Miradi

- ***Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo***

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa ukarabati na maboresho ya miundombinu ya Uwanja wa Gombani Pemba.

Wizara inaongozwa na Katibu Mkuu ambaye anaripoti kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Tangu kuanzishwa kwake, Wizara imeanzisha na kutekeleza miradi mbali mbali kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi wa Zanzibar ambapo miradi hiyo imeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2022/2023, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilitumia jumla ya **shilingi Bilioni 5.642** kwa ajili ya ukarabati wa uwanja wa Gombani Pemba. Kati ya fedha hizo **shilingi Bilioni 2.8** zilitumika kwa awamu ya mwanzo ya ukarabati na **shilingi Bilioni 2.842** ikiwa ni ongezeko la gharama (addendum) lililojitokeza katika ukarabati wa uwanja huo.

Utekelezaji wa mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 ya fedha zinazotumika kugharamia mradi huu.

- ***Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA)***

Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makaazi. Kwa mujibu wa Mkataba uliosainiwa kati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wakala wa Majengo Zanzibar inawajibika kufanya majukumu yafuatayo: -

- Kutekeleza majukumu yote muhimu na kuhakikisha viwango na ubora katika utekelezaji wa mradi huo; na
- Kufanya kazi kama mkaguzi kwa niaba na maelekezo ya Wizara na Mtaalamu wa Vifaa vya Michezo, na hasa itajumuisha: -
    - Kufanya kazi kama Mwakilishi wa Wizara kwenye eneo la ujenzi na kuripoti kwa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha ripoti ya maendeleo ya ujenzi;

- Kusimamia shughuli za ujenzi wa kila siku kwenye eneo la ujenzi na kuhakikisha kazi ya mkandarasi inafanyika kwa mujibu wa mpango kazi ulioidhinishwa, na ubora kulingana na vipimo na makisio ya gharama za ujenzi (BoQ);
- Kusimamia kama mwakilishi wa Wizara na uratibu wa shughuli za ujenzi chini ya mkataba, kwa kupokea Madai ya Mkandarasi, kupitia na kutoa maoni au ushauri kwa maandishi kwa Mshauri na Wizara; na
- Kama Wakala wa Kazi, ZBA itakuwa na jukumu la kukagua kwa mujibu wa makisio ya gharama za ujenzi (BoQ) na maagizo ya kupima tofauti ambayo yana athari za kifedha na kutoa maoni kwa maandishi kwa Mshauri na Wizara.

### 2.3.2 Fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo (kufanya ukarabati na uboreshaji wa Uwanja wa Gombani) Pemba

Utekelezaji wa mradi huo uligharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 kama ilivyofafanuliwa katika Jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 1: Mgawanyo wa Bajeti kwa mwaka 2020/2021 - 2022/2023**

| Mwaka wa Fedha | Bajeti ya maendeleo ya viwanja vya michezo (Tsh) | Bajeti ya ukarabati wa Uwanja wa Gombani (Tsh) | Kiasi cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya ukarabati wa uwanja wa Gombani (Tsh) | Asilimia ya kutolewa kwa fedha (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2020/2021 | NIL | NIL | NIL | - |
| 2021/2022 | 7,000,000,000 | 2,400,000,000 | NIL | - |
| 2022/2023 | 7,000,000,000 | 3,000,000,000 | 2,312,570,917 | 77 |
| 2023/2024 | 34,000,000,000 | NIL | NIL | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi juu ya Taarifa ya Bajeti, 2023*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa, kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha, kuanzia 2020/2021 hadi 2022/2023, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilipokea fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Gombani katika mwaka mmoja tu wa fedha ambao ni 2022/2023 sawa na asilimia 77 ya fedha zilizopangwa kutolewa kwa mwaka huo. Hata hivyo, kiasi kilichotolewa kilikuwa ni kidogo ikilinganishwa na gharama za jumla ya mkataba.

### 2.3.3 Majukumu ya wahusika wengine katika utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa Uwanja

Majukumu ya wahusika wengine katika ukarabati wa Miundombinu ya Uwanja wa Michezo wa Gombani Pemba yamebainishwa kwa muhtasari kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Majukumu ya Wahusika wengine**

| Wahusika | Majukumu | Matarajio / Bidhaa / Huduma |
|---|---|---|
| Wizara ya Fedha | Utoaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. | Upatikanaji wa fedha kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. |
| Tume ya Mipango | Kupanga na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. | Kupata mashirikiano mazuri katika utekelekezaji wa miradi. |
| ZEMA | Kuhakikisha kunakuwepo na usimamizi imara wa mazingira katika eneo la utekelezaji wa mradi. | Kupungua kwa vitendo vya uharibifu wa mazingira. |
| Mshauri Elekezi wa Mradi | Kusimamia utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa masharti ya mkataba. | Ubora wa kazi, Mradi kukamilika kwa wakati na kwa mujibu wa masharti ya mkataba. |
| Karani | Kuiwakilisha Wizara kuhusu masuala yote ya kiufundi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi. | Ubora wa kazi, Kukamilika mradi ndani ya muda kwa mujibu mkataba |
| Mkandarasi wa Mradi | Kuwajibika kwa utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa mkataba | Ubora wa kazi, Mradi wa Kukamilisha ndani ya mkataba |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwa Wahusika wa Mradi,2023*

Mahusiano ya wahusika wakuu (key stakeholders) ni kama inavyooneshwa katika picha hapo chini: -

**Picha Nambari 2: Muhtasari wa Mahusiano kati ya wahusika wakuu**




*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Sheria na miongozo ya Vipimo vya Kazi za Ujenzi Toleo la 1970, 2023*

## 2.4 Mchakato wa Utekelezaji wa Mradi

### 2.4.1 Mchakato wa Utekelezaji wa Mradi uliyokaguliwa

Mchakato wa utekelezaji wa miradi kuanzia hatua ya awali ya kuanzishwa kwa mradi, hatua ya kutolewa kwa fedha, hatua ya ununuzi kupitia usimamizi wa mkataba. Muhtasari wa mchakato wa utekelezaji wa mradi ni kama ifuatavyo:

## Jadweli Nambari 3: Mchakato wa utekelezaji wa mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani

| Hatua | Shughuli zilizofanyika | Matarajio ya Matokeo | Taasisi Husika |
|---|---|---|---|
| Kuandaa Mpango na Kusanifu Mradi | Kupanga mbinu za kutekeleza mradi pamoja na kufanya usanifu wa mradi | Kutayarishwa kwa Vipimo na viwango vilivyoandaliwa kwa utekelezaji wa mradi | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| Mchakato wa kufanya ununuzi na mikataba kwa wakandarasi, washauri, bidhaa na huduma kwa miradi | Mpango wa Ununuzi wa Mwaka;<br>Mahitaji ya Ununuzi kwa ajili ya kazi na huduma za ushauri;<br>Utiaji saini wa mkataba. | Mwaka na miradi ya ununuzi;<br>Upatikanaji wa fedha na uthibitisho wa mahitaji;<br>Mkandarasi wa kazi na mshauri wa usimamizi; Na Mkataba. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| Makisio, Utoaji na utumiaji wa fedha za mradi | Kuandaa mpango wa biashara;<br>Utoaji wa fedha; na<br>Uthibitisho wa matumizi ya fedha | Fedha za miradi ya kila mwaka;<br>Kutegemea fedha za miradi ya kila mwaka;<br>Upatikanaji wa fedha za miradi ya kila mwaka; | Idara ya Michezo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| Utekelezaji wa mradi | Upangaji wa kazi za Ujenzi kwa Mkandarasi;<br>Usimamizi wa Ujenzi na Mshauri; na malipo ya mwajiri. | Utekelezaji wa mradi kwa gharama za mradi;<br>Mradi umekamilika ndani ya muda uliopendekezwa;<br>Mradi unatekelezwa kwa ubora unaotarajiwa. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Washauri na Wakandarasi |
| Mazingira, usalama na athari za kijamii | Usajili wa mradi na ZEMA;<br>Maandalizi ya mazingira, na kuchukuwa tahadhari za kiusalama;<br>Utekelezaji wa mipango iliyopangwa ya kupunguza athari za kiusalama. | Ulinzi wa mazingira;<br>Usalama wakati wa ujenzi;<br>Ulinzi wa afya ndani na nje ya miradi. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ZEMA, Washauri na Wakandarasi. |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi juu ya Mchakato wa Utekelezaji wa Mradi, 2023*

Muhtasari wa mchakato huo ni kama unavyoonekana katika picha hapo chini: -

### Picha Nambari 3: Ukarabati wa Uwanja wa Gombani




*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Awamu za Mradi, 2023*

## 2.5 Taarifa na maelezo ya Mradi

Sehemu hii inatoa taarifa fupi za mradi juu ya maeneo yote ya wajibu wa watendaji kuelekea utekelezaji wa Mradi. Mradi huu ni kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani ambapo muhtasari wa taarifa hizo ni kama inavyoonekana hapo chini: -

### 2.5.1 Taarifa ya Mradi

Mradi huu ni moja kati ya miradi mikubwa iliyofanyika Pemba ukiwa na lengo la kufanya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Chake Chake Pemba.

Upeo wa Mkataba wa Matengenezo ya Miundombinu ya Uwanja vya Michezo Gombani Pemba ni kama ifuatavyo: Kazi za Umeme, Kazi za utoaji wa huduma, Huduma za TEHAMA, Kupaka rangi, Ubao wa Kuonesha Matokeo ya Magoli na taa za kwenye minara. Maelezo juu ya Mkataba wa Huduma ya Ushauri yanawasilishwa katika jadweli hapo chini:

## Jadweli Nambari 4: Taarifa ya Mradi kuhusu Mkataba wa Mshauri Elekezi

| | |
|---|---|
| Jina la Mkataba: | Huduma za Ushauri elekezi kuhusu usanifu na usimamizi wa ukarabati wa miundombinu ya Uwanja wa Michezo Gombani. |
| Nambari ya Mkataba: | SMZ/J03/W/RCB/2021 – 22/20 |
| Mteja: | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| Mfadhili: | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| Mshauri Elekezi: | Diamond Builders Limited Consulting Firm |
| Gharama za Mkataba: | TZS 161,000,000 |
| Tarehe ya Kusaini: | Julai, 2022 |
| Tarehe ya Kutolewa: | Julai, 2022 |
| Muda wa Mkataba: | miezi nane (8) |
| Tarehe ya Kukamilisha: | Baada ya miezi 8 tangu tarehe ya kuanza |

Vile vile, taarifa za mradi huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 5: Taarifa ya Mkataba wa Kazi ya Mradi

| | |
|---|---|
| Jina la Mkataba | Matengenezo ya Miundombinu ya Uwanja wa Michezo Gombani Pemba (Ukarabati na maboresho ya Uwanja) |
| Nambari ya Mkataba | SMZ/SO1/W/RCB/2021 – 22/20 |
| Mwajiri | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| Mfadhili | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| Mshauri | Diamond Builders Limited Consulting Firm |
| Mkandarasi | Salem Construction Company Ltd na JV OSAJU Company Ltd. |
| Utiaji saini wa Mkataba | 13 Julai, 2022 |
| Tarehe ya Umiliki wa Eneo | 19 Julai, 2022 |
| Tarehe ya Kutolewa | Tarehe 21 Oktoba, 2022 kulingana na Ripoti za Maendeleo ya Kila Mwezi na 27 Julai, 2022 kulingana na Masharti Maalum ya Mkataba. |
| Tarehe ya Kukamilisha Kazi ya Mradi | Tarehe 6 Disemba, 2022 kulingana na Ripoti za Maendeleo ya Kila Mwezi na tarehe 15 Disemba, 2022 |
| Kipindi cha Matayarisho | Wiki 4 |
| Tarehe ya marekebisho ya Kukamilisha Kazi | 31 Oktoba, 2023 |
| Kipindi cha Mkataba | Siku 180 za kalenda (wiki 26) |
| Kiwango cha zuio (Retention) | 10% ya thamani ya kazi za Hati ya Malipo ya Muda |

| | |
|---|---|
| Malipo ya awali | 20% ya bei ya Mkataba kulipwa mara tu baada ya kusaini mkataba na baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali. |
| Kipindi cha Uangalizi wa Mradi (defects liability period): | Miezi 12 |
| Mwanzo wa Tarehe ya Kipindi cha Uangalizi wa Mradi | Bado haijafikiwa |
| Tarehe ya Kukabidhi (Mwisho wa Kipindi cha Uangalizi wa Mradi). | Bado haijafikiwa |
| Hati ya Malipo ya Awali | TZS 560,000,000 (Pamoja na VAT) |
| Kiasi cha malipo ya Mkataba wa Awali: | TZS Bilioni 2.8 (Pamoja na VAT) |
| Fedha za Malipo | Shilingi ya Tanzania |
| Ongezeko la Muda Uliopewa | Hadi Oktoba, 2023 |
| Ukomo wa Ongezeko la bei ya Mkataba | Kazi ya ziada isiyozidi 15% ya mkataba wa awali sawa na shilingi 420,191,600 imeidhinishwa. |
| Riba kwa malipo yaliyocheleweshwa | - |
| Hali ya sasa (Julai, 2023) | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika taarifa za mkataba*

Zaidi ya hayo, taarifa za Mkataba kati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na ZBA ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 6: Taarifa za Mkataba wa Usimamizi wa mradi kati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA)

| | |
|---|---|
| Jina la Mkataba | Kusimamia Ukarabati wa Miundombinu ya Uwanja wa Michezo Gombani Pemba |
| Nambari ya Mkataba | SMZ/J03/W/RCB/2021 – 22/20 |
| Tarehe ya Kusaini Mkataba | 6 Januari, 2023 |
| Mteja / Mwajiri | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| Karani | Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) |
| Kipindi cha Mkataba | 15 Disemba 2022 hadi 15 Julai 2023 au kipindi kingine chochote kama inaweza baadaye kukubaliwa na wahusika kwa maandishi |

| | |
|---|---|
| Kiasi cha mkataba (Malipo kwa Karani wa Kazi) | TZS 20,000,000/- |
| Malipo yaliyofanywa kwa ZBA hadi sasa | Hakuna malipo yaliyotolewa hadi sasa |
| Ratiba ya Malipo | Kulingana na hadidu rejea (ToR) |
| Masharti ya Malipo | Malipo yatafanywa kwa 50% kabla ya siku 30 baada ya kuwasilishwa na Mshauri ankara kwa nakala kwa Mratibu. Hadidu Rejea nambari 4.3 inahitaji awamu ya kwanza ya 50% kulipwa kwa Karani wa kazi baada ya kusainiwa kwa makubaliano. Awamu ya pili ya 25% itafanywa kwa 70% ya maendeleo ya kazi. Awamu ya tatu ya 20% itafanywa baada ya ripoti ya mwisho kupitishwa na uongozi. Sehemu ya mwisho ya 5% italipwa baada ya kumalizika kwa kipindi cha Uangalizi wa Mradi. |
| Mratibu | Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Utafiti |




# SURA YA TATU





# 3.0 MATOKEO YA UKAGUZI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi juu ya vipengele vya usimamizi wa mkataba vinavyohusika katika kutathmini utoshelevu wa michakato ya usimamizi wa mradi kama vile muda, gharama na ubora wa utekelezaji wa mradi. Vipengele vya usimamizi wa mkataba vinaelezea usimamizi, tathmini na ufuatiliaji wa wakandarasi na washauri elekezi, utumiaji wa rasilimali zilizoainishwa katika nyaraka za Mkataba, kufungwa kwa mradi na kuzinduliwa. Pia inahusisha kuangalia uhusiano wa kazi kati ya wahusika wote wanaohusika katika mradi huo.

## 3.2 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusiana na Uanzishwaji na Mipango

### 3.2.1 Hatua ya Uanzishwaji na Upangaji wa Mradi

Sehemu hii inaeleza matokeo kuhusiana na mchakato wa Uanzishwaji na Mpango wa mradi wa ukarabati na maboresho ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba. Sehemu hii hutoa maelezo juu ya uanzishaji wa mradi na upangaji, muundo na vipimo kwa madhumuni ya zabuni na utekelezaji wa mradi. Baadhi ya dosari zilizobainika ni kama ifuatavyo: -

**(a) Makisio ya fedha yasiyoridhisha katika Upangaji na Uanzishwaji wa Mradi**

Kifungu nambari 43(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba mahitaji yote ya ununuzi au uondoaji yanatakiwa kufanyika kukiwa na uthibitisho kwamba kiasi kamili cha fedha kwa kipindi kinachotakiwa zinapatikana au zitapatikana baada ya kuingia mkataba.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu za fedha zilizoelekezwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi na kubaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi ni shilingi Bilioni 2.4. Hata hivyo, ukaguzi umebaini hakukuwa na fedha zilizoingizwa katika kipindi hicho cha uanzishwaji wa mradi.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilitenga bajeti ya shilingi Bilioni 3 kwa ajili ya mradi huo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla ya shilingi Bilioni 2.3 ziliingizwa na kutumika sawa na asilimia 77 ya bajeti, na hiki ndicho kipindi ambacho mkataba wa kazi ulisainiwa wenye thamani ya shilingi Bilioni 2.8 (Pamoja na VAT), Mkataba wa Huduma za Ushauri Elekezi (Diamond Builders Limited) ulisainiwa wenye thamani ya shilingi Milioni 161 (Pamoja na VAT), na Mkataba wa Huduma ya Ushauri kwa Karani wa Kazi (ZBA) ulisainiwa wenye thamani ya shilingi Milioni 20 ukitengeneza jumla ya shilingi bilioni 2.981. Hali hii imesababishwa na kutokuwepo kwa mipango imara ya usimamizi wa mradi kwa Wizara ***(Rejea jadweli nambari 1).***

Kukosekana kwa mpango mzuri wa fedha za mradi kunaweza kupelekea athari ya kutopatikana fedha kwa wakati kutoka Serikalini jambo ambalo linaweza kusababisha hatari ya mradi kuchelewa kukamilika kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuandaa mipango imara ya kuanzisha miradi na kuhakikisha utekelezaji miradi inayopangwa inazingatia bajeti halisi ya Wizara ili kuepuka hatari ya kutokukamilika kwa wakati na hatimae kupelekea ongezeko la gharama za ziada.

### (b) Kutokufanyika kwa Tathmini ya kutosha kuhusu mahitaji ya ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Pemba

Ukaguzi ulipitia taarifa mbali mbali za mradi na kubaini kwamba mradi wa ukarabati na uboreshaji wa Uwanja wa Gombani Pemba ulipangwa na kuanzishwa na Serikali ili kutimiza matakwa ya sera na mpango wake wa kuboresha miundombinu ya michezo kwa wananchi wake.

Aidha, kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba KIM/KIM.1/VOL.11/88 ya tarehe 31 Mei, 2021 imeonesha kwamba kuwa Kamishna wa Michezo kama moja ya Idara ya mtumiaji aliomba fedha kutoka kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Gombani. Katibu Mkuu alipeleka ombi hilo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni na Bodi kuamua kufanya mkutano tarehe 4 Juni, 2021 ambapo wajumbe walifahamishwa juu ya kazi ya ukarabati.

Wajumbe wa bodi ya zabuni walijadiliana kuwa, njia ya ununuzi katika zabuni itaamuliwa katika kikao kinachofuata cha Bodi ya Zabuni baada ya kupatikana fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi kwa mujibu wa makadirio katika gharama za makisio ya ujenzi.

Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi unaoonyesha kuanzishwa kwa mradi huo kabla ya kupokea barua kutoka kwa Kamishna wa Michezo.

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara haikufanya tathmini ya kutosha ya kuangalia mahitaji na bajeti ya utekelezaji wa mradi jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa ufanisi katika mipango iliyopangwa ya miradi.

Aidha, kutokana na kutofanyika maamuzi mazuri katika mipango na upeo wa utekelezaji wa mradi na vile vile kuwepo kwa dosari katika matayarisho ya mkataba ya mwanzoni kumepelekea bajeti iliyopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kuwa hafifu kutokana na bajeti hiyo kuzingatia mahitaji ya kazi tu na sio kujumuishwa pamoja na gharama za Mshauri elekezi kwa ajili ya Usimamizi mzuri wa mradi.

Kutofanyika kwa tathmini ya kutosha ya mahitaji kumesababishwa na ukosefu wa wafanyakazi wenye taaluma ya kiufundi ndani ya taasisi ambao wangeweza kutoa mwongozo sahihi juu ya masuala muhimu/ shughuli zinazopaswa kufanyika katika mradi ili kupatikana utekelezaji mzuri wa mradi.

Tathmini duni iliyofanyika kwa mahitaji ya mradi imesababisha kuwepo kwa mapungufu katika maandalizi na usanifu wa mradi hasa katika kuingiza masuala yote muhimu ya shughuli zinazoweza kufanyika wakati wa utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kufanya mambo yafuatayo: -

- Kuhakikisha kuwa katika miradi inayokuja kunakuwepo na wataalamu wenye sifa za kiufundi (Technical Personnel) ili kutoa miongozo ya kiufundi katika hatua za upangaji wa miradi.
- Kwa kuwa mradi bado unaendelea, Wizara kuhakikisha inatumia vyema Taasisi ya ZBA kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kusimamia ukarabati wa Uwanja wa Gombani.
- Kuhakikisha inatumia washauri elekezi wenye uwezo na sifa za kitaalamu katika hatua za upangaji wa mradi ili kuepuka hatari zinazoweza kutokea kutokana na mipango duni ya mradi inayosababishwa na wataalamu wasio na sifa.

### (c) Kutokufanyika kwa matayarisho ya mahitaji ya Wizara kabla ya kufanyika kwa makisio ya gharama za Ujenzi (BoQ)

Taratibu zilizobora zinaeleza kwamba mteja atatoa mahitaji maalum ambayo yatazingatiwa katika upangaji na usanifu wa miradi. Mahitaji hayo maalum hutarajiwa kuonesha suala zima la nafasi inayohitajika katika ujenzi, ubora wa kazi, gharama na wakati.

Licha ya kuwepo kwa hadidu rejea iliyomtaka Mshauri elekezi kufanya mapitio ya BoQ iliyoandaliwa na Mshauri huyo huyo, ukaguzi ulibaini kwamba hakukuwa na mahitaji maalum yaliyotoka katika Wizara kwa ajili ya Matengenezo na Maboresho ya Miundombinu ya Uwanja wa Michezo Gombani Pemba ambayo yalitumika kama muongozo katika maandalizi ya (BoQ) ya awali.

Kukosekana kwa Mahitaji kutoka katika Wizara kwa ajili ya makisio ya awali ya gharama za Ujenzi kumepelekea kutokufahamika kwa mahitaji halisi ya kazi za matengenezo ya ukarabati wa uwanja kutoka kwa Wizara.

Hali hii pia ilithibitika kupitia dosari mbalimbali zilizokuwa zikijitokeza na kuwasilishwa katika Wizara kutoka kwa Mshauri Elekezi, ambapo dosari hizo zimeonekana wakati wa hatua ya utekelezaji kutokana na uwepo wa mahitaji duni ya utekelezaji wa mradi kutokana na ukosefu wa wataalamu wenye sifa za kitaalamu katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wenye uwezo wa kutoa miongozo wakati wa hatua za upangaji wa mradi.

Kukosekana kwa mahitaji ya Wizara kwa ajili ya maandalizi ya awali ya BoQ kumesababisha kuwepo kwa tofauti ambazo zimeonekana wakati wa hatua ya utekelezaji zilizosababishwa na mahitaji duni ya utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuwashirikisha wataalamu wenye sifa za kiufundi kuanzia hatua ya upangaji wa mradi ili kuhakikisha kuwa upangaji na usanifu wa mradi unazingatia matakwa ya Wizara husika.

### (d) Kukosekana kwa Ripoti ya Upembuzi Yakinifu

Taratibu zilizobora zinahitaji upembuzi yakinifu kufanyika katika miradi ili kubaini ikiwa miradi inayotaka kutekelezwa inafaa au haifai kwa miradi ya uwekezaji wa kijamii au kifedha ili kuamua uwezekano wake wa mafanikio.

Mapitio ya taarifa za Mradi yalibainisha kuwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi huo haukufanyika jambo ambalo limepelekea kutokuwepo kwa tathmini ya mradi katika hali ya kiuchumi, kifedha, kijamii, na kimazingira.

Upembuzi yakinifu haukufanyika kutokana na kutokuwepo kwa miongozo imara katika kufanya matayarisho ya mradi kwa hatua za awali. Hii ni kwa sababu, Wizara ilishirikisha mshauri binafsi na kufanya matayarisho ya BoQ pekee wakati masuala mengine muhimu ya mradi kama vile kiuchumi, kifedha, kijamii na mazingira hayakutathminiwa.

Kukosekana kwa Ripoti ya upembuzi yakinifu juu ya ukarabati wa Uwanja wa Gombani kumesababisha kufanyika kwa maamuzi yasiyo sahihi juu ya kiwango cha kazi za ukarabati, hali halisi ya shughuli zinazofanyika wakati wa kazi za matengenezo, na usanifu wa mradi jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa matumizi makubwa ya fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa unafanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi ili kuwezesha mipango, muundo na usanifu mzuri wa mradi.

### (e) Kukosekana kwa Tathmini ya Mradi

Tathmini ya mradi ni mchakato wa kutathmini kwa njia iliyopangwa, hali ya kuendelea na mradi au pendekezo la mradi. Mara nyingi inafanyika kwa kulinganisha mambo mbalimbali, kutumia tathmini ya kiuchumi au mbinu nyingine ya uchambuzi wa uamuzi[1].

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba tathmini ya mradi kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Gombani haikufanyika.

Ukaguzi umebaini hakukuwa na tathmini iliyofanywa ya kulinganisha mambo mbalimbali, kwa kutumia tathmini ya kiuchumi au mbinu nyingine ya uchambuzi katika maamuzi yaliyofanyika ya ukarabati wa Uwanja wa Gombani.

Kutofanyika kwa tathmini ya mradi kumesababisha utekelezaji usio na ufanisi wa mradi uliopelekea ucheleweshaji wa kukamilika kwa mradi, na gharama kubwa kutokana na tofauti zilizojitokeza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kufanya tathmini ya kina kwa kulinganisha vigezo mbalimbali ikiwemo vya kiuchumi au mbinu nyingine za uchambuzi ili kuhakikisha unapatikana utekelezaji mzuri wa mradi na kuepuka kujitokeza ucheleweshaji wa kukamilika kwa mradi, ubora mzuri na kuingia gharama kubwa kutokana na tofauti hizo.

1 MEDS-044B1E.p65 (egyankosh.ac.in)

### (f) Kutokujumushwa kwa Matayarisho ya Usanifu wa Mradi katika upeo wa Huduma za Ushauri Elekezi

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Hadidu Rejea (ToR) kuhusiana na upeo wa utekelezaji wa mradi inahitaji kuhusisha utoaji wa huduma utakaojumuisha matayarisho ya BoQ, usimamizi na ukaguzi katika hatua zote za mradi, msaada na ushauri wakati wa zabuni, na usimamizi wa kipindi cha uangalizi wa mradi na usimamizi wa ujenzi wa kazi hadi kukamilika kwa mradi.

Hadidu rejea ilionyesha zaidi kuwa huduma hiyo itajumuisha ukarabati wa uwanja uliopo Gombani na utafikia eneo la asili la uwanja lililojengwa kutokana na mita za mraba zilizopo.

Ukaguzi ulibaini kuwa huduma ya ushauri inaitwa "Huduma za Ushauri wa usanifu na usimamizi wa Kudumisha Uwanja wa Michezo wa Pemba", hata hivyo, upeo wa huduma ya ushauri elekezi kulingana na hadidu rejea haukujumuisha maandalizi ya usanifu na kwamba mshauri amekuwa akizingatia kipengele cha usanifu katika malipo kinyume na mahitaji ya hadidu rejea.

Hii imethibitishwa na ombi la malipo lililowasilishwa na kulipwa ambalo lilionyesha kuwa mshauri alikuwa akiomba malipo kwa utoaji wa huduma za ushauri, kusanifu uwanja na usimamizi jambo ambalo hakukuwa na shughuli za usanifu zinazozalishwa na mshauri kama vile michoro na nyenginezo.

Sababu ya kumlipa mshauri kwa kipengele cha usanifu wakati hakuna usanifu wowote wa uwanja ni kutokana na usimamizi duni wa mkataba baina ya Wizara na ZBA (Karani wa Kazi).

Kumlipa mshauri kwa shughuli ambazo hajatekeleza ni upotevu wa fedha za Serikali ambazo zinaweza kutumika kufadhili shughuli zingine.

## 3.3 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusiana na Ununuzi

Sehemu hii inatoa tathmini ya mchakato wa ununuzi na mkataba wa Washauri Elekezi na Wakandarasi kwa mradi ili kubaini kama michakato na mkataba wake ulifanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni husika za manunuzi.

Mapitio ya kumbukumbu za manunuzi yalibaini kwamba michakato ya ununuzi wa Mshauri wa Usimamizi wa Ujenzi na Makandarasi, kwa kiasi fulani, ilifanyika kulingana na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Kanuni zake za 2020. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu mbali mbali katika michakato ya ununuzi kama ilivyoelezwa hapa chini.

### 3.3.1 Mchakato wa manunuzi kuhusu upatikanaji wa Mkandarasi

Ukaguzi ulibaini uwepo wa udhaifu katika mchakato wa manunuzi kuhusu upatikanaji wa Mkandarasi kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba. Maelezo ya kila udhaifu yamebainishwa katika vifungu vifuatavyo: -

#### (i) Uzingatiaji wa Udhibiti wa Gharama wakati wa Ununuzi na ufanyaji wa Tathmini ya zabuni kwa Mkandarasi Mkuu

Kanuni nambari 119 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2020, inaitaka taasisi inayofanya manunuzi kuhakikisha kuwa zabuni zinalinganishwa kati yao ili kubaini gharama ya chini kabisa ya tathmini ya ununuzi wa bidhaa, kazi au huduma au bei iliyopimwa zaidi ya ukusanyaji wa mapato.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kuwa, makubaliano ya mkataba baina ya mkandarasi na Wizara yaliyofungwa kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba yalifanyika kwa awamu mbili.

Awamu ya kwanza na ya pili ya uandaaji wa Nyaraka za zabuni ilionyesha kuwa, makubaliano ya mkataba yalifanyika katika mwaka wa fedha 2021-2022 kupitia taratibu za zabuni za ushindani wa kimataifa kama ilivyoainishwa katika Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, Zabuni ilitangazwa katika Gazeti la Zanzibar Leo la siku Alhamisi 21 Oktoba, 2021 ambayo iliwaalika wakandarasi waliosajiliwa daraja la 1 na 2 kwa ajili ya ujenzi (Kazi ambazo ni pamoja na kazi za Umeme, Kazi za huduma, huduma za ICT, Uchoraji, Ubao wa Kuonesha Matokeo na Mnara wa Taa), ambapo Wakandarasi 10 walinunua hati ya zabuni na wakandarasi watatu tu walirudisha hati ya zabuni iliyojazwa mnamo tarehe 5 Novemba, 2021.

Hata hivyo, ukaguzi haukupatiwa nyaraka za tathmini nzima ya zabuni kwa awamu ya kwanza ikiwa ni pamoja na nyaraka ya tathmini ya uwezo wa mzabuni. Lakini kupitia barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) ya kumbukumbu namba MUUMU. BA.97/383/04/52 ya tarehe 14 Machi, 2022, Katibu Mkuu alishauriwa kuwa utaratibu mzima wa manunuzi ufutwe na kurudiwa kwa kufuata njia na taratibu sahihi zitakazokidhi muda na mahitaji ya Uwanja wa Gombani kwa mujibu wa sheria na kanuni za manunuzi.

Awamu ya pili ya manunuzi, tarehe 26 Machi, 2022 Bodi ya Zabuni ilikubaliana njia ya makubaliano ya mkataba itakayotumika ni Zabuni za Ushindani zilizozuiliwa (RCB) na sio Zabuni za Ushindani wa Kimataifa (ICB) kutokana na upungufu wa muda wa utekelezaji wa mradi.

Kuanzia tarehe 14 Aprili, 2022 nyaraka za Zabuni kwa awamu ya pili zilitolewa kwa wakandarasi 9 bila malipo na tarehe 11 Mei, 2022 wazabuni wawili tu waliwasilisha zabuni hiyo kwa Wizara. Nyaraka za zabuni zilifunguliwa tarehe 20 Mei, 2022 na tarehe 25 Mei, 2022 kamati ya tathmini ilianza tathmini ya zabuni kisha ripoti ya tathmini ilipendekeza M/S Salem Construction Limited JV Osaju Company Limited kuwa zabuni ya chini kabisa ya tathmini ya kupewa mkataba.

### (ii) Kutokuwepo kwa mipango imara ya kifedha kwa mradi

Kifungu nambari 42 (1) (a) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza Taasisi inayofanya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma katika kila mwaka wa fedha kwa tarehe iliyoamuliwa na Mlipaji Mkuu, kuandaa na kuwasilisha Mpango wake wa Manunuzi wa Mwaka kwa Mlipaji Mkuu na kwa Mamlaka ili kuepuka ununuzi wa dharura kwa hali yoyote iwezekanavyo.

Kupitia sheria hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi umebaini kuwa kulikuwa na mgao mdogo wa fedha ambapo mpango wa manunuzi ulionesha kiasi kilichopangwa kutumika kwa ajili ya mradi huo ni shilingi Bilioni 2 badala ya shilingi Bilioni 2.8 kama kiasi cha mkataba ambacho Wizara iliingia na Mkandarasi M/S Salem Construction Company Limited JV M/S Osaju Company Limited.

Vile vile, mapitio ya mpango wa ununuzi wa mwaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yalionyesha kuwa hakukuwa na mpango wa ununuzi katika ukarabati wa uwanja wa Gombani kwa mkandarasi ambao uliingizwa unaoweza kuongeza upungufu wa fedha katika mpango wa ununuzi wa mwaka uliyopita, hali hii ni kutokana na kutokuwepo kwa mipango ya kutosha kwa mradi.

Kuwepo kwa uhaba wa fedha kunaweza kusababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi kutokana na fedha zisizotosheleza za ujenzi. Aidha, inaweza kusababisha malipo ya riba, hasara na gharama wakati hati za malipo ya muda yaliyothibitishwa hayalipwi kwa wakati kutokana na kutojumuishwa kwa kiasi kilichobaki katika mipango ya kila mwaka ya miaka inayofuata.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara katika miradi ijayo kuhakikisha unafanya makadirio yote ya gharama za mradi na unajumuisha makadirio kwa mujibu wa Sheria ya nambari Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2016.

### (iii) Tofauti ya Idadi ya Wazabuni kati ya Ripoti ya Tathmini ya zabuni na Fomu ya kutoa zabuni kwa Hati ya Zabuni

Mapitio ya ripoti ya tathmini ya zabuni ya matengenezo ya miundombinu ya Uwanja wa michezo Gombani Pemba ya tarehe 25 Mei, 2022 yalibainisha kuwa ripoti ya tathmini imeonyesha wazabuni 12 walipewa hati ya zabuni kwa ajili ya mradi uliopendekezwa kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 7: Majina na Anwani ya Wazabuni ambao walibainishwa na kupewa Hati za Zabuni kulingana na Ripoti ya Tathmini**

| Namba | Jina la Mzabuni | Anwani |
|---|---|---|
| 1 | M/S Rans Company Limited | P.O.Box 3267 Zanzibar |
| 2 | M/S CSI Construction | P.O.Box 96 Dar Es Salaam |
| 3 | M/S Quality Building Contractors Limited | P.O.Box 2089 Zanzibar |
| 4 | M/S Salem Ujenzi Limited | P.O.Box 3398 Zanzibar |
| 5 | M/S Mazurui Building Contractors Limited | P.O.Box 1143 Zanzibar |
| 6 | M/S Estim Construction Company Zanzibar | P.O.Box 19716 Dar Es Salaam |
| 7 | M/S Advent Construction Limited | P.O.Box 132 Dar Es Salaam |
| 8 | M/S Dezo Civil Contractor Company Limited | P.O.Box 139 Dar Es Salaam |
| 9 | M/S WCEC Limited | P.O.Box 34619 Dar Es Salaam |
| 10 | M/S Humprey Ujenzi Limited | P.O.Box 6107 Arusha |
| 11 | M/S Suma JKT Construction Company Limited | P.O.Box 1694 Dar Es Salaam |
| 12 | M/S Mohammedi Builders Limited | P.O.Box 38439 Zanzibar |

*Chanzo: Uchambuzi wa Ripoti ya Tathmini ya zabuni uliofanywa na Wakaguzi,2023*

Mapitio zaidi yalifanyika kwa fomu iliyosainiwa na wakandarasi waliopewa hati za zabuni na kubaini kwamba wakandarasi 9 tu ndio waliopewa hati za zabuni badala ya wakandarasi 12 kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Tathmini ya Zabuni. Maelezo ya wakandarasi 9 ni kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 8: Majina na Anwani ya Wazabuni ambao walipewa Hati za Zabuni kulingana na Fomu ya Utoaji wa Zabuni

| Namba | Jina la Mzabuni | Tarehe ya kutoa nukuu | Jina la Mtu aliyepewa Hati ya Quotation / Zabuni |
|---|---|---|---|
| 1 | M/S Quality Building Contractors Limited | 15/04/2022 | Abeid A. Said |
| 2 | M/S Salem Construction Limited | 15/04/2022 | Amarido |
| 3 | M/S Mazurui Building Construction Limited | 16/04/2022 | Himly A. Nasoor |
| 4 | M/S Dezo Civil Contractor Company Limited | 16/04/2022 | Jabir Muhdini |
| 5 | M/S Rans Company Limited | 16/04/2022 | - |
| 6 | M/S Advent Construction Limited | 19/04/2022 | Mungu wa Diana |
| 7 | M/S Mohammedi Builders Limited | 19/04/2022 | |
| 8 | M/S Humprey Construction Limited | 19/04/2022 | Ricky Nkya |
| 9 | M/S Estim Construction Company Zanzibar | 19/04/2022 | Vinesh P Miruni |

*Chanzo: Fomu ya Toleo la Hati za Zabuni zilizopitiwa tarehe 14 Aprili 2022*

Jadweli nambari 7 linaonesha kuwa wazabuni 12 walipatiwa hati za zabuni wakati Jadweli nambari 8 likionyesha kuwa ni wazabuni 9 tu waliopewa hati za zabuni za Matengenezo ya Miundombinu ya Viwanja vya Michezo Gombani Pemba.

Ukaguzi ulibaini kuwa wazabuni watatu wa ziada ambao hawakujumuishwa katika fomu ya utoaji wa hati za zabuni walitokana na tathmini duni ya nyaraka za zabuni na kamati ya tathmini ya zabuni ambayo ilisababisha mkanganyiko wa ripoti ya tathmini ya zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo, kunakuwa na usawa na uwazi katika tathmini za zabuni.

#### (iv) Kutokuzingatiwa kwa vigezo vya mwisho (Post Qualification) katika kuwapata wazabuni

Kifungu nambari 33 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Afisa Masuuli, Bodi ya zabuni, Kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Idara husika na kamati ya tathmini zitafanya kazi zake bila ya kuingiliwa kulingana na kazi na uwezo wao, na katika Kanuni nambari 133(12) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2020, ambayo inasema kwamba kutalazimika kufanyika uhakiki wa vigezo vya mwisho (Post Qualification) katika kuwapata wazabuni kwa kupitia kamati ya tathmini.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba WHVUM/MUUMU/22/16/VOL.1/68 ya tarehe 9 Machi, 2022 na kupitia mahojiano ya afisa mwandamizi kutoka Wizarani, ukaguzi ulibaini kwamba kamati maalum iliyoundwa na Bodi ya zabuni kwa ajili ya kuangalia vigezo vya mwisho katika kuchagua zabuni haikuwa ni sehemu ya kamati ya tathmini ya zabuni bali ilikuwa ni wajumbe wa kamati ya bodi ya zabuni akiwemo Mhandisi Mkaazi kwa wakati huo jambo ambalo limepelekea Bodi ya zabuni kutoa mapendekezo ya mshindi wa Zabuni hali iliyoathiri majadiliano ya idhini ya tuzo ambazo baadae zilifutwa na Afisa Masuuli wa Wizara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa kunakuwa na uzingatiaji mzuri wa sheria na kanuni za manunuzi katika usimamizi na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya Wizara.

### (v) Kutokuwepo kwa Mpango wa Majadiliano (Negotiation Plan) katika vikao vya Majadiliano

Kanuni nambari 135(5)(a) za Kanuni za manunuzi wa Umma ya 2020 inazitaka timu za majadiliano kuandaa mpango wa majadiliano ambao utabainisha masuala yatakayojadiliwa kama yalivyoainishwa katika ripoti ya tathmini na malengo yatakayofikiwa na kila inapowezekana, kupima malengo na kuweka vigezo vya juu na vya chini vya majadiliano ambavyo Bodi ya Zabuni itaidhinisha mpango wa majadiliano kabla ya mazungumzo.

Mapitio ya Mkataba yamebainisha kuwa vikao vya majadiliano vilifanyika katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar tarehe 7 Juni, 2022 na vile vile kumbukumbu za vikao vya majadiliano ziliandaliwa. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa malengo ya majadiliano hayo hayakutajwa. Aidha, hakukuwa na ushahidi uliotolewa ili kuthibitisha kwamba mpango wa majadiliano uliandaliwa na kupitishwa na bodi ya zabuni.

Kutokuwepo kwa mpango wa majadiliano kunaweza kupelekea kushindwa kupatikana kwa ufanisi wakati wa kikao cha majadiliano kinachofanywa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara katika miradi ijayo kuhakikisha kuwa mipango ya mazungumzo inaandaliwa kabla ya mkutano wa mazungumzo.

### (vi) Kupewa Kazi ya Mkataba kwa Mkandarasi ambae hakua na sifa

Kanuni nambari 85(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2020 inasema kuwa Taasisi ya Ununuzi na Utoaji wa Zabuni itatathmini sifa za wazabuni kwa mujibu wa vigezo na taratibu za kufuzu zilizowekwa katika nyaraka za kabla ya kufuzu, ikiwa zipo, na katika nyaraka za zabuni au nyaraka nyingine za kufanya zabuni au nukuu.

Kupitia barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar yenye kumbukumbu namba MUUMU. BA.97/383/04/52 ya tarehe 14 Machi, 2022 kuhusu mapendekezo ya zabuni yenye zabuni namba WHVUM/MUUMU/22/16/VOL.1/68, moja ya sababu ambayo Mamlaka ilitoa kwa Wizara ili utaratibu mzima wa ununuzi wa zabuni ufutwe na kurudiwa ni "Moja ya kampuni katika ubia (Salem Construction Company Limited JV Osaju Company Limited) haikufikia vigezo vya usajili kama inavyotakiwa na hati ya zabuni iliyotolewa kwa wazabuni". Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar (ZCRB) na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) usajili wa Salem na Osaju wote wamesajiliwa kama wakandarasi. Maelezo ya usajili kwa wakandarasi hao wawili yamewasilishwa katika jadweli hapo chini.

## Jadweli Nambari 9: Maelezo ya Usajili chini ya ZCRB na CRB

| Namba | Jina la Mkandarasi | Aina ya kazi inayosajiliwa | Taasisi ya Kusajili | Daraja la Usajili | Nambari ya Usajili | Tarehe ya Usajili |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | M/s Osaju Company Limited | Mkandarasi wa Kazi Za Kiraia | ZCRB | 5 | C-V/0089/04/2021 | 15/04/2021 |
| 2. | M/S Salem Construction Company | Mkandarasi wa Ujenzi | ZCRB | 1 | | 19/01/2012 |
| 3. | M/S Salem Construction Company | Mkandarasi wa Ujenzi | CRB | 1 | B1/0125/9/12 | 20/09/2012 |
| 4. | M/S Salem Construction Company | Mkandarasi wa Kazi Za Umeme | CRB | 2 | E2/0013/1/10 | 7/01/2010 |
| 5. | Kampuni ya Ujenzi ya M/S Salem | Mkandarasi wa Kazi za Kiraia | CRB | 3 | C3/100/06/2016 | 8/06/2016 |

*Chanzo: Tathmini ya Thamani ya Zabuni zilizowasilishwa na Kampuni ya Ujenzi ya M/S Salem JV M/S OSAJU Company Limited iliyofanywa na Wakaguzi*

Mahitaji ya nyaraka za zabuni yanahitaji wakandarasi wanaostahiki waliosajiliwa katika daraja la 1 la mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kazi ikiwa ni pamoja na Kazi za Umeme, Kazi za Huduma, Huduma za TEHAMA, Uchoraji, Ubao ya Alama na Taa za Mnara.

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa, Salem Construction Company Limited inamiliki daraja la 1 kama mkandarasi wa ujenzi na daraja la 2 kama Mkandarasi wa Umeme na daraja la 3 kama Mkandarasi wa Kazi za Kiraia wakati Osaju anamiliki daraja la 5 kama Mkandarasi wa Kazi za Kiraia. Hata hivyo, maelezo kuhusu daraja la usajili kama Mkandarasi wa Kazi za Umeme hayapo jambo ambalo limesababisha utendaji duni wa kazi kutokana na kwenda kinyume na vigezo na mahitaji ya hati ya zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unazingatia mahitaji ya nyaraka za zabuni zinazotolewa kwa wazabuni na maelezo rasmi ya ufafanuzi yatolewe kwa wazabuni wote kabla ya kuwasilisha zabuni na fomu za ufunguzi wa nyaraka za zabuni ili kuepuka kutoa zabuni kwa wakandarasi wasiokuwa na sifa.

### (vii) Uingiaji wa mkataba bila ya kuwepo kwa ufafanuzi wa gharama za ziada katika makisio ya gharama za ujenzi

Kifungu nambari 9.1 na 9.2 cha Maagizo kwa Wazabuni kinaeleza kwamba kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Zabuni, Taasisi ya Ununuzi na uondoshaji kwa sababu yoyote, ikiwa kwa mpango wake mwenyewe au kwa kujibu kutokana na ufafanuzi ulioombwa na mzabuni, inaweza kurekebisha hati ya zabuni kwa kutoa nyongeza ya mkataba (addendum) ambapo nyongeza yoyote itakayotolewa itakuwa sehemu ya nyaraka za zabuni na itawasilishwa kwa njia ya maandishi au baruapepe kwa wote ambao wamenunua nyaraka za zabuni moja kwa moja kutoka kwa Taasisi ya Ununuzi na uondoshaji.

Katika kikao cha awali cha kuanza zabuni na ziara ya kutembelea eneo la ujenzi ambayo ilifanyika tarehe 22 na tarehe 23 Aprili, 2022 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa ajili ya mapendekezo ya matengenezo na maboresho ya miundombinu ya Uwanja wa Michezo wa Gombani Pemba, miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa na kukubaliwa baina ya Wizara na Mkandarasi ni hoja za ufafanuzi ambazo zilifanywa kwa BoQ ya Mkataba na nyaraka za zabuni kuwa ni sehemu ya hati ya zabuni zenye alama ya ufafanuzi katika hati ya mkataba kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 2**.

Kuingia katika mkataba bila ya kuzingatia maelezo ya awali ya zabuni kunaweza kusababisha kujirudia kwa shughuli za mradi zilizopangwa kutokana na tofauti zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi jambo ambalo limepelekea uwepo wa kazi za ziada zilizozidi asilimia 15 ya gharama za mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa, shughuli zote zilizo nje ya mkataba haziwasilishwi kwa Wizara kama kazi za ziada kwani ziliunda sehemu ya mkataba kupitia mkutano wa awali kabla ya kusainiwa kwa mkataba.

### 3.3.2 Mchakato wa kumpata Mshauri Elekezi

#### (i) Mchakato usioridhisha wa kumpata Mshauri Elekezi wa Uwanja wa Gombani

Kifungu nambari 13 cha Masharti ya Hadidu Rejea (ToR) kilitaka manunuzi ya mshauri yafanyike kwa kutumia Njia ya Ununuzi wa Chanzo Kimoja na Mshauri alitakiwa kuchaguliwa kupitia utaratibu wa Consulting Qualification Selection (CQS) kama inavyoelezwa katika Sheria Nambari ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Kwa mujibu wa Kanuni nambari 4(2)(d) ya Kanuni za manunuzi ya Umma za 2020 Maafisa wote wa umma wakiwemo Maafisa Masuuli na Wajumbe wa Bodi za Zabuni, wakati wa kufanya au kuidhinisha manunuzi wataongozwa na misingi ya uadilifu, uwajibikaji na uwazi katika mchakato wa ununuzi.

Kwa mujibu wa Kanuni nambari 5(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2020 Maafisa wa Umma, wajumbe wa Bodi za Zabuni na Maafisa Masuuli, wakati wa kufanya au kuidhinisha manunuzi watachagua taratibu zinazofaa na kusababisha manunuzi kufanyika kwa weledi, tija na ufanisi.

Katika mapitio ya mapendekezo ya Ununuzi kwa Huduma za Ushauri kwa Matengenezo ya miundombinu ya Uwanja wa Michezo wa Gombani Pemba ukaguzi ulibaini kuwa taarifa ya Barua ya Tuzo ilitumwa kwa Kampuni ya Ushauri ya M/S Diamond Builders Limited ikiitaarifu kampuni ya Ushauri kwamba zabuni yake ya tarehe 1 Aprili, 2022 kwa Huduma za Ushauri imepokelewa na kutathminiwa ambapo Mshauri Elekezi ametakiwa ndani ya siku 3 kuthibitisha kukubali na kuwa tayari kwa ajili ya kuanza kazi.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa utaratibu uliotumika kwa kumpata mshauri elekezi huyo haukuzingatia matakwa ya Sheria namba 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa kutokuzingatiwa hali ya ushindani katika upatikanaji wa Mshauri Elekezi ambapo ilibainika Mshauri Elekezi kuthibitisha kukubali kwake kufanya kazi mnamo tarehe 20 Aprili, 2022 ikiwa ni siku 3 tangu kupatiwa barua ya kuthibitisha kukubali kwake. Hata hivyo zabuni ya kampuni iliyotathminiwa, ripoti kamili ya tathmini ya zabuni na idhini ya Ripoti ya Tathmini ya Zabuni iliyotayarishwa na Bodi ya Zabuni hazikupatikana kwa ukaguzi.

Kukosekana kwa nyaraka nilizozibainisha hapo juu kunatoa taswira ya kwamba mchakato wa ununuzi wa huduma za ushauri ulikosa ushindani na haukuwa wa haki jambo ambalo limepelekea kutokuwepo kwa uwazi katika mchakato wa kumpata mshauri elekezi. Pamoja na uwepo wa dosari hizo mambo yafuatayo yamebainika: -

**(ii) Manunuzi ya huduma kutoka kwa Mshauri Elekezi ambayo hayakuwa katika Mpango wa Ununuzi wa Mwaka**

Kifungu nambari 42(7) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinahitaji manunuzi yasifanyike nje ya mpango wa manunuzi isipokuwa katika hali ya dharura na ya haraka.

Mapitio ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 yalibainisha kwamba ununuzi na uondoshaji wa huduma ya ushauri kwa uwanja wa Gombani haukuwa kwenye mpango mkuu wa mwaka wa manunuzi wa miaka hii.  Maafisa waliohojiwa wa Wizara hiyo walisema kuwa sababu ya kutojumuishwa kwa huduma ya ushauri katika mpango wa manunuzi wa mwaka ni kwamba huduma ya ushauri iliingizwa katika kazi za ukarabati ndani ya mkataba wa kazi, hata hivyo, bajeti iliyozingatiwa ilikuwa tu kutumika kwa shughuli zote chini ya mkataba wa kazi tu.

Ukaguzi umebaini kwamba kutojumuishwa kwa mkataba wa huduma ya ushauri katika mpango mkuu wa mwaka wa manunuzi kulitokana na mipango duni ya usimamizi wa mradi jambo ambalo limepelekea uwepo wa matumizi ya fedha ambazo hazikukusudiwa kwa ajili ya utoaji wa huduma ya ushauri.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaongeza umakini katika kupanga, kusimamia na kufuatilia vipengele vyote vya mkataba ikiwa ni pamoja na kujumuisha bajeti ya gharama za huduma za mshauri elekezi katika mpango wake wa manunuzi wa mwaka kwa miradi ijayo.

### (iii) Wizara kuingia Mkataba wa Huduma ya Ushauri Elekezi bila uthibitisho wa upatikanaji wa fedha

Kifungu nambari 43(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba mchakato wa ununuzi au uondoshaji utafanyika au utaendelea tu kwa uthibitisho kwamba fedha, kwa kiasi kamili kwa kipindi kinachotakiwa, zinapatikana au zitapatikana wakati mkataba utakapofungwa.

Ukaguzi ulipitia kumbukumbu za mradi na kubaini kwamba hakukuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha wakati mkataba ulishafungwa.

Ukosefu wa uthibitisho wa fedha wakati wa ufungaji wa mkataba hauleti taswira njema ya ufadhili mzuri wa mradi jambo ambalo huwenda likapelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa wakati au kujitokeza kwa ongezeko la gharama linalotokana na kupanda kwa thamani ya bidhaa au kujitokeza tozo kutokana na kuchelewa kufanya malipo kwa wakandarasi kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha shughuli zote za miradi zilizopangwa kutekelezwa zinajumuishwa katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa mradi na kuepusha kujitokeza kwa ongezeko la gharama nje ya mpango wa bajeti ya mradi.

### (iv) Kukosekana kwa idhini ya manunuzi kutoka kwa Afisa Masuuli

Kanuni nambari 43(1) ya Kanuni za manunuzi ya Umma za 2020 inahitaji manunuzi yoyote yanayofanywa na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji kuidhinishwa na Afisa Masuuli.

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na ushahidi unaoonyesha kuwa zabuni ya huduma za ushauri elekezi kwa ajili ya ukarabati na maboresho wa Uwanja wa Gombani iliidhinishwa na Afisa Masuuli.

Kukosekana kwa idhini ya Afisa Masuuli kunapelekea uwepo wa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma unaotokana na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unasimamia vizuri mchakato wa manunuzi unaofanywa na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Uondoshaji (PDMU) ili kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo kunakuwa na ufanisi katika mchakato wa manunuzi.

### (v) Kukosekana kwa idhini ya Hati ya zabuni ya mkataba wa Huduma za Mshauri Elekezi kwa Bodi ya Zabuni

Kanuni nambari 43(2)(b) ya Kanuni za Manunuzi za Umma ya 2020 inaitaka Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kabla ya kutangaza zabuni, kwanza kuipeleka kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kupata idhini yake: hati ya zabuni ikiwa ni pamoja na vipimo au maelezo ya riba na masharti ya hadidu rejea, zabuni nyingine au mapendekezo.

Mapitio ya majalada ya ununuzi yalionyesha kuwa hakukuwa na ushahidi wa idhini ya hati ya zabuni ikiwa ni pamoja na maelezo kutoka kwa bodi ya zabuni kwa ajili ya ununuzi wa huduma za mshauri elekezi katika usimamizi wa ukarabati wa uwanja wa Gombani. Hali hii imetokana na Mradi kushindwa kutunza kumbukumbu vizuri kutokana na uhamisho wa wafanyakazi katika Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Uondoshaji.

Kuendelea kuwahamisha watendaji wa mradi kunapelekea uwezekano wa kukosekana kwa nyaraka muhimu za utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kunakuwepo utunzaji mzuri wa kumbukumbu za nyaraka zote za manunuzi.

### (vi) Kukosekana kwa Ripoti ya Tathmini ya Zabuni kwa huduma ya Mshauri Elekezi

Kifungu nambari 45(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, kinaitaka Bodi ya Zabuni kupitia tathmini na mapendekezo yaliyowasilishwa na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Uondoshaji na kuweza: (a) kuidhinisha mapendekezo hayo; (b) kupendekeza tuzo ya mkataba kwa Afisa Masuuli; au (c) kukataa kuidhinisha mapendekezo ya tuzo ya zabuni na kupeleka tathmini kwa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Usambazaji na sababu za kutathmini upya zabuni, kurudia tena au hatua nyingine.

Katika mapitio ya nyaraka za mradi ukaguzi ulibaini hakukuwa na uthibitisho wa mapendekezo ya Ripoti ya Tathmini ya Zabuni iliyowasilishwa na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na uondoshaji kwa bodi ya zabuni kwa ajili ya kuthibitisha. Hali hii ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Kukosekana kwa taarifa kutoka kwa Bodi za zabuni ambazo zinaweza kuongezwa kwenye hati ya zabuni ili kuboresha hati hizo kunaweza kupelekea kukosekana kwa uwazi na haki katika uandaaji wa nyaraka za zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaweka utunzaji mzuri wa kumbukumbu za nyaraka zote za manunuzi pamoja na kuhakikisha kwamba ripoti za thathmini ya zabuni zinaidhinishwa na Bodi ya Zabuni.

## 3.4 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusiana na Usimamizi wa Mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo ya ukaguzi kutoka kwa vipengele vya usimamizi wa mkataba kama ilivyopimwa wakati wa ukaguzi katika matengenezo ya uwanja wa michezo Gombani Pemba. Upeo wa Mkataba wa Matengenezo ya Miundombinu ya Uwanja wa Michezo Pemba unaojumuisha Kazi za Umeme, Huduma za kufanya kazi, Huduma za TEHAMA, Uchoraji, Bango la Kutangaza matokeo, Taa za minara na kazi nyingine. Zifuatazo ni dosari ambazo zimebainika katika utekelezaji wa miradi hiyo: -

### 3.4.1 Usimamizi wa Mkataba wa Kazi

Ukaguzi umebaini uwepo wa udhaifu katika usimamizi wa mkataba wa kazi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba. Baadhi ya dosari zilizobainika katika usimamizi wa mkataba wa kazi ni kama zifuatazo: -

#### (i) Vigezo hafifu vya mradi

Kwa mujibu wa Fomu ya Mkataba Kifungu cha (2) ambayo imetaja aina ya nyaraka ambazo zitasomwa na kufafanuliwa kama sehemu ya makubaliano na moja ya nyaraka zilizotajwa ni nyaraka ya vigezo. Mapitio ya Mkataba wa ukarabati wa uwanja wa Gombani yaligundua kuwa hakukuwa na nyaraka kamili ya vipimo na vigezo kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba, hati pekee ya vipimo iliyoambatanishwa ilikuwa kwa maelezo ya ziada ya ubao wa alama wa Kieletroniki wa LED kama ilivyokubaliwa katika hadidu rejea za mazungumzo ya mapatano.

Ukaguzi umebaini baadhi ya vipimo vilitolewa katika hati za makisio ya gharama za ujenzi (BoQ) vitu vingi muhimu vimekosekana kutokana na uwepo wa ubunifu wa mradi kutokana na kutojitosheleza kwa mchoro wa utekelezaji wa mradi.

Kukosekana kwa nyaraka za vipimo maalum kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kumepelekea uwepo wa upungufu wa taarifa juu ya ubora wa vifaa, kazi na bei katika nyaraka za zabuni jambo ambalo linaweza kusababisha utekelezaji wa mradi katika kiwango cha chini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kunakuwepo ubunifu na usanifu katika uandaaji wa miradi ijayo ili kupatikana lengo lililokusudiwa.

### (ii) Kukosekana kwa Masharti Maalum ya Mkataba

Mapitio ya Masharti Maalum ya Mkataba kwa Mkataba Namba SMZ/SO1/W/RCB/2021-22/20 imebainika kuwa kuna baadhi ya vifungu vya Masharti Maalum vya Mkataba vinakinzana na kile kilichokubaliwa katika mazungumzo ya tarehe 7 Juni, 2022 kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 10: Kupingana na Masharti Maalum ya Mkataba na Majadiliano katika Mkataba Namba SMZ/ SO1/W/RCB/2021-22/20**

| Kifungu cha SCC | Jinsi SCC ilivyosema | Hadidu rejea za Mazungumzo |
|---|---|---|
| GCC 51.1 | Ukomo wa uhifadhi utakuwa 20% ya bei ya mkataba | Ukomo wa uhifadhi utakuwa 5% ya bei ya mkataba |
| GCC 1.1 (W) | Tarehe ya kuanza itakuwa tarehe 27/07/2022 na<br>Tarehe ya kukamilika kwa kazi yote itakuwa: 15/12/2022 ambayo hufanya (Siku 142) | Mkandarasi alikubali kufanya ukarabati kwa kipindi kisichozidi miezi mitano (5) kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa mkataba, 13/7/2022 na kukamilika 27/12/2022 ambayo inafanya (Siku 148) |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkataba Namba. SMZ/SOI/W/RCB/2021-22/20 uliofanywa na wakaguzi, 2023*

Jadweli hapo juu linaonesha kipengele cha Masharti Maalum ya Mkataba ukaguzi ulibaini uwepo wa Ukomo wa uhifadhi wa asilimia 20 ya bei ya mkataba wakati wa makubaliano ukomo wa uhifadhi utakuwa asilimia 5 ya bei ya mkataba.

Aidha, kipengele cha Masharti Maalum ya Mkataba kilionyesha tarehe ya kuanza ujenzi ni tarehe 27/07/2022 na tarehe ya kukamilika kwa ujenzi huo ni 15/12/2022 ambayo inafanya jumla ya siku 142, wakati baada ya mazungumzo kwamba Mkandarasi ataanza kutekeleza ukarabati kwa kipindi kisichozidi miezi mitano (5) kutoka tarehe ya kusaini mkataba 13/07/2022 ambapo tarehe ya kukamilisha mkataba huo ni tarehe 27/12/2022 ambayo inafanya Siku 148 na sio kama ilivyoelezwa katika kipengele cha Masharti Maalum ya Mkataba.

Hali hii inasababisha mchaganyiko katika kutekeleza mradi kutokana na kutokuzingatiwa mazungumzo ya awali na Mkandarasi jambo ambalo lingeweza kubadilisha masharti maalum yaliyomo ndani ya mkataba

Aidha, ukaguzi ulibaini uwepo wa vipimo vya usalama wa utendaji katika masharti maalum ya mkataba chini ya kifungu cha 55.1 ambacho kinaeleza kuwa Usalama wa Utendaji utakuwa kiwango cha chini sawa na asilimia 0.10 ya bei ya mkataba na dhamana ya benki isiyokuwa na masharti sawa na shilingi 2,800,000 ambacho ni kiasi kidogo ukilinganisha na kiasi cha jumla cha mkataba kwa mradi uliopendekezwa.

Mapitio zaidi ya kifungu cha 1.1 cha kipengele cha Masharti Maalum ya Mkataba yanaeleza kuwa msimamizi wa mradi ni Bodi ya Usajili ya Wakandarasi Zanzibar (ZCRB) na M/S Diamond Builders Limited lakini Maafisa Waandamizi kutoka Wizara waliohojiwa tarehe 12 Julai, 2023 walisema kuwa ZCRB sio msimamizi wa mradi kama ilivyoelezwa katika SCC, msimamizi wa mradi aliyepewa mkataba ni Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na Diamond Builders Limited.

Hata hivyo, ukaguzi ulipatiwa nakala ya mkataba kati ya Wizara na M/S Diamond Builders Limited wakati ulipotembelea katika eneo la ujenzi kwa ajili ya ukaguzi. Aidha, mkataba kati ya Wizara na ZBA ulipatikana baada ya kurudi kutoka eneo la ujenzi.

Kutokuzingatia vya kutosha kwa vipengele Masharti maalum ya mkataba kunaweza kusababisha utekelezaji wa mradi katika kiwango kisichoridhisha jambo ambalo linapelekea kukosekana haki kupitia mchakato wa zabuni ambao unanyima fursa kwa wazabuni kujiingiza katika mchakato wa ununuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo kunakuwa na maandalizi ya kutosha kupitia masharti maalum ya mkataba ili kufikia lengo lililokusudiwa.

### (iii) Dosari iliyobainika katika Hati ya Dhamana (Hati ya Uwakala)

Hati za zabuni zinahitaji wakandarasi wanaostahiki ambao wamesajiliwa katika madaraja ya 1 na 2 ya mkataba wa ujenzi wa kazi (kazi ikiwa ni pamoja na Kazi za Umeme, kazi za huduma, Huduma za TEHAMA, Uchoraji, Ubao wa matokeo na Taa za Mnara).

Ukaguzi ulipitia hati ya dhamana iliyotolewa kwa mujibu wa mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ/SO1/W/RCB/2021-22/20 na kubaini kwamba Bw. Ussi Salum Juma Pondeza ambae ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya M/S Osaju Limited na amesajiliwa katika daraja la 5 katika kazi za ukandarasi ambae amepewa hati ya dhamana kwa ajili ya kupewa mamlaka kamili ya kufanya chochote kwa mujibu wa (JV AGREEMENT) katika utekelezaji wa zabuni nambari SMZ/SO1/W/RCB/2021-22/20.

Ukaguzi umebaini kuwa hati ya dhamana ya Wakala iliyotolewa haikustahili kwa mujibu wa mahitaji ya nyaraka za zabuni kwa kufanya hivyo, kunapelekea shughuli zote za mkataba huo zitaendeshwa na mkandarasi ambaye hana sifa kulingana na mahitaji ya hati ya zabuni.

Kutolewa kwa dhamana kwa kampuni ya M/S Osaju Company Limited ni kuruhusu shughuli za mradi kusimamiwa na mkandarasi asiye na sifa kwa mujibu wa nyaraka ya zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba katika miradi ijayo wanazingatia vigezo vya hati ya Uwakala ili kuweza kumpata Mkandarasi mwenye sifa zinazokidhi.

### (iv) Miradi iliyosimamiwa na Wakandarasi wasiokuwa na Hati ya Dhamana

Hati ya dhamana iliyotolewa kwa ajili ya mashirikiano baina ya Kampuni ya M/S Salem Construction Limited na M/S Osaju Construction Company Limited iliidhinisha kampuni ya Osaju Contstruction Company Limited ambapo hati hiyo ilimteua Ussi Salum Pondeza ambae ni Mkugurenzi Mkuu wa M/S Osaju Construction Company Limited na kuidhinishwa kuwa ndio mshirika mkuu katika mkataba huo.

Ukaguzi ulibaini kuwa hati ya dhamana iliyotolewa ilimtaka muhusika kuchukuwa hatua zote muhimu zilizoainishwa katika mkataba na kufanya jambo jengine lolote ambalo limeainishwa katika mkataba wa ujenzi wenye nambari ya usajili SMZ/SOI/W/RCB/2021-22/20 kwa ajili ya Matengenezo ya Miundombinu ya Uwanja wa Michezo wa Gombani Pemba.

Hata hivyo kampuni ya M/S Salem Construction ilibainika kufanya maombi mbali mbali ikiwemo maombi ya malipo ya gharama za ujenzi, maombi ya malipo ya ghrama za ziada pamoja na maombi ya ongezeko la muda jambo ambalo limepelekea kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa mikataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba miradi inasimamiwa ipaswavyo na wahusika waliopata dhamana kwa mujibu wa utaratibu uliobainishwa.

**(v) Kukosekana kwa vigezo vya jumla na vigezo maalum vya mradi**

Ukaguzi ulitathmini uhalali wa mikataba na kukagua nyaraka za mkataba (Fomu ya Mkataba, Barua ya Kukubalika, zabuni ya Mkandarasi, Masharti maalum ya Mikataba (SCC), Masharti ya Jumla ya Mikataba (GCC), Vigezo vya jumla, Vigezo Maalum, Michoro, BOQ, mazungumzo ya awali ya mkataba) ikiwa yamesainiwa na kupigwa muhuri na pande zote katika kila ukurasa wa mwanzo. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa nyaraka za mkataba zilikosa maelezo (Maelezo ya jumla na maelezo maalum).

Kukosekana kwa vigezo vya jumla na maalum ni kutokana na muundo duni wa mradi ambao haukuzingatia vegezo vya mradi husika.

Kukosekana kwa vigezo vya mradi kunaweza kusababisha hatari kwa kukosekana kwa msaada juu ya gharama za mradi kwa vifaa, utendaji na kazi. Pia, ukosefu wa vigezo husababisha kushindwa kupunguza hatari za mradi kwa kukosa msaada ikiwa itatokea migogoro yoyote ya kisheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba katika miradi ijayo kuwe na muundo wa kutosha wa mradi ambao unazingatia vigezo na vipimo vya mradi. Pia, Wizara ihakikishe inashirikisha washauri wenye ujuzi na wataalamu wenye sifa katika kubuni miradi.

**(vi) Mapungufu katika ripoti ya utekelezaji wa kazi juu ya shughuli zinazofanyika katika eneo la ujenzi (Ukosefu wa Taarifa juu ya majaribio ya Vifaa)**

Mapitio ya Ripoti za Maendeleo za Kila Mwezi (Januari hadi Juni, 2023) juu ya utekelezaji wa mradi zilibainisha kuwa kulikuwa na taarifa juu ya shughuli zilizofanyika kwenye eneo la mradi. Ripoti zilionyesha katika ukaguzi wa kutathmini shughuli za mradi zinazofanywa katika eneo hilo na ubora na maendeleo ya kazi ambapo ripoti hizo hazikuonesha taarifa kuhusiana na majaribio yaliyofanyika katika zege iliyoingizwa ili kuthibitisha ubora wa baa za chuma zilizoimarishwa na saruji iliyowekwa katika sehemu tofauti kama vile besi za mnara, boriti kwa milango ya choo. Hali hii ilisababishwa na usimamizi usioridhisha wa mkataba baina ya Mshauri, Mkandarasi na Wizara.

Kutokufanyika kwa vipimo kunaweza kukapelekea kutokuwa na uhakika wa uimara wa nguzo za zege zilizojengwa, nguzo za zege zilizojengwa kwenye milango ya choo pamoja na vikalio vya minara vilivyojengwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa Mshauri anawasilisha matokeo ya vipimo vya saruji alivyotumia ili kupima ubora wa kazi unaolingana na thamani halisi ya fedha iliyotumika ili kunusuru uwezekano wa kuingiza hasara Serikali.

### (vii) Ujenzi wa Kituo (kibanda) cha Transfoma uliofanyika nje ya jengo la uwanja

Mkataba wa makisio ya gharama za vifaa vya ujenzi (BoQ), Bili namba mbili (2) kipengele C ukurasa namba tatu kati ya kurasa 19, kifungu kilimtaka mkandarasi kuingia mkataba wa kutengeneza kituo (kibanda) ambacho kitasambaza umeme kwa kutumia transfoma na vitu vyote vinavyohitajika katika kibanda hicho ili kuweza kufanya kazi.

Wakati wa ziara ya eneo hilo ukaguzi ulibaini kuwa sehemu iliyopendekezwa kujengwa kituo cha usambazaji wa umeme sio sehemu iliyokusudiwa jambo ambalo limetia shaka kutekelezwa kwa makubaliano hayo kwani imebainika transfoma inayotumika inasambaza umeme katika maeneo mbali mbali ya kijamii na umeme kutoka kwenye transforma kwenda kwenye uwanja umeungwa kupitia nguzo kuu za umeme ambapo huwenda ikapelekea kujitokeza kwa upatikanaji wa umeme hafifu kwa ajili ya matumizi ya uwanja.

Aidha, kutokana na uungwaji wa umeme katika sehemu isiyorasmi kwa mujibu wa BoQ ukaguzi uliomba kupatiwa hatimiliki ya sehemu iliyowekwa transfoma, pamoja na uthibitisho unaothibitisha umiliki wa transfoma hiyo kuwa ni mali ya uwanja kwa lengo la kuepusha kujitokeza kwa mizozo baina ya wananchi na Serikali jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupatiwa uthibitisho huo. Picha hapo chini inaonesha transforma iliyojengwa nje ya uwanja kinyume na BoQ.

**Picha Nambari 4: Kituo cha Transforma iliyowekwa juu ya kibanda kwa ajili ya matumizi ya Uwanja**



*Picha ya kituo cha Transfoma kilichojengwa nje ya eneo la uwanja*

Kukosekana kwa ushahidi juu ya umiliki wa transforma kunaweza kusababisha hatari ya kwamba transforma iliyowekwa sio ile inayohitajika kwa mujibu wa mkataba. Vile vile, kuna uwezekano wa kusababisha kujitokeza kwa kodi kutokana na kiwanja kilichotumika hakikuwa na umiliki jambo ambalo linaweza kupelekea Wizara kuingia gharama za ziada zisizotarajiwa ambazo ziko nje ya makubaliano ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unafuatilia kwa karibu jambo hilo ili kunusuru kujitokeza kwa mizozo baina ya Wizara na Wananchi au kuingia gharama za ziada za tozo ya eneo hilo kinyume na matarajio jambo ambalo litaibebesha mzigo mzito Serikali.

### (viii) Mwenendo wa mawasiliano usioridhisha baina ya pande mbili za Mkataba

Mkataba wa kazi unahitaji kwamba mawasiliano yote kutoka kwa mkandarasi yaelekezwe/yapitishwe kwa mshauri ikiwa mawasiliano hayo yako ndani ya uwezo wa mshauri kuamua, mshauri ana uwezo wa kuamua na kutoa taarifa kwa mteja, lakini ikiwa ni katika uwezo wa Mteja mkandarasi anaandika kwa mshauri na mshauri anaandika barua nyingine au barua kwa Mteja akiarifu na kushauri juu ya suala hilo na viambatisho vya Barua kutoka kwa mkandarasi na vinginevyo.

Hata hivyo, mapitio ya majalada ya Mradi na Barua za Mawasiliano zilibainisha kuwa mawasiliano mengi hayakufuata njia sahihi ya mtiririko wa mawasiliano. Hii ilitokana na usimamizi hafifu wa Mshauri Elekezi.

Kushindwa kwa mkandarasi kufuata mtiririko sahihi wa mawasiliano kunaweza kusababisha mgogoro katika mradi kwani mmoja wa wahusika anaweza kuwa hajui maamuzi yaliyotolewa na pande nyengine. Pia, inaweza kusababisha utendaji duni wa kazi na kutopatikana kwa ubora wa kiwango cha juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa Usimamizi wa Mshauri unadhibiti vizuri masharti ya mikataba ikiwemo kipengele cha mawasiliano ili kuwezesha mwenendo sahihi wa mawasiliano.

### 3.4.2 Kuchelewa kuanza kwa mradi

Kwa mujibu wa masharti maalum ya Mkataba (SCC) Kifungu cha 1, GCC 1.1, tarehe ya kuanza ilitakiwa kuwa mnamo 27 Julai, 2022. Hata hivyo, mapitio ya Ripoti za Maendeleo ya kila mwezi za mradi huo yalionyesha kuwa mradi ulianza tarehe 21 Oktoba, 2022, na kuchelewa kwa siku 86 (sawa na miezi mitatu).

Kwa mujibu wa mahojiano na maafisa wa mkandarasi, ukaguzi ulibaini kuwa kuchelewa kuanza kwa mradi huo kulitokana na kuchelewa kutolewa kwa fedha za malipo ya awali kutoka Wizarani. Hata hivyo, mapitio ya kumbukumbu za malipo yalibaini kuwa kuchelewa kwa malipo kulitokana na kuchelewa kwa uwasilishaji wa dhamana ya benki ya malipo ya awali. Vile vile kumbukumbu za malipo zilionyesha kuwa malipo ya awali kwa mkandarasi yalifanyika tarehe 6 Oktoba, 2022 wakati mkandarasi aliwasilisha dhamana ya benki ya malipo ya awali mnamo tarehe 2 Novemba, 2022. Hali hii inaonyesha kuwa mkandarasi alilipwa malipo ya awali kabla ya kuwasilisha dhamana ya benki ya malipo ya awali.

Ukaguzi ulibaini hali hiyo ilitokana na usimamizi duni wa mkataba kwa Mshauri ambapo inaweza kuhakikisha kuwa mkandarasi anawasilisha dhamana ya benki ya malipo ya awali.

Kuchelewa kuanza utekelezaji wa mradi kwa wakati kumepelekea kuathiri malengo ya uanzishwaji wa mradi huo jambo ambalo limeinyima fursa jamii kunufanika na malengo ya uanzishwaji wa mradi huo kama ilivyopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kumuelekeza Mshauri kuweka usimamizi wa kutosha wa mikataba ili kuhakikisha Mkandarasi anatekeleza mradi huo kulingana na matakwa ya mkataba. Vile vile, Wizara inashauriwa kutolipa malipo ya awali bila kupokea dhamana ya benki ya malipo ya awali kutoka kwa mkandarasi ili kuepuka hatari ya kupoteza fedha za Serikali.

### (i) Mabadiliko ya muda wakati wa utekelezaji wa mradi

Kifungu nambari 31 cha GCC (kuongezeka kwa tarehe ya Kukamilika iliyokusudiwa), Kifungu kidogo cha 31.1 kinamtaka Meneja wa Mradi kuongeza tarehe ya kukamilika mradi iliyokusudiwa ikiwa Tukio la Fidia litatokea au tofauti imetolewa ambayo inafanya kuwa vigumu kwa kukamilisha kwa tarehe ya kukamilisha iliyokusudiwa bila mkandarasi kuchukua hatua za kuharakisha kazi iliyobaki, ambayo itasababisha mkandarasi kupata gharama ya ziada.

Mapitio ya Ripoti za maendeleo ya kila mwezi kwa mradi ilionyesha kuwa kulikuwa na tofauti wakati wa kukamilisha mradi kutoka tarehe 15 Disemba, 2022 (kama kwa SCC Kifungu 1, GCC 1.1) hadi tarehe 31 Oktoba, 2023. Hata hivyo, hadi muda wa ukaguzi huo mwezi Julai 2023, mradi haujakamilika na kulikuwa na kasi ndogo ya shughuli za matengenezo.

Ukaguzi huo pia ulibaini kuwa kulikuwa na maombi mawili ya kuongezwa muda ambayo yaliwasilishwa kwa Mteja (Wizara) kupitia mshauri msimamizi na Wizara baada ya kupokea maombi ya kuongezwa muda, iliidhinisha maombi hayo. Maelezo juu ya maombi yaliyowasilishwa kwa Mteja na idhini zilizotolewa zinawasilishwa katika jadweli hapo chini.

### Jadweli Nambari 11: Maelezo kuhusu Ombi la Kuongezwa Muda uliowasilishwa Wizarani na Mkandarasi kupitia Mshauri

| Namba ya Maombi | Tarehe ya Maombi | Tarehe ya kuidhinishwa na Wizara | Muda wa Kupewa | | | Sababu za kuongeza muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya Mwisho | Miezi | |
| 01 | 6/12/ 2022 | | Januari, 2023 | 30/04/ 2023 | 4 | Kuongezeka kwa wigo wa kazi, kuchelewa kwa makabidhiano ya eneo la kazi , na kuchelewa kutolewa kwa malipo ya awali |
| 02 | 03/04/2023 | 27/04/2023 | 01/05/2023 | 31/10/2023 | 6 | Ukuzaji wa wigo wa kazi na malipo ya kuchelewa |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Maombi ya Kuongezwa kwa Muda, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilitoa idhini ya kuongezwa muda baada ya kupitiwa upya kwa ombi la kwanza la kuongezwa muda uliowasilishwa na mkandarasi kupitia mshauri, kwa misingi ya malipo yaliyocheleweshwa, kuchelewa kwa wigo wa kazi pamoja na kuchelewa kukabidhiwa.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kuchelewa kutolewa kwa malipo ya awali kulitokana na kuchelewa kuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya benki isiyokuwa na masharti mara tu baada ya mkataba kusainiwa. Aidha, kupitia ukaguzi wa hati za malipo ulibaini kuwa mkandarasi alifanyiwa malipo kabla ya kuwasilisha dhamana ya benki jambo ambalo ni kinyume na masharti ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo, kunakuwa na maandalizi ya kutosha na ukaguzi wa hati za makisio ya gharama za ujenzi kuanzia hatua ya awali hadi kukamilika kwa mradi.

### *(ii) Tofauti ya asilimia ya malipo iliyojitokeza katika urejeshaji wa malipo ya awali*

Kifungu nambari 54.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba wenye Nambari. SMZ/ SO1/W/RCB/2021-22/20 kilionyesha kuwa urejeshaji wa malipo ya awali (advanced payment) ya kila mwezi ni asilimia 50 kwa LOT 2 kwa mujibu wa kiasi cha malipo kinachotolewa kwa kila hati ya malipo "Interim Payment Certificate". Aidha kwa mujibu wa kumbukumbu za mazungumzo kati ya mkandarasi na kamati ya mazungumzo yaliyofanyika tarehe 7 Juni, 2022 yalikubaliana na utaratibu huo.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya muhtasari uliopitiwa wa Hati za Malipo ya Muda (Interim Payment Certificate No.1) iliyoandaliwa na mshauri kwa mkandarasi na kubaini kuwa asilimia 10 ilitumika kuhesabu kiasi cha malipo ya awali badala ya asilimia 50 ambayo ilielezwa katika Masharti Maalum ya Mkataba na katika kumbukumbu za mazungumzo.

Kutokana na dosari hiyo iliyobainika huwenda ilitokana na usimamizi wa mkataba usioridhisha au kuwepo kwa uwezekano wa Mshauri Elekezi kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kutokutoa ushahidi wa kuhalalisha mabadiliko ya asilimia ya urejeshaji wa malipo ya awali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba unakuwa makini katika kusimamia masharti ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa mchanganyiko wa urejeshwaji kwa kiwango cha asilimia ya fedha inayopaswa kurejeshwa kwa mujibu wa masharti maalum ya mkataba.

### *(iii) Usimamizi wa Gharama za Mradi*

Ukaguzi ulitathmini gharama za mradi wakati wa utekelezaji na kubaini udhaifu kama ilivyoelezwa katika vifungu vifuatavyo: -

**(a) Mkandarasi alilipwa malipo ya awali kiasi cha shilingi 560,000,000 kabla ya kuwasilishwa kwa dhamana ya benki ya malipo ya awali kwa Wizara**

Kifungu nambari 54.1 cha GCC (Kifungu cha 23 cha SCC) kinahitaji kiasi cha malipo ya awali (advanced payment) ya asilimia 20 ya bei ya Mkataba kulipwa mara moja baada ya kusaini mkataba na wakati wa kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali.

Kwa mujibu wa masharti maalum ya mkataba yaliitaka Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo kufanya malipo ya awali ya asilimia 20 ya gharama ya mkataba mara baada ya mkandarasi kuwasilisha dhamana ya benki isiyo na masharti (Unconditional Bank Guarantee), hata hivyo dhamana ya benki isiyo na masharti itaendelea kutumika hadi malipo ya awali yatakapolipwa ambapo kiasi cha dhamana kitaendelea kupungua kadiri mkandarasi atakapofanyiwa malipo.

Ukaguzi ulibaini Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilifanya malipo ya shilingi 560,000,000 bila ya uwepo wa hati ya dhamana ya benki isiyo na masharti maalum jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba. Hali hiyo ilibainika pale mkandarasi alipowasilisha barua ya tarehe 18 Julai, 2022 ya kuomba malipo ya awali na kupokelewa tarehe 15 Agosti, 2022 ambapo Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilifanya malipo ya awali tarehe 6 Oktoba, 2022 wakati hati ya dhamana ya benki isiyo na masharti maaalum ilipokelewa tarehe 2 Novemba, 2022.

Hii inaonyesha kuwa Wizara ilimlipa mkandarasi malipo ya awali kabla ya kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali kinyume na masharti ya mkataba.

Kutokana na uwepo wa usimamizi duni wa mikataba inawezekana ikawa ndio sababu pekee iliyopelekea kufanyika kwa malipo kinyume na makubaliano ya mkataba.

Kufanyika kwa malipo ya awali bila ya kuzingatia uwasilishwaji wa dhamana ya benki huwenda kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pale mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza makubaliano ya mkataba au kutokuwa na uwezo wa kukamilisha kazi alizopewa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba unazingatia masharti maalum yaliyoainishwa katika mikataba pamoja na kuwa na usimamizi mzuri wa malipo yanapofanyika kwa wakandarasi.

**(b) Kutokurejeshwa malipo ya awali**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 54.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba na Kifungu cha 23 cha Masharti Maalum ya Mkataba vinaeleza kwamba mkandarasi alitakiwa kulipa malipo ya awali ya asilimia 50 kwa kila mwezi ya kiasi cha Cheti cha Malipo ya Muda.

Aidha, kifungu nambari 54.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza malipo ya awali yatalipwa kwa punguzo la kiasi cha fedha kutokana na kufanyika kwa malipo ya Mkandarasi kwa mujibu wa ufanyaji wa kazi au ukamilishaji wa kiwango cha kazi, hapatakuwa na malipo yatakayolipwa kwa kuzingatia tathmini ya ukamilishaji wa kazi aliyoifanya.

Kwa mujibu wa kumbukumbu za malipo (Interim Payment Certificate 1) ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 1,099,460,139.79 zimelipwa bila ya mazingatio ya kuzuwia asilimia 50 ya malipo ya awali kwa mujibu wa masharti Maalum ya Mkataba (Interim Payment Certificate) ambayo ni sawa na shilingi 549,730,069.90.

Kutokurejesha kwa malipo ya awali kwa mujibu wa Cheti cha Malipo ya Muda (IPC 1) kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pindipo Mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza masharti maalum ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa mikataba pamoja na uwepo wa Washauri wa Mradi ili kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya ukiukwaji wa utaratibu.

### (c) Malipo yaliyofanywa kwa Dola za Marekani badala ya kutumia Shilingi ya Tanzania kwa Barua ya Mkopo (Letter of Credit)

Kifungu nambari 46.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kwamba malipo yote yafanyike kwa mujibu wa fedha iliyoainishwa katika mkataba vyenginevyo kuwe na uwiano wa sarafu itakayotumika kuwiana na bei ya mkataba.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba WHVUM/TU/29/7/VOL.111/52 ya tarehe 16 Januari, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ilionyesha kuwa Wizara iliomba kiasi cha Dola za Marekani 332,006.89 kwa ajili ya kumlipa mkandarasi wa Matengenezo ya Miundombinu ya uwanja wa Gombani kupitia Mkataba wenye nambari SMZ/S01/W/RCB/2021-22/20 kwa barua ya mkopo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kinyume na mahitaji ya mkataba wa kazi.

Aidha, ukaguzi umebaini Wizara imefanya malipo kwa hati ya malipo yenye nambari za utambuzi wa malipo "DUMMY FOR MAY, 2023 DEVELOPMENT" ya tarehe 10 Mei, 2023 yalionyesha kuwa Wizara ililipa kiasi cha Dola za Kimarekani 332,006.89 jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya mkataba ambayo yalieleza malipo yote yafanyike kwa shilingi ya Kitanzania.

Kutokana na dosari iliyobainika hapo juu huwenda ilitokana na usimamizi usioridhisha wa mkataba unaofanywa na timu ya usimamizi (Diamond Builders Limited na Wakala wa Majengo Zanzibar kama Karani wa Kazi) ambao ungehakikisha unazingatia kwa ufanisi matakwa ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unasimamia ipasavyo ili kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo haifanyi malipo kwa Dola ya Marekani endapo matakwa ya mkataba yataruhusu malipo kwa shilingi za Tanzania.

Aidha, ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuimarisha mfumo wake wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa mshauri anatekeleza majukumu yake kwa weledi na bidii ili kuwezesha usimamizi mzuri wa mkataba.

### (d) Ununuzi wa Bidhaa kupitia Barua ya Mkopo katika Mkataba wa Kazi na bila kuwa na Mkataba na Benki au Benki na Mkandarasi

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba WHVUM/TU/29/7/VOL. 111/52 ya tarehe 16 Januari, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliyoomba malipo ya USD 332,006.89 kwenda Wizara ya Fedha na kuitaka Wizara ya Fedha kufanya malipo bila ya uwepo wa mkataba wowote kati ya benki na Wizara au mkataba kati ya benki na Mkandarasi.

Kutokana na dosari hiyo ukaguzi umebaini kuwa ununuzi wa vifaa katika mkataba wa kazi haukukubaliwa wakati rasimu ya mkataba wa kazi ilipopelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kwa ajili ya uchunguzi, hata hivyo, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilirudisha ununuzi wa vifaa kupitia 'Letter of Credit' katika mkutano wa mazungumzo kati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Mkandarasi jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya mkataba na pia ni kinyume na mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo alikikataa Kipengele cha kufanya matumizi kwa kutumia 'letter of Credit' na kuishauri Wizara kufanya mapitio mapya na marekebisho ya kipengele hicho katika mkataba. Hata hivyo Wizara ilishindwa kutekeleza ushauri wa Mwanasheria Mkuu.

Pamoja na ukweli kwamba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliondoa Kipengele cha ununuzi wa vifaa kupitia Barua ya Mikopo baada ya kuongozwa na Mwanasheria Mkuu (Maelezo juu ya kuingizwa kwa maoni yameambatanishwa katika **Kiambatisho Nambari 3**), ukaguzi umebaini Wizara ilirudisha Kipengele hicho wakati wa mkutano wa mazungumzo kwani mkataba wa mwisho na uliosainiwa wa kazi uliondoa Kipengele hicho.

Kitendo cha Wizara kutozingatia ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wakati wa uwasilishaji wa rasimu ya mkataba au kufanya malipo kwa kuzingatia barua ya Mkopo bila ya kuwa na Mkataba kati ya Wizara na benki au benki na Mkandarasi kinaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pindipo mkandarasi atakaposhindwa kuwasilisha vifaa katika sehemu ya utekelezaji wa mradi.

Pia kunaweza kujitokeza kitendo cha kufanyika kwa malipo ya ziada kwa mkandarasi kwani malipo ya ununuzi wa vifaa yalitathminiwa kwa mazingatio ya makisio ya gharama za vifaa (BoQ) ambapo malipo ya vifaa hivyo hivyo yanaonekana kujitokeza tena katika 'letter of Credit'.

### (e) Kumalizika kwa Dhamana ya Benki ya Malipo ya Awali bila ya kuongeza Muda

Kwa mujibu wa Dhamana ya Benki ya Malipo ya awali yenye kumbukumbu namba 002GTLC222980001iliyotolewa na benki ya Taifa ya Biashara Limited ilimaliza muda wa matumizi tarehe 7 Aprili 2023.

Hata hivyo, katika ukaguzi wa majalada ya Mradi, ukaguzi ulibaini kumalizika kwa muda wa dhamana ya benki ya malipo ya awali ambapo hadi mnamo mwezi wa Julai 2023 ukaguzi ulipokamilika, imebainika mkandarasi hajawasilisha hati mpya ya dhamana wakati ambao mradi haujakamilika na bado unaendelea.

Kutofanywa upya kwa dhamana ya benki ya malipo ya awali kuna athari kwa upotezaji wa fedha za Serikali ikiwa mkandarasi atashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo jambo ambalo linatoa viashiria vya usimamizi duni wa mradi uliofanywa na karani wa usimamizi wa mradi (ZBA) au mshauri elekezi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaimarisha udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi imara wa mikataba katika utekelezaji wa miradi.

### (f) Malipo yaliyolipwa bila ya kuwepo Dhamana ya Benki shilingi 73,043,478.26

Kifungu nambari 54.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kilihitaji kiasi cha malipo ya awali hadi asilimia 20 ya bei ya mkataba na kulipwa mara moja baada ya kusaini mkataba na baada ya kuwasilisha Dhamana ya Malipo ya awali.

Mapitio ya Barua yenye kumbukumbu namba Z194/1.9/1.9.1/01 ya tarehe 2 Novemba, 2022 kutoka kwa Mkandarasi Salem Construction Company Limited kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilionyesha kuwa Mkandarasi aliwasilisha Hati ya dhamana yenye Marejeo namba 002GTLC222980001 iliyotolewa tarehe 25 Oktoba, 2022 na Benki ya Taifa ya Biashara yenye thamani ya shilingi 486,956,521.74.

Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia 20 ya jumla ya mkataba unaofikia shilingi 560,000,000 ulilipwa kwa mkandarasi kwa mazingatio ya hati ya dhamana yenye thamani ya shilingi 486,956,521.74 kukiwa na tofauti ya shilingi 73,043,478.26 na dhamana jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya masharti ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuimarisha mifumo yake ya udhibiti wa ndani ili kuepusha Serikali kuingia hasara kutokana na kutokuzingatiwa kwa hati za dhamana ya benki.

**(g) Malipo yaliyoidhinishwa bila ya kufanyiwa tathmini ya kazi shilingi 1,099,460,139.79**

Kifungu cha 45.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kilimtaka Meneja wa Mradi kuamua thamani ya kazi iliyotekelezwa. Pia, kifungu cha 45.4 kilihitaji thamani ya kazi inayotekelezwa inayojumuisha mchanganuo wa kazi iliyofanywa.

Kwa mujibu wa mapitio ya IPC 1 ya mradi huo ilibainika kuwa malipo ya kazi zilizotekelezwa zenye thamani ya shilingi 1,099,460,139.79 zililipwa bila ya kufanyiwa tathmini ya kazi iliyopimwa kama ilivyoorodheshwa katika makisio ya gharama za kazi. Hii pia ilithibitishwa kupitia hati ya Malipo Namba. J03PV2200001679 ambapo imebainika malipo yaliyofanyika yalilipwa kwa gharama za ujumla kwa kila kazi iliyotekelezwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na mchanganuo wa gharama za kazi iliyofanyika kwa kila kipengele kilichowasilishwa kwa ajili ya malipo, hata hivyo ukaguzi ulibaini kuwa maelezo ya malipo yaliyoandaliwa na mshauri yalikuwa kwa tathmini ya kifedha na sio hesabu ya kazi zilizofanyika.

Kumlipa mkandarasi bila ya kufanya tathmini ya kazi zilizotekelezwa kunaleta hatari ya kumlipa mkandarasi kwa kazi ambazo hazijatekelezwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuweka usimamizi wa kutosha wa mkataba ili kuhakikisha kuwa katika maandalizi yajayo ya IPC, IPCS imetayarishwa kulingana na hesabu ya kazi zilizopimwa na sio kutumia tathmini ya kifedha kuichukulia kama IPC.

### 3.5 Usimamizi wa Tofauti zinazojitokeza kwenye ongezeko la fedha (Addendum)

Ukaguzi wa nyaraka ulionyesha kuwa kulikuwa na tofauti katika utekelezaji wa mradi huo. Maelezo ya tofauti yanawasilishwa katika vifungu vifuatavyo:-

#### 3.5.1 Malipo ya ziada ya shilingi 266,717,200 yaliyopitishwa na Mshauri elekezi bila ya kuidhinishwa na Wizara

Kifungu cha 43.1 cha GCC kinamtaka mkandarasi kumpa Meneja wa Mradi makisio ya gharama ya kuingiza tofauti wakati alipoombwa kufanya hivyo na Meneja wa Mradi. Meneja wa Mradi atafanya tathmini ya makisio ya gharama, ambayo itatolewa ndani ya siku saba (7) za ombi ndani ya kipindi chochote kilichotajwa na Meneja wa Mradi na kabla ya Uthamini (valuation) kuagizwa.

Mapitio ya kumbukumbu za malipo ya Mradi yalionyesha kuwa Meneja wa Mradi alijumuisha tofauti ya shilingi 266,717,200 katika IPC 1 ambayo haikuidhinishwa na Wizara jambo ambalo lilipelekea kuwa na jumla ya malipo ya shilingi 1,099,460,139.79 iliyolipwa kwa hati namba JO3PV2200001679 kinyume na utaratibu.

#### 3.5.2 Malipo ya ziada ya shilingi 411,657,100 yaliyopitishwa tena na Mshauri Elekezi bila ya kuidhinishwa na Wizara

Mapitio ya kumbukumbu za malipo yalionyesha kuwa Mshauri Elekezi aliidhinisha kiasi cha shilingi 658,790,839 kupitia Cheti cha Malipo ya Muda (IPC 2) tarehe 6 Mei, 2023, na kuiomba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kulipa kiasi kilichopendekezwa kwa Mkandarasi.

Mapitio zaidi ya mradi yalionyesha kuwa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kupitia barua yenye kumbukumbu namba CA:57/218/01/71 aliomba malipo ya kiasi cha shilingi 658,790,839 kwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango. Ukaguzi umebaini uwepo wa ziada ya shilingi 411,657,100 ambazo ziliorodheshwa katika Cheti cha Malipo ya Muda nambari 2 jambo ambalo hakukuwa na ushahidi wa kwamba Wizara iliridhia uwepo wa ongezeko la malipo hayo.

Uwepo wa ongezeko la fedha kinyume na utaratibu ulisababishwa na usimamizi usioridhisha wa mkataba, kukosekana kwa mawasiliano baina ya mshauri elekezi na karani wa usimamizi wa mradi (ZBA), kutokuwa na uwelewa wa usimamizi wa miradi kwa Wizara jambo ambalo lilipelekea kufanya malipo bila ya kuwa na utaalamu wa kupitia na kukagua vyeti vya malipo ya kazi vinavyowasilishwa kwa ajili ya malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa Mshauri anasimamia mkataba kwa weledi na ufanisi ili kuhakikisha tofauti hazilipwi bila ya idhini ya Wizara. Pia, mchanganuo wa gharama unaandaliwa kwa shughuli zilizolipwa. Hii ni pamoja na kurejesha tofauti mbili za kulipwa (shilingi 266,717,200 katika Cheti cha Malipo ya Muda 1 na shilingi 411,657,100 katika Cheti cha Malipo ya Muda 2).

### 3.5.3 Usimamizi wa Mkataba wa Huduma ya Ushauri

Ukaguzi ulipitia mkataba wa huduma ya ushauri kwa ajili ya usanifu, usimamizi na ukarabati wa miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba kati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Kampuni ya Ushauri ya M/S Diamond Builders Limited na kubaini mapungufu yafuatayo: -

#### (a) Kukosekana kwa tarehe ya kusaini Mkataba

Mapitio ya Mkataba baina ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Mshauri Elekezi (Consultant) wa utoaji wa huduma za ushauri kwa ajili ya kubuni na kusimamia ukarabati wa miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba namba SMZ/JO3/W/RCB/2021-22/20 yenye jumla ya Mkataba wa shilingi 161,000,000 pamoja na VAT. Ukaguzi ulibainisha kuwa tarehe za kuanza kwa utoaji wa huduma za ushauri hazikubainishwa katika mkataba na pia hakuna hati iliyopatikana kwa ajili ukaguzi inayoonyesha kuwa Mteja na Mshauri walikubaliana mwanzoni tarehe ya kuanza. Mkataba umetaja mwezi na mwaka tu wakati uliposainiwa lakini siku haijatajwa.

Mapitio ya hadidu rejea za mazungumzo kati ya mshauri na kamati ya mazungumzo yalionyesha kuwa mshauri alikubali kufanya kazi kama mshauri wa mradi kwa kipindi ambacho mkandarasi atahitaji kukamilisha kazi hiyo na pia ndani ya muda wote ulioongezwa aliyopewa mkandarasi mara baada ya mkataba kusainiwa.

#### (b) Ukosefu wa Utoaji wa Bima ya Utaalamu (Proffessional Indemnity Insurance) katika Mkataba wa Mshauri

Ukaguzi ulibainisha kuwa mkataba wa utoaji wa huduma za ushauri kwa ajili ya kubuni na kusimamia ukarabati wa uwanja haukuwa na kifungu kinachomtaka Mshauri kumpa mteja bima ya kitaalamu. Vile vile, hadi wakati wa ukaguzi, Julai 2023, Mshauri hakuulizwa kutoa bima jambo ambalo ni kwenda kinyume na utaratibu bora wa miradi ya ujenzi.

Ukosefu wa bima ya kitaalamu (Proffessional Indemnity Insurance) humweka Mteja katika hatari ya kushindwa kwa mradi ikiwa Mshauri atashindwa kutekeleza makubaliano ya mkataba na hatimae itapelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo, utoaji wa vifaa vya bima ya kitaalamu unajumuishwa katika Mkataba wa Huduma ya Ushauri ili kumfanya Mshauri awajibike ikiwa kuna hitilafu za Mshauri.

### (c) Kukosekana kwa shahidi katika sehemu ya Mshauri kwenye Mkataba

Mapitio ya Mkataba wa Huduma ya Ushauri uliosainiwa umebaini kuwa Mkataba huo umesainiwa katika sehemu mbili za Wizara (Katibu Mkuu na kushuhudiwa na Afisa Sheria), hata hivyo, kwa upande wa Ushauri, mkataba umesainiwa na Meneja wa Mradi tu bila kushuhudiwa na afisa mwingine yeyote kutoka Kampuni ya Ushauri.

Kukosekana kwa mashahidi kwa upande wa kampuni ya ushauri kunafanya kutokamilika kwa taratibu za kisheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unasimamia kikamilifu kuhakikisha mikataba yote kuwa na pande zote wahusika zinakuwa na mashahidi katika mkataba. Kwa kuongezea, tarehe halisi ya kusaini mkataba inapaswa kuandikwa vizuri ili kuepusha kujitokeza kwa migogoro ya kisheria.

### (d) Kuchelewa kwa kuanza kwa Huduma za Ushauri

Kwa mujibu wa kifungu nambari 13.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC), Mkataba ulihitaji kuanza kwa huduma hizo kuanzia Julai, 2022.

Mahojiano na maafisa wa Mshauri na Mapitio ya Wahandisi wa Mradi yalibaini kuwa mshauri alianza huduma mnamo Disemba, 2022 na kuchelewa kwa miezi mitano.

Kwa mujibu wa afisa aliyehojiwa wa mshauri alieleza kwamba sababu ya kuchelewa kuanza kwa mradi huo ni kutokana na Wizara kuchelewa kumlipa mkandarasi malipo ya awali ambayo yalilipwa Oktoba, 2022. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba mradi umechelewa kuanza kutokana na mkandarasi kuchelewa kuwasilisha dhamana ya benki ya malipo ya awali (Unconditional) ambapo mkandarasi aliwasilisha dhamana ya benki ya malipo ya awali tarehe 2 Novemba, 2022.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha kuwa mradi ijao inaanza kwa wakati ili kuepuka kuchelewa kukamilika kwa mradi husika.

### *i. Kuchelewa kukamilika kwa Mkataba wa Huduma za Ushauri*

Kwa mujibu wa kifungu nambari 12.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC), muda ulitakiwa kuwa miezi minane kuanzia tarehe ya kuanza kutumika ambayo ni sawa na siku 240 hadi mwisho wa mradi.

Hata hivyo, hadi muda wa ukaguzi huu mnamo Julai 2023, mradi huo bado haujakamilika.

Sababu ya kuchelewa kukamilika kwa mradi ilikuwa kuchelewa kuwasilishwa kwa vifaa ambavyo ni taa kubwa za uwanjani, Njia za riadha (Tartan track), nyasi bandia, na Ubao wa Matokeo kutoka China ambapo ulitengenezwa.

Kuchelewa kwa kukamilika kwa mradi kunaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika miradi ijayo kuhakikisha Mshauri anamsimamia mkandarasi kwa kuhakikisha anapeleka kwa wakati zana/vifaa vilivyoagizwa kutoka nje endapo mkataba wa kazi utahusisha ununuzi wa samani na vifaa.

### *ii. Kutowasilishwa kwa Dhamana ya Malipo ya Awali*

Kifungu nambari 45.1(a)(2) cha SCC cha Masharti Maalum ya Mkataba kilihitaji dhamana ya malipo ya awali kuwa katika kiasi na katika sarafu ya malipo ya awali.

Pia, kifungu nambari 45.1(a)(2) cha SCC kilihitaji malipo ya awali (advanced payment) ya asilimia 50 ya jumla ya Mkataba kwa fedha za kitanzania kufanywa ndani ya siku 30 baada ya tarehe ya kusaini mkataba, na kwamba Mteja kwa awamu zilizo sawa kulingana na taarifa za miezi mitatu (3) ya awali atalipwa hadi yatakapokamilika.

Mapitio ya majalada ya Mradi na hati za Malipo Na. J03PV2200001863 iliyotolewa tarehe 5 Mei, 2023 yalionyesha kuwa Mshauri alilipwa shilingi 60,869,565.45 kwa huduma za ushauri, usanifu, na usimamizi wa miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kama malipo ya awali. Hata hivyo, hakukuwa na uthibitisho wa upatikanaji wa dhamana ya malipo ya awali ambayo iliyowasilishwa kabla ya kutolewa kwa malipo hayo kwa Mshauri na Wizara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kumtaka Mshauri Msimamizi kuanzisha usimamizi wa kutosha wa mkataba na kuhakikisha kuwa dhamana ya benki ya malipo ya awali inawasilishwa kabla ya kuidhinisha ankara za malipo kutoka kwa Mshauri.

## 3.6 Mahitaji ya Taarifa

Sehemu hii inatoa matokeo kuhusu mahitaji ya ripoti. Inatoa kiwango cha utimilifu wa uwasilishaji wa ripoti kulingana na Masharti ya Marejeo ya utoaji wa huduma za ushauri. Maelezo juu ya kila kipengele cha mahitaji ya kuripoti yanawasilishwa katika sehemu ndogo ifuatayo:-

### 3.6.1 Ripoti ya Uanzishwaji wa Mradi (Inception Report)

Sehemu ya 8.1 (i) ya Hadidu rejea inahitaji Mshauri kuwasilisha ripoti ya kuanzishwa kwa mradi ndani ya wiki mbili baada ya kuanza kazi, ambayo itajumuisha mbinu ya kina na mpango wa kazi kwa kazi inayofanyika na matarajio ya matokeo na malengo ya kazi.

Mapitio ya Majalada ya Mradi na mahojiano na maafisa wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo yalionyesha kuwa Mshauri hakuwasilisha Ripoti ya Mapokezi kwa Wizara kulingana na mahitaji ya Hadidu rejea.

#### (i) Uwasilishaji wa Ripoti za Maendeleo ya Ujenzi za kila mwezi

Kifungu nambari 8.1 (ii) cha Masharti ya Marejeo (ToR) kinamtaka Mshauri kuwasilisha ripoti za maendeleo ya kila mwezi ndani ya wiki ya kwanza ya kila Mwezi wa Kalenda, ambayo itajumuisha kati ya mambo ya maendeleo dhidi ya ratiba ya utekelezaji iliyokubaliwa, maendeleo ya kifedha dhidi ya bajeti na maelezo mengine yote husika.

Mapitio ya kumbukumbu za Mradi yalibainika kuwa mshauri aliwasilisha ripoti za maendeleo za mwezi wa Januari hadi Juni 2023 wakati ripoti za maendeleo ya kila mwezi kutoka Julai wakati mradi ulianza hadi Disemba, 2022 hazikupatikana kwa ukaguzi.

Hali hii ilitokana na kutokuwepo kwa ukosefu wa kumbumbu za kutosha zilizohifadhiwa na Wizara jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa taarifa hizo za ukaguzi na hatimae kushindwa kufanya tathmini ikiwa kulikuwa na uzingatiaji wa ratiba katika uwasilishaji wa ripoti za maendeleo ya kila mwezi na mshauri.

### (ii) Kutowasilishwa kwa Ripoti ya robo mwaka za Maendeleo ya Ujenzi na Ushauri Elekezi

Kifungu nambari 8.1 (iii) cha hadidu rejea kilimtaka Mshauri wakati wa zoezi kuwasilisha taarifa za maendeleo ya ujenzi wa robo mwaka kabla ya siku ya kumi ya mwezi wa kwanza katika robo inayofuata ambapo ripoti zilipaswa kubadilishwa ili kujumuisha maelezo muhimu.

Pia, Sehemu ya 8.1 (iv) ya hadidu rejea ilimtaka Mshauri wakati wa zoezi kuwasilisha ripoti za maendeleo ya ushauri wa robo mwaka zinazoelezea shughuli za wafanyakazi wa mshauri, matatizo ikiwa yapo, taarifa ya kifedha ya makubaliano ya ushauri, na taarifa nyengine muhimu kwa maendeleo ya utekelezaji wa kazi na kuwasilishwa ndani ya kipindi cha siku kumi za mwezi wa kwanza katika robo inayofuata.

Mapitio ya Majalada ya Mradi/Mawasiliano na mahojiano na maafisa wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, na msimamizi wa ukaguzi alibainisha kuwa hakukuwa na uwasilishaji wa ripoti hizo.

Kutowasilisha Ripoti ya Uanzishwaji wa Mradi, Ripoti za maendeleo ya ujenzi wa robo mwaka, na ripoti za maendeleo ya ushauri wa robo mwaka ni kutokana na ufuatiliaji duni/ usimamizi usiofaa wa mkataba na Mteja na ZBA kama Karani wa Mteja wa kazi katika kusimamia utekelezaji wa mradi kwani imebainika Wizara haina wataalamu wa kiufundi wa kusimamia utekelezaji wa mradi.

Aidha, kukosekana kwa uwasilishaji wa ripoti hizo kumesababisha kukosekana kwa taarifa za kifedha kuhusu utekelezaji wa mradi huo ambao upo katika hatari kubwa ya kumlipa mkandarasi. Pia, ukosefu wa uwasilishaji wa Ripoti ya Uanzishwaji wa Mradi hautoi uhakika kwa Mteja juu ya majukumu yake na majukumu ya mshauri katika mradi. Hii ni kwa sababu gharama zilizopatikana katika mradi hadi sasa ni kubwa kuliko kile kilichotekelezwa katika eneo la ujenzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha katika miradi ijayo, Mshauri Elekezi kuwasilisha ripoti ya awali za Mradi baada ya kusaini mkataba. Pia, kwa sasa, Mshauri anapaswa kuwasilisha ripoti zote zinazohitajika ambazo ni Ripoti za Maendeleo ya ujenzi wa robo mwaka na ripoti za maendeleo ya huduma ya ushauri wa robo mwaka kama ilivyo kwa hadidu rejea.

### (iii) Kutojumuishwa kwa kipindi cha dhima ya Kasoro (defective liability period) katika Mkataba wa huduma ya ushauri

Kwa mujibu wa kifungu nambari 12.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC), muda wa utoaji wa huduma za ushauri ulitakiwa kuwa miezi minane. Pia, kifungu nambari 13.1 cha SCC, kuanza kwa huduma ilikuwa Julai, 2022 idadi ya siku ilitakiwa kuwa siku 240 kumaliza mradi, na kumalizika kwa Mkataba kulitakiwa kuwa Machi, 2023 (Kipindi cha muda kitakuwa miezi minne kabla ya ujenzi, miezi nane kwa ujenzi na miezi kumi na mbili kwa kipindi cha dhima ya kasoro).

Mapitio ya Majalada ya Mradi na Mkataba wa Huduma za Ushauri Nambari. SMZ/J03/W/RCB/2021-22/20 uliofungwa kati ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, na Kampuni ya Ushauri ya M/S Diamond Builders Limited, ukaguzi ulibaini kuwa mkataba huo ulihusisha miezi nane (8) tu ya ujenzi kuanzia Julai, 2022 hadi kumalizika kwa Mkataba Machi, 2023. Hata hivyo, kipindi cha dhima ya kasoro haijabainishwa katika mkataba.

Vile vile, mapitio ya hadidu rejea za Mkutano wa Majadiliano ya tarehe 29 Aprili, 2022 yalionyesha kuwa mshauri alikubali kufanya kazi ya ukarabati na uboreshaji wa Uwanja wa Gombani Pemba kwa kipindi ambacho mkataba utahitaji kukamilisha kazi, ikiwa ni pamoja na muda ambao mkataba utaomba kuongezwa baada ya kumalizika kwa muda uliokubaliwa, mara baada ya kusaini mkataba. Hata hivyo, Mkutano wa majadiliano haukujadili kipindi cha dhima ya kasoro.

Kushindwa kujumuisha kipindi cha dhima ya kasoro katika Mkataba wa Huduma ya Ushauri husababisha hatari ya ukosefu wa uwajibikaji kwa mshauri.

### (iv) Kutokuandaliwa kwa Ripoti za Fedha na kujitokeza kwa mapungufu katika maandalizi ya ripoti za maendeleo ya mradi kwa Mshauri elekezi kwenda kwa mteja kulipelekea kufanyika malipo ya ziada kwa kazi ambazo hazikufanyika

Kifungu cha 6.2(e) cha **Kiambatisho A,** Hadidu Rejea (ToR) cha Mkataba wa utoaji wa huduma za ushauri kwa ajili ya kubuni na kusimamia matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba, kilimtaka Mshauri kuandaa ripoti za maendeleo ya mradi na ripoti za mara kwa mara za fedha zinazohusiana na ripoti za maendeleo ya mradi.

Mapitio ya kumbukumbu za mradi yalibaini kuwa hakukuwa na Ripoti za Maendeleo ya kila mwezi kwa mwezi wa Julai hadi Disemba 2022, hata hivyo, Ukaguzi ulipatiwa Ripoti za Maendeleo ya Kila Mwezi kwa Januari hadi Juni, 2023 tu. Baada ya uhakiki wa ripoti hiyo, ukaguzi ulibaini kuwa katika taarifa zote wameonyesha tu kuwa malipo ya awali ndiyo malipo pekee ambayo mkandarasi amepokea hadi Aprili 2023 wakati ukweli ni hadi Aprili mkandarasi alikuwa tayari amelipwa malipo ya pili baada ya malipo ya awali na pia ripoti ya Aprili inasema kuwa "mkandarasi anakabiliwa na changamoto ya malipo ambayo husababisha baadhi ya kazi kuchelewa" lakini ukweli ni hadi Aprili, 2023 mkandarasi alilipwa karibu nusu ya jumla ya malipo ya mkataba ambayo ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kazi zilizotekelezwa kulingana na mkataba.

Ukaguzi umebaini kuwa hadi tarehe 27 Julai, 2023 wakati wa ukaguzi huu mkandarasi alikuwa amelipwa jumla ya shilingi 2,322,523,580.79. Maelezo yanawasilishwa katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 12: Malipo yaliyofanywa kwa Mkandarasi hadi sasa**

| Nam | Aina ya Cheti | Malipo Halisi yaliyolipwa kwa Mkandarasi (Shilingi) | Kodi kwa ZRA (Shilingi) | Kodi Kwa TRA (Shilingi) | Jumla ya Malipo ya Cheti kwa Mkandarasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyeti vya malipo ya awali | 507,895,652.17 | 36,521,739.13 | 15,582,608.70 | 560,000,000.00 |
| 2 | Cheti cha 1 | 988,135,911.00 | 71,054,835.00 | 40,269,393.79 | 1,099,460,139.79 |
| 3 | Barua ya Mkopo iliyolipwa kwa mkandarasi | | | | 663,063,441.00 |
| **Jumla ya Malipo Yaliyofanywa kwa Mkandarasi hadi sasa** | | | | | **2,322,523,580.79** |

*Chanzo: Uchambuzi wa vyeti vya Malipo na hati za malipo uliofanywa na Wakaguzi, 2023.*

Kutokana na jadweli hapo juu, hadi sasa, mkandarasi amelipwa jumla ya shilingi 2,322,523,580.79 pamoja na VAT sawa na asilimia 82.95 ya jumla ya Mkataba wa shilingi 2,800,000,000 ikiwa ni pamoja na kazi za ukarabati na kufanya tofauti ya shilingi 477,476,419.21 kati ya kiasi kilicholipwa na kiasi cha mkataba.

Aidha, timu ya ukaguzi pamoja na Mwakilishi wa Mkandarasi na Mshauri walifanya ziara ya pamoja katika eneo la ujenzi na kuchukua vipimo na uhakiki wa kazi zote zilizofanywa hadi sasa na kazi zote ambazo zinatekelezwa kwa mujibu wa mkataba wa hati za makisio ya gharama za ujenzi.

Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 20 Julai, 2023 hadi tarehe 23 Julai, 2023, na baada ya kutembelea eneo la ujenzi tathmini ya wakaguzi ilifanyika juu ya kazi zilizofanywa hadi wakati wa ziara na kupatikana matokeo kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapa chini: -

**Jadweli Nambari 13: Muhtasari wa Tathmini ya Thamani ya Kazi zilizofanywa hadi sasa dhidi ya Kazi za Mkataba kulingana na Mkataba wa hati za makisio ya gharama za ujenzi**

| Nambari ya kipengele | Bili katika Mkataba wa BoQ | Kiasi kwa mujibu wa BoQ (Tsh) (A) | Kiasi cha fedha kwa mujibu wa kazi iliyotokelezwa (B) (Tsh) | Thamani ya kazi ambazo hazijatekelezwa hadi wakati wa ukaguzi = (A-B) (Tsh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bili Namba 1: MAELEZO | 225,000,000 | 123,804,884.85 | 101,195,115 |
| 2 | Bili Namba 2: UJENZI MKUU | 2,198,495,900 | 276,152,700 | 1,922,343,200 |
| | **JUMLA (bila ya VAT)** | **2,423,495,900** | **399,957,585** | **2,023,538,315** |

*Chanzo: Uchambuzi wa kazi zilizotekelezwa kwa mujibu wa BoQ za Mkataba, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa jumla ya shilingi 2,423,495,900 (bila ya VAT) ilikuwa ni thamani ya kazi za mkataba kwa mkandarasi kwa mujibu wa mkataba hati za makisio ya gharama za ujenzi na baada ya kutembelea eneo la mradi na vipimo vya kazi zote zilizo chini ya mkataba ni kazi tu zenye thamani ya shilingi 399,957,585 (pamoja na VAT) zilitekelezwa hadi kufikia hatua ya malipo stahiki na thamani ya jumla ya kazi zinazofikia shilingi 2,023,538,315 (pamoja na VAT), kazi nyengine zilikuwa zinaendelea na nyengine hazikutekelezwa kabisa wakati wa ziara ya eneo la mradi na vipimo ambavyo vilianza kutoka tarehe 20 Julai, 2023 hadi tarehe 23 Julai, 2023. Hali hii inamaanisha kuwa hadi sasa kazi zilizotekelezwa kuhusiana na malipo yaliyofanywa kwa mkandarasi yamelipwa kwa hivyo inamaanisha tayari analipwa hata kwa kazi ambazo kwenye eneo la mradi bado hazijatekelezwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kufanya yafuatayo: -

a) Kuelekeza Mshauri wa Usimamizi kuimarisha utaratibu wake wa kudhibiti ili kuhakikisha kuwa kuna utekelezaji wa kutosha wa majukumu yake katika usimamizi wa mkataba. Hii ni pamoja na kufanya kazi zake kwa bidii, kwa weledi na kwa ufanisi kwa utekelezaji mzuri wa mradi.

b) Kuepuka kuidhinisha malipo kwa shughuli ambazo hazijatekelezwa na malipo yanapaswa kufanywa tu kwa kazi zilizotekelezwa.

c) Kuhakikisha kuwa, kwa shughuli zinazolipwa bila kutekelezwa malipo yake yahifadhiwe na kuhamishiwa kugharamia shughuli nyingine ambazo bado hazijatekelezwa ili muda wa utekelezaji wa shughuli hizo uwe tayari, mfuko uliotengwa utumike kwa malipo ili kudhibiti fedha za mradi ili kuhakikisha thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za mradi.

d) Kuhakikisha kuwa katika miradi ya baadaye inahusisha Makampuni ya Ushauri ambayo yana uzoefu unaohitajika kulingana na Masharti ya Marejeleo yaliyoandaliwa (ToR) ili kuhakikisha usawa na uwazi katika mchakato wa ununuzi.

## 3.7 Matokeo ya ukaguzi kuhusiana na Usimamizi wa Fedha za Mradi na Udhibiti wa Ndani (Udhibiti wa gharama)

Sehemu hii inatoa matokeo kuhusu usimamizi wa kifedha wa mradi na udhibiti wa ndani pamoja na udhibiti wa gharama. Maelezo yanawasilishwa katika sehemu zifuatazo.

### 3.7.1 Matayarisho yasiojitosheleza ya makisio ya gharama za ujenzi (BoQ)

Ukaguzi uliofanyika ulibaini udhaifu katika maandalizi ya hati za makisio ya gharama za ujenzi kwa ajili ya matengenezo na maboresho ya miundombinu ya uwanja wa michezo wa Gombani Pemba. Hali halisi ni kama inavyoelezewa hapo chini: -

**(a) Wizara ilitumia aina tatu tofauti za makadirio ya gharama za ujenzi kwa Mradi**

Kanuni ya 125(1) ya Kanuni za Manunuzi wa Umma, 2020 ilitaka kuwa, "Kutakuwa na makadirio ya thamani ambayo ni msingi wa ununuzi na utoaji wa bidhaa, kazi au huduma" ambayo ni zaidi kufanyika kabla ya kuanza mradi wowote wa ujenzi.

Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara iliandaa matoleo mawili ya makadirio ya gharama za ujenzi kwa mradi huu ambayo ni tofauti katika baadhi ya vitu na thamani ya jumla na BoQ moja kwa kazi za ziada kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo Gombani Pemba, na kufanya jumla ya BoQ tatu kama ilivyoelezwa katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 14: Gharama za Ujenzi Makadirio BoQ kwa Mradi**

| Namba | Maelezo | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | BoQ ambayo ilitumika katika hati ya zabuni kwa ununuzi wa awamu ya 1 | 2,477,881,410 |
| 2 | BoQ ambayo ilitumika katika hati ya zabuni kwa awamu ya 2 ya manunuzi (Hati ya Mkataba BoQ) | 3,132,745,475 |
| 3 | BoQ ya 1 kwa kazi za ziada | 420,191,600 |

*Chanzo: BoQ iliyopitiwa upya kwa ukarabati wa Uwanja wa Gombani*

Kutokana na jadweli hapo juu, BoQ ya kwanza yenye thamani ya shilingi 2,477,881,410 ilitumika katika hati ya zabuni ya awamu ya kwanza ya manunuzi, na BoQ ambazo zilitumika katika hati ya zabuni ya awamu ya pili ya manunuzi (Contract Document BoQ) yenye thamani ya shilingi 3,132,745,475 na BoQ kwa kazi za ziada zenye thamani ya shilingi 420,191,600. BoQ zote tatu zilikuwa na mapungufu kama ilivyoelezwa hapa chini:-

### (b) Maandalizi ya hati za makisio ya gharama za ujenzi bila kuonyesha Majina ya Mwajiri, Msanifu, na Mtafiti wa mradi (quantity surveyor)

Sehemu B ya Taarifa za Awali, Kifungu B1 cha Njia ya Kawaida ya Upimaji (SMM) ya Ujenzi wa Toleo la Kwanza la Afrika Mashariki la 1970, inahitaji makisio ya gharama za ujenzi (BoQ) kuonyesha majina na anuwani za mwajiri, msanifu, na mchunguzi wa kiasi ambacho walihusika katika kubuni na kuandaa (BoQ) ambacho pia kinahusika katika utekelezaji wa mradi huo. Maelezo haya yanapaswa kuonyeshwa katika bili namba moja ya BoQ ambayo ni taarifa za awali.

Mapitio ya bili namba moja ya taarifa za awali katika mkataba wa BoQ namba SMZ/SO1/W/RCB/2021-22/20, ukaguzi haukuweza kuona majina na anuwani za mwajiri, msanifu, mpimaji na kampuni zao ambazo zilihusika katika kubuni na kuandaa makisio ya gharama za ujenzi ambao pia wanahusika katika utekelezaji wa mradi.

Kushindwa kuonesha maelezo haya kunaondoa wajibu na jukumu la watumishi hawa katika kipindi cha utekelezaji wa mradi kwani kutokana na BoQ zilivyoandaliwa ni vigumu kujua Jina la Mwajiri, jina la kampuni ya Usanifu inayohusika katika kubuni na pia ni vigumu kujua kampuni ya 'Quantity Surveyor' inayohusika katika maandalizi ya BoQ.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo wataalamu wenye uwezo wahusishwe katika maandalizi ya hati za makisio ya gharama za ujenzi (BoQ).

### (c) Utoaji usioridhisha wa Vipimo katika hati za makisio ya gharama za ujenzi (BoQ)

Ukaguzi ulibaini kwamba gharama za makisio ya ujenzi ambazo zilitumika katika hati ya zabuni ya awamu ya kwanza ya ununuzi na gharama za makisio ya ujenzi katika Mkataba kwa ajili ya matengenezo yaliyopendekezwa ya ukarabati wa uwanja wa Gombani Pemba hazikuandaliwa kwa usahihi. Hali hii ni kutokana na ukweli kwamba hati ya zabuni iliona gharama za makisio ya ujenzi ni kuwa sawa na mchanganuo wa bei, pia kitengo cha kipimo kilichotumika kwa vitu vifuatavyo havikulingana na mahitaji ya BoQ kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 15: Utoaji usiotosheleza wa Vipimo katika BoQ iliyotumika katika Hati ya Zabuni kwa Awamu ya Kwanza ya Ununuzi na katika BoQ na Njia ya Kawaida ya Vipimo (SMM)

| Namba | Maelezo | Kipimo cha Upimaji kulingana na Hati ya Zabuni Awamu ya 1 (BoQ) | Kipimo kinachohitajika kulingana na njia ya kipimo cha kawaida (SMM) |
|---|---|---|---|
| **BOQ KUTUMIKA KATIKA HATI YA ZABUNI KWA AWAMU YA KWANZA YA UNUNUZI** | | | |
| 1. | Udongo wa Eneo la kazi (Site Earthing)- Minara (Towers)<br><br>Ununuzi na ufungaji wa mfumo wa ardhini karibu na Minara ikiwa ni pamoja na kuweka baa za TGB kutoka katika zege, kuweka baa za TGB kwenye ngazi, kuunganisha vifaa muhimu na kitu kingine kwa mfumo wa kutuliza na "cablelugs", Kuambatisha kondakta kwa kutumia vipande vya chuma kwa mguu wa mnara, unganisha ringi ya EGL (EGL Ring). kuweka denzo (apply denzo) kubandika kwenye lagi zote za kebo. Kiwango kinajumuisha zana zote. (Cable lug crimper, kuweka denzo, nk) | Loti | Nr |
| 2. | Muundo wa Mnara na uchambuzi wa uwekaji | Mnara | Nr |
| 3. | Kupungua kwa taa zilizopo (ikiwa ni pamoja na waya za umeme) juu ya mnara kabla ya kupunguza urefu wa mnara | Loti | Nr |
| 4. | Marekebisho ya Mnara (juu) ili kukidhi muundo mpya wa mwanga | Mnara | Kipengele |
| 5. | Ukarabati wa mnara (ikiwa ni pamoja na Kuimarisha, kubadilisha Bolts & nati , na upakaji wa rangi) | Mnara | Kipengele |

| Namba | Maelezo | Kipimo cha Upimaji kulingana na Hati ya Zabuni Awamu ya 1 (BoQ) | Kipimo kinachohitajika kulingana na njia ya kipimo cha kawaida (SMM) |
|---|---|---|---|
| 6. | Ununuzi, Ufungaji, na Uagizaji wa 16Pcs of Earth rods na 100m ya 70mm$^{2,}$ CU / bare ya waya za chini ya ardhi kwa Jenereta, Paneli kwenye nguzo, kizuizi cha taa (lighting arrestor), nguzo yenyewe & chumba cha kudhibiti Earthling (shaba halisi,16mm) ikiwa ni pamoja na vifaa vya earthling. | Loti | Nr |
| 7. | Usambazaji na kuweka tofali nchi 5 kwenye sehemu zilizo wazi | PC | $M^2$ |
| **BoQ ya MKATABA** | | | |
| 8. | Ununuzi na uwekaji wa matofali ya inchi 5 5N / $MM^2$ kwa ajili ya maeneo yaliyowazi yaliyozunguka uwanja. | Nr | $M^2$ |

*Chanzo: Uchambuzi wa BoQ uliofanywa na Wakaguzi, 2023*

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo kunakuwa wataalamu wenye uwezo watakaohusika katika maandalizi ya BoQ.

### (d) Kutojitosheleza kwa makisio ya gharama za ujenzi

Kifungu A cha Maelezo, Kifungu A3 (b) cha utaratibu wa Kawaida wa Upimaji (SMM) wa Ujenzi wa Toleo la Kwanza la Afrika Mashariki la 1970, ambayo inasema kuwa vitu vyote katika BoQ vitajumuisha; Kazi na gharama zote kuhusiana na vifaa, bidhaa na gharama zote kwa mfano Usafirishaji, uwasilishaji, kutoa mzigo, kuhifadhi, kufunga mzigo, utunzaji, kupandisha, kupunguza), kurekebisha vifaa na bidhaa katika nafasi, Matumizi ya mtambo, Takataka, Viwanja vya nje, gharama za kazi za awali, malipo ya uendeshaji na faida itakayopatikana.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya BoQ ambazo ziliingizwa katika hati ya zabuni ya Awamu ya Kwanza kuwa BoQ ilikuwa na awamu mbili, awamu moja ilikuwa na vitu ambavyo vilikuwa na maelezo ya kazi ambazo mkandarasi alitakiwa kujaza kiwango ambacho kilikuwa na bei ya vifaa na gharama zote zinazohusiana lakini awamu nyengine ni awamu ya nyenzo ambazo zilihitaji bei tu lakini zilionyeshwa katika BoQ ambapo zote zilikuwa na gharama zinazohitajika kuhifadhiwa kwa kiwango ambacho kinajumuisha bei za vifaa na gharama zao zote zinazohusiana kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 16: Vitu vilivyotolewa katika BoQ vilivyotumika katika hati ya zabuni kwa Awamu ya Kwanza ya Ununuzi wa Vifaa**

| Namba | Maelezo | Kiasi Kulingana na Hati ya Zabuni Awamu ya 1 (BoQ) |
|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa mifuko ya Saruji | Mfuko |
| 2. | Usambazaji wa Projekta ya TV | Seti |
| 3. | Usambazaji wa Samani za Ukumbi | Seti |

*Chanzo: Uchambuzi wa BoQ ambayo ilitumika katika hati ya zabuni kwa ununuzi wa awamu ya 1, 2023*

Jadweli hapo juu ya vifaa vilivyooneshwa zilijumuishwa kwenye BoQ wakati vifaa hivyo vipo katika mfumo wa orodha ya vifaa na sio maelezo ya kazi ya kufanywa. Kuingizwa kwa orodha ya nyenzo kwa BoQ ya kazi kunaweza kusababisha malipo mara mbili kwani kitu kimoja kitalipwa kama kazi iliyofanywa kwa upande mmoja na kwa upande mwingine italipwa kama nyenzo, matokeo yake yatasababisha upotezaji wa fedha za Serikali.

Kuingizwa kwa orodha ya vifaa kwenye BoQ ya kazi inaweza kusababisha kufanyika malipo mara mbili kama kitu kimoja kitalipwa kama kazi iliyofanywa kwa upande mmoja na kwa upande mwingine italipwa kama nyenzo ambapo matokeo yake itasababisha kujitokeza kufanya malipo mara mbili kwa gharama ambazo hazikuoneshwa kwenye BoQ.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo wataalamu wenye uwezo wanahusika katika maandalizi ya BoQ ili kuhakikisha upangaji na ukadiriaji wa makisio unafanywa kwa mazingatio ya thamani halisi ya fedha kwa mujibu wa vifaa na kazi inayohitajika kufanyika.

### (e) Maandalizi ya BoQ bila ya kuzingatia bei za bidhaa

Mapitio ya BoQ ambayo yaliingizwa katika hati ya zabuni kwa awamu ya 1 ya ununuzi yalibainisha kuwa BoQ iliyoandaliwa haikuzingatia bei ya bidhaa katika mapendekezo ya ukarabati wa Uwanja wa Michezo wa Gombani Pemba, ambapo taarifa zilizokosekana ilikuwa kama ifuatavyo: -

Katika Bili nambari moja imekosekana taarifa ya gharama za awali, Bili nambari mbili ilikosa gharama za ujenzi pamoja na ujumla ikiwemo ubomoaji na ubadilishaji wa muundombinu, kwenye Bili nambari tatu ilikosa gharama za ujenzi wa Ukuta, Bili nambari nne ilikosa gharama za ujenzi wa Paa, Bili nambari tano ilikosa gharama za Madirisha, Bili Nambari sita ilikosa gharama za Milango, Bili nambari saba ilikosa gharama za Uchoraji na Mapambo, Bill nambari nane ilikosa gharma za uwekaji wa vifaa mbali mbali, Bili nambari tisa ilikosa gharama za uwekaji wa miundombinu ya maji, vifaa vya kuzimia moto na Bili nambari kumi imekosa gharama za jumla kuu.

Ukaguzi ulipitia taarifa za mikataba pamoja na BoQ na kubaini kuwa BoQ iliyotayarishwa ilikosa taarifa muhimu ikiwemo gharama ya ubomoaji na marekebisho, pamoja na gharama za Mabomba ya maji, gharama za vifaa vya Kupambana na moto,pamoja na gharama za jumla kuu.

Utayarishaji wa BoQ ambazo hazikujumuisha gharama ya kazi zitakazofanywa kunaweza kupelekea uwepo wa tofauti za gharama zitakazojitokeza pamoja na kusababisha viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo inaajiri wataalamu wenye uwezo wa kutayarisha BoQ zenye kujitosheleza kwa vigezo na mahitaji ya kazi husika.

### (f) Kukosekana kwa maelezo ya kina kuhusiana na vigezo vya vifaa kwenye BoQ

Mapitio ya BoQ ambayo yaliingizwa katika hati ya zabuni kwa awamu ya 1 ya ununuzi ukaguzi umebaini BoQ iliyomo ndani ya mkataba ilikosa baadhi ya taarifa muhimu za vigezo vilivyotolewa kwa awamu ya kwanza kwenye hati ya zabuni na BoQ ya mkataba ambapo ilibainika vigezo vyake havikutosheleza kwa sababu vilikuwa na makadirio hafifu ya vifaa na kupelekea kuwa na utekelezaji mgumu kwa mkandarasi na hata kwa Wizara kuweza kuelewa aina ya kazi ambazo zinahitaji kutekelezwa na aina ya vifaa ambavyo vinahitaji kutumika.

Kutokana na hali hiyo kulipelekea kujitokeza kwa ugumu kutathmini kazi iliyotekelezwa na iliyokuwa haikutekelezwa na mkandarasi. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 4**.

Kutokana na hali iliyobainishwa hapo juu ya kutoainisha kwa baadhi ya bidhaa/ vifaa katika hati ya zabuni kunaweza kupelekea kujitokeza kwa tofauti ambazo zinaweza kusababisha ongezeko la gharama zisizo za lazima na hatimae kuathiri utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo wataalamu wenye uwezo wanahusika katika maandalizi ya makisio ya gharama za vifaa ili kuepusha kujitokeza kwa baadhi ya vifaa kujirudia katika BoQ.

### (g) Kutokuzingatia vitu muhimu vya Kazi katika BoQ kulikosababisha Gharama za ziada kwa Mkataba zinazofikia shilingi 420,191,600

Katika mapitio ya mkataba wa makisio ya gharama za vifaa vya ujenzi kwa kazi za ziada, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na vitu muhimu vilivyokosekana kama vile; vifaa vya kazi za ubomoaji na mabadiliko, vifaa vya mabomba na kazi za kuzima moto, na vifaa vya mitambo ya umeme. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 17: Muhtasari wa Vifaa vya kazi za ziada kwa Kazi isizozidi 15% ya Jumla ya Mkataba kulingana na BoQ**

| Bidhaa katika BoQ | Maelezo ya Kazi | Gharama katika BoQ kwa kazi za ziada zisizozidi 15% |
|---|---|---|
| Kipengele 1.0 -1.28 | Kazi ya kufunga mabomba ya maji | 102,228,100.00 |
| Kipengele 2.0 | Kazi ya ubomoaji | 210,191,500.00 |
| Kipengele 3.0 | Ufungaji wa umeme kwa jengo kuu | 42,987,200.00 |
| Kipengele 4.0 | Kazi ya Umaliziaji (Finishing) | 37,784,800.00 |
| Kipengele 5.0 | Marekebisho ya Guta (Gutter Rectifications) | 27,000,000.00 |
| **Jumla** | | **420,191,600.00** |

*Chanzo: Kazi za ziada hazizidi asilimia 15 (BoQ)*

Jadweli hapo juu linaonyesha gharama za ziada za kiasi cha shilingi 420,191,600 zilizojumuishwa katika mkataba kutokana na maandalizi duni ya mkataba wa kwanza BoQ. Hii ilisababisha ongezeko la gharama za mkataba zisizo za lazima na pia imesababisha ucheleweshaji wa kukamilika kwa kazi za ukarabati kwani baadhi ya kazi hizi za ziada zinahitajika kuja kwanza kabla ya kushiriki katika kazi zilizopewa mkandarasi chini ya Mkataba wa BoQ. Hii ilisababishwa na uratibu usioridhisha kati ya Mshauri aliyehusika katika maandalizi ya BoQ iliyojumuishwa na Mkataba na wafanyakazi wa kiufundi wa Wizara ambao walikagua BoQ iliyoandaliwa na Mshauri.

**(h) Kuidhinisha zaidi ya mara moja kwa kazi zenye kufanana ambazo zilibainika katika hatua za Ufafanuzi wa zabuni katika BoQ iliyoambatanishwa na Mkataba na kuidhinisha upya katika kazi za ziada**

Kifungu kidogo cha 9.1 na 9.2 cha Maagizo kwa Wazabuni (ITB) kinaeleza kwamba kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni, Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa sababu yoyote, inaweza kurekebisha hati za zabuni kwa kutoa nyongeza na nyongeza yoyote iliyotolewa itakuwa sehemu ya hati za zabuni na itawasilishwa kwa maandishi au baruapepe kwa wote ambao wamenunua nyaraka za zabuni moja kwa moja kutoka kwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi kupitia mapitio ya barua yenye kumbukumbu namba WHWM/BZ/11/1/VOL.1/205 ya tarehe 6 Mei, 2022 umebaini kuwa Wizara baada ya kikao cha awali kilichofanyika tarehe 22 Aprili, 2022 katika Ofisi za Makao Makuu ya Wizara Unguja na ziara ya kikazi iliyofanyika tarehe 23 Aprili, 2022 katika eneo hilo, Wizara ilichukua hatua ya kuandika barua rasmi kwa cha hatua za ufafanuzi kwa wakandarasi wote ambao walipewa nyaraka za ununuzi wa Ukarabati wa miundombinu ya uwanja wa michezo Pemba ili kufafanua masuala na kujibu maswali juu ya jambo lolote ambalo liliibuliwa wakati wa mkutano na wakati wa ziara ya eneo la ujenzi, kwamba hii inamaanisha mambo yote yaliyojadiliwa na kutolewa ufafanuzi yaliwasilishwa kwa wakandarasi wote na yalijumuishwa katika hati ya zabuni na kuwa sehemu ya mkataba.

Zaidi ya hayo, mapitio ya barua yenye kumbukumbu namba CCD: 182/236/01 kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwenda kwa Meneja wa Mradi ya tarehe 16 Juni, 2023 iliidhinisha kazi za ziada zisizozidi asilimia 15 ya jumla ya mkataba (shilingi 2,800,000,000) yenye thamani ya shilingi 420,191,600.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya kazi ambazo zilishajumuishwa katika kazi ya awali zilibainika kuinigizwa kwa mara nyengine katika kazi ya ziada iliyoidhinishwa ambayo ilitakiwa isizidi asilimia 15 ya bei ya mkataba wa awali.

Kutokana na kujitokeza kwa dosari hiyo imebainika uwepo wa viashiria vya kufanyika kwa malipo mara mbili kwa baadhi ya kazi ambazo zilishajumuishwa katika kazi ya awali na hatimae huwenda ikapelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma pindipo mkandarasi atakapolipwa malipo ya ziada. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 18: Muhtasari wa Kazi ambazo zilitozwa malipo mara mbili katika Mkataba mmoja**

| Description | Clarification Point | Contract BoQ | BoQ for additional works not exceeding 15% |
|---|---|---|---|
| Transformer Shed | **Item 7**- Remove the existing non load bearing wall single panel (column to column), supply and install entrance gate full sized area to allow transformer to move through it | Item 3/C-Substation Installation and Commissioning including Shedding (1lot) | Item 1/J-Demolition of the dry wall partition and replace with the new (M/S) |
| Conference hall tiles | **Item 10**-Supply and Install porcelain polished floor tiles for conference hall size 600x600x12mm thick to floor including remove existing tiles and prepare the surface to receive new tiles | - | Careful demolish the all the floor tiles and replace it with new tiles (M/S) and remove all the debris |
| Broadcast Control Room | **Item 13**- Renovate Broadcast Control Room by supply and install the following; Prepare the surface to receive new floor tiles 600x600mm | - | Careful demolish the all the floor tiles and replace it with new tiles (M/S) and remove all the debris |
| Players Dressing and toilet rooms renovation | **Item 11**- Remove existing door and apply 150mm thick brick wall to fill the opening sized 1x2.5metres | Supply and Install 5 inch Bricks 5N/MM2 for all gapes around the Stadium | |

*Chanzo: Vidokezo vya Ufafanuzi wa Bidding kwa Wakandarasi, BoQ za Mkataba, na idhini ya kazi za ziada zisizozidi 15% ya jumla ya mkataba*

*"The table above indicates that, the above Transformer Shed was allocated and approved thrice in all documents. For Conference Hall tiles, the work for removing existing tiles and preparing the surface to receive new tiles has been allocated twice; it is allocated in clarification points and also allocated in BoQ for additional works not exceeding 15%. The work for Broadcast Control Room; it is also allocated in two documents which are Clarification Points document and in Additional Works not exceeding 15%. While for Players Dressing and toilet rooms renovation, the item for filling the opening has been provided thrice in Clarification Points and in Contract BoQ."*

Kutokana na taarifa iliyobainishwa hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara: -

(i) Kufanya mapitio ya idhini iliyotolewa kwa kazi za ziada zisizozidi asilimia 15 ya jumla ya bei ya mkataba na kufanya mabadiliko ya kazi zilizojitokeza zaidi ya mara moja ili kuepusha kuja kufanyika kwa malipo ya ziada.

(ii) Kuhakikisha kwamba kwa fedha itakayopatikana ambayo haitolipwa kwa kazi zilizojirejea kama nilivyozibainisha hapo juu ni vyema fedha hiyo ikatumika kwa kazi za ziada zilizopangwa ambazo hazitafikia asilimia 15 ya mkataba wa awali.

(iii) Kuhakikisha kwamba inaomba muongozo wa utekelezaji wa kazi za ziada kwa Mamlaka ya Manunuzi hii ni kutokana na kwamba makubaliano yaliyoidhinishwa ya asilimia 15 yamejumuisha shughuli zilizojirejea ambazo zilifafanuliwa katika mkutano wa awali wa utekelezaji wa mradi kabla ya kupata idhini ya asilimia 15 ya mkataba wa jumla wa kazi za ziada jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma.

(iv) Kuhakikisha kuwa katika miradi ijayo, inatoa kipaombele katika utoaji wa kazi kwa makampuni yenye sifa, ujuzi na uwezo wa kuishauri vyema Wizara juu ya usimamizi wa miradi ya Serikali.

### 3.7.2 Kujitokeza kwa dosari katika kazi za ziada zilizoidhinishwa

Kwa mujibu wa utaratibu kila BoQ ya mkataba inatakiwa iandaliwe ikiwa na idadi ya vifaa vinavyolingana na thamani ya fedha ambayo itajumuishwa katika gharama ya mkataba.

Katika mapitio ya BoQ zilizoandaliwa kwa kazi ya ziada imebainika kujitokeza kwa dosari ya uwepo wa tofauti ya gharama inayotokana na kiasi duni cha fedha kilichowekwa ambacho hakiendani na uhalisia na bei ya vifaa inayopaswa kununuliwa ima kwa kuzidishwa kiasi cha bei au kupunguzwa idadi ya vifaa na hatimae kutokea kwa athari ya gharama halisi ya mkataba. Hali halisi ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jadweli hapa chini.

## Jadweli Nambari 19: Uchambuzi wa BoQ kwa kazi za ziada zilizowasilishwa na Mshauri

| Kipengele | Maelezo | Kiasi | Kipimo | Kiwango (Shilingi) | Kiasi katika BoQ (Shilingi) (B) | Kiasi kilichobainika kwa mujibu wa Ukaguzi (Shilingi) (A) | Tofauti (Shilingi) C=A-B |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Umaliziaji wa tarazo (Sakafu) | 400 | $m^2$ | 580,000 | 23,200,000 | 232,000,000 | 208,800,000 |

*Chanzo: Uchambuzi wa kazi za ziada zilizoidhinishwa tarehe 16 Juni, 2023*

Kutokana na jadweli hapo juu, ukaguzi ulibaini kujitokeza kwa dosari iliyoripotiwa ya kiasi cha shilingi 580,000 kwa uwekaji wa tarazo kwa kila $m^2$ moja iliyonukuliwa na mkandarasi badala ya shilingi 58,000 iliyokusudiwa na Wizara na kupelekea uwepo wa tofauti wa shilingi 208,800,000 ambayo itasababisha kuongezeka kwa gharama za mkataba.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuwa makini katika kupitia taarifa za ukokotoaji wa hesabu zinazoandaliwa katika BoQ ili ziweze kuendana na uhalisia wa kila hitajio lililobainishwa katika BoQ kwa lengo la kunusuru kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma.

### 3.7.3 Kujumuishwa kazi zinazopaswa kufanywa na mshauri elekezi katika kazi za ziada za wakandarasi

Mapitio ya kazi za ziada zilizoidhinishwa katika BoQ kwa mkandarasi kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba CCD: 182/236/01 ya tarehe 16 Juni, 2023 kutoka Wizara kwenda kwa Meneja wa Mradi ilibainisha kuwa moja ya kazi ambayo iliidhinishwa chini ya Kipengele G cha kazi ya Kubomoa ilikuwa kazi ambayo imejumuishwa katika mkataba wa Mshauri lakini pia iliidhinishwa kama kazi ya ziada kwa mkandarasi.

Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 20: Uchambuzi wa BoQ kwa Kazi za Ziada zilizowasilishwa na Mshauri**

| Kipengele | Maelezo | Kiasi | Kitengo | Kiwango (TZS) | Kiasi katika BoQ ya ziada (B), TZS |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UBOMOAJI<br>- Uchunguzi wa paa zima na sehemu za sakafu zinazovuja kwenye jengo. | | Kipengele | 7,250,000 | 7,250,000 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa kazi za ziada zilizoidhinishwa tarehe 16 Juni, 2023*

Kutokana na jadweli liliopo hapo juu linabainisha ya kwamba pindipo kukikosekana kwa utaalamu wa kuchambua na kubagua majukumu ya kazi za mshauri elekezi na kazi za mkandarasi huwenda ikapelekea Serikali kulipa malipo ya kazi ya aina moja kwa mkandarasi na mshauri elekezi na hatimae kupoteza fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kupitia upya utaratibu wa kazi za ziada zilizotolewa ili kunusuru kujitokeza kufanyika malipo ya ziada ambayo yatasababisha upotevu wa fedha za umma.

### 3.7.4 Kutojumuishwa kwa baadhi ya kazi muhimu katika BoQ ya mkataba wa kazi za ukarabati

Mapitio ya BoQ za Mkataba na BoQ kwa kazi za ziada zisizozidi asilimia 15 ya jumla ya mkataba na kupitia ziara za eneo la utekelezaji wa mradi iliofanywa tarehe 20 Julai, 2023 hadi 23 Julai, 2023, ukaguzi ulibaini kujitokeza kwa dosari za kutojumuishwa kwa baadhi ya kazi muhimu katika BoQ ya mkataba kama ilivyobainishwa katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 21: Vitu muhimu ambavyo havijajumuishwa katika BoQ za Mkataba na katika BoQ kwa kazi ya ziada

| Item | Description of Work |
|---|---|
| 1 | Plumbing works not included<br>• In Additional works BoQ there is no item for urinals and western type toilet in item for sanitary appliance but at site first fix for the forehead mentioned has been installed;<br>• There is no item for Bib corks for all toilets;<br>• In additional BoQ there are only two shower for player's rooms but for other bath room such as for Referees and Match Commissioner there is no shower provided for them;<br>• At site first fix of draining water has been done but the appliance / item which will be used the floor drain is not provided in all BoQ; and<br>• In all bath room there is no provision of item in all BoQ to cover all requirements in the bathroom such as Towel holder, soap dish holder |
| 2 | Septic and Soak away Pits |
| 3 | Renovation of spectaculars toilets<br>• Repair of all defects in floors, doors, wall in all the toilets including repainting<br>• Plumbing works and electrical works in all the Spectaculars toilets<br>• In Spectaculars toilets not all Hand wash sinks and urinal sinks need to be removed some need to be washed and changes to be made only to the in-late water tape and outlet pipe but some need to be replaced with the new ones it is the work of consultant team in corroborations with the client to conduct condition survey |
| 4 | Repair of spectaculars sitting stairs |
| 5 | Hacking and repainting of the whole stadium structure with the inclusion of painting to spectaculars sitting stairs |
| 6 | Repair of gates to the Entrance of spectaculars toilets |
| 7 | Repair of all stadium structural members such as beams and columns and walls including hacking, plastering and painting to cover all open reinforcements bars to the inner side and outside of stadium |
| 8 | Repair of concrete slab and concrete gutter including hacking, plastering and installment of new water proof materials to the slab and gutters |
| 9 | Fire Fighting installations to all stadium compounds |
| 10 | Repair of all damaged guiding Mesh and steel Handrails to the VIP Stage and steel Handrails to the stairs leading to spectaculars toilets including brushing them to remove the old paints and painting them with the new paints |

*Chanzo: Uchambuzi wa BoQ za Mkataba, BoQ zilizoidhinishwa kwa kazi za ziada na ziara ya eneo iliyofanywa na Wakaguzi, 2023*

Kutokana na kujitokeza kwa dosari hizo ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara: -

(i) Kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti mzuri wa mikataba kupitia Mshauri Elekezi katika kutekeleza majukumu yake.

(ii) Kuhakikisha vitu hivi na vingine vyote ambavyo Wizara inaviona vina umuhimu ni vyema kujumuishwa katika kazi za ukarabati ili kufikia mahitaji ya uwanja kuweza kutumika kama ilivyokusudiwa.

(iii) Kuhakikisha kuwa inatoa kazi kwa kampuni za ushauri zenye uwezo wa usimamizi wa mradi kuanzia hatua ya awali hadi kumalizika kwa mradi ili kunusuru kujitokeza kwa ongezeko la gharama zisizo za lazima kwa mradi.

### 3.7.5 Tozo ya Bidhaa za aina moja, ambayo hutumia Vifaa sawa na ukubwa sawa lakini imebainishwa kuwa na kiwango Tofauti katika BoQ za Mkataba

Kifungu nambari 43.2(c) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kwamba, ikiwa kazi inalingana na maelezo ya bidhaa katika makisio ya gharama za vifaa vya ujenzi, kiwango cha makisio ya gharama za vifaa kitatumika kuhesabu thamani ya utofauti.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa, bidhaa ya usambazaji na Ufungaji wa milango ya Vyoo vyenye urefu na upana wa futi 2.5x7 (Aluminium) ilivyoainishwa kwenye BoQ ya Mkataba chini ya vitu viwili tofauti na viwango viwili tofauti licha ya mabadiliko yaliyofanywa katika Sehemu ya Ufafanuzi ambayo iliunda sehemu ya hati ya zabuni kwa kubadilisha milango ya mbao kwa milango ya alumini (aluminium). Maelezo yanawasilishwa kwenye jadweli hapa chini:-

**Jadweli Nambari 22: Uchambuzi wa BoQ za Mkataba**

| Kipengele | Maelezo | Idadi katika Kipengele A | Idadi katika Kipengele H | Kipimo | Kiwango katika Kipengele A (R) | Kiwango katika Kipengele H (Z) | Tofauti ya M=Z-R |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Usambazaji na kuweka Milango ya Vyoo 2.5x7 feet ( Aluminium ) | 68 | 3 | Nr | 425,000 | 2,750,000 | 2,325,000 |

*Chanzo: Uchambuzi wa BoQ za Mkataba uliofanywa na Wakaguzi, 2023*

Jadweli hapo juu linaonesha kwamba Milango ya aluminiaum yenye kuonyesha vigezo na ukubwa unaolingana ambapo hupimwa kwa kipimo cha aina moja vilibainika kuwa na gharama tofauti ambapo kipimo cha kwanza cha mlango katika jengo kuu kilikua na thamani ya shilingi 425,000 na kipimo cha pili cha mlango wa vyoo vya watazamaji kilikua na thamani ya shilingi 2,750,000 na kupelekea kujitokeza kwa ziada ya shilingi 2,325,000 kwa kiwango ambacho kilitozwa kwa kila mlango wa aluminiaum wa choo cha watazamaji.

Kutokana na maelezo yaliyopo hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuwa na usimamizi wa karibu na Mshauri Elekezi kufanya mapitio mapya ya gharama zilizowasilishwa ili kunusuru kujitokeza kwa ongezeko la gharama za mradi zisizo za lazima.

### 3.7.6 Upungufu wa vipimo kwa vifaa vilivyomo kwenye BoQ za mkataba

Mapitio ya BoQ za Mkataba kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya uwanja wa michezo Gombani Pemba kupitia ziara ya ukaguzi iliyofanywa kuanzia tarehe 20 Julai 2023 hadi tarehe 23 Julai 2023 ilibainika kuwa kulikuwa na baadhi ya vifaa katika BoQ ambavyo vilikuwa chini ya kipimo kwa idadi inayohitajika kulingana na utekelezaji wa kazi za mradi kama inavyoonekana katika jadweli hapa chini: -

**Jadweli Nambari 23: Uchambuzi wa BoQ ya Mkataba**

| Kipengele | Maelezo | Idadi katika BoQ ya Mkataba | Idadi kulingana na uthibitisho wa eneo | Kwa kila kimoja | Kiwango katika BoQ ya Mkataba | Kiasi katika mkataba BoQ (B) | Kiasi ambacho kitakuwa mara baadaya milango yote kuwekwa (a) | Tofauti C=A-B |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Usambazaji na kuweka Milango ya Vyoo vya watazamaji 2.5x7 feet ( Aluminium) | 3 | 62 | Nr | 425,000 | 1,275,000 | 26,350,000 | 25,075,000 |

*Chanzo: Uchambuzi wa BoQ za Mkataba ulifanywa na wakaguzi, 2023*

Kutokana na jadweli hapo juu linaonesha kwamba kujitokeza kwa dosari ya makadirio ya vifaa vinavyohitajika katika BoQ pamoja na thamani halisi ya fedha ya ununuzi wa kila kifaa jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa gharama ya ziada ya shilingi 25,075,000.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu inaweza kuashiria ya kwamba mshauri elekezi hakuwa na uwezo wa usimamizi wa kazi alizopaswa kusimamia kwa mujibu wa mkataba, hata hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kukosekana kwa wataalamu wenye uzoefu wa kusimamia shughuli za utekelezaji wa mradi kutoka Wizarani ambao wangetoa usaidizi au ushauri wakati wa kuandaa na kupitia BoQ kabla ya kuanza kutumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha inakuwa makini katika uandaaji na utayarishaji wa BoQ kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

### 3.7.7 Kukosekana kwa ushahidi wa kuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi (Performance Security)

Kifungu nambari 55.1 cha GCC kinaeleza ya kwamba hati ya dhamana ya utendaji kazi itawasilishwa kabla ya tarehe iliyoainishwa katika barua ya kukubali kufanya kazi ambapo hati hiyo itakuwa halali kimatumizi hadi siku 28 kuanzia siku iliyotolewa cheti cha ukamilishaji wa kazi kwa mujibu wa hati ya dhamana ya benki na vile vile itadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe iliyotolewa hati ya kukamilisha kazi kwa mujibu wa hati ya dhamana.

Ukaguzi umebaini kuwa na hati ya dhamana iliyowasilishwa na Mkandarasi kwa Wizara jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya masharti maalum ya mkataba, vile vile hakukuwa na makabidhiano ya hati ya dhamana.

Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana kunaweza kupelekea kujitokeza kwa ukosefu wa fedha za umma na kuisababishia hasara Serikali pindipo mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza masharti ya mkataba au kushindwa kuendelea na kazi kwa sababu mbali mbali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha unasimamia vyema makubaliano ya mkataba ili kunusuru kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

### 3.7.8 Kukosekana kwa maandalizi mazuri ya hati za malipo ya muda (IPCs)

Kifungu nambari 6.2(n) cha Masharti ya Marejeo (ToR) ya mkataba wa utoaji wa huduma za ushauri kwa ajili ya kubuni, kusimamia na kufanya ukarabati wa uwanja wa michezo wa Gombani Pemba, kilimtaka Mshauri kuandaa hesabu za kazi zilizofanywa, kazi zilizokamilika na kutoa IPC kwa idhini ya Wizara.

Katika ukaguzi wa IPC 1 iliyoandaliwa na mshauri elekezi, ukaguzi ulibaini kwamba mshauri aliandaa muhtasari wa hati ya malipo ya muda kwa tathmini ya kifedha na sio thamani ya muhtasari unaojumuisha malipo ya kazi iliyofanywa kwa kuorodhesha mgawanyiko wa kazi zilizofanywa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa mshauri elekezi aliwasilisha kiasi tofauti cha malipo kabla ya idhini ya Bodi ya Zabuni bila kuonyesha mchanganuo uliojumuisha kazi zilizofanywa kwa mujibu wa cheti cha malipo ya muda (IPC).

Kufanya malipo ya kazi bila ya kuwa na IPC iliyotayarishwa na kupitishwa katika Bodi ya Zabuni inapelekea uwepo wa utendaji duni wa timu ya washauri elekezi pamoja na ukosefu wa ukaguzi yakinifu katika mradi unaofanywa na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) kama karani wa kazi ya mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba unafanya malipo ya IPC zilizotayarishwa na kuhakikiwa na Mshauri elekezi baada ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

### 3.7.9 Kulipa Kampuni ya Ushauri shilingi 70,000,000 mbali na kutotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma ya Ushauri

Kiambatisho A, Hadidu rejea (ToR) za Mkataba wa utoaji wa huduma za ushauri kwa ajili ya kubuni na kusimamia kwa ajili ya kudumisha uwanja wa michezo wa Gombani Pemba, ilimtaka Mshauri kubuni mradi huo ipasavyo.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mkataba wa Wizara na kubaini kwamba Mshauri Elekezi hakuandaa michoro yoyote ya ukarabati au ujenzi kwa ajili ya kazi za ukarabati, hivyo wazabuni walipewa hati za zabuni bila ya michoro na kabla ya kusaini utekelezaji wa kazi Mkandarasi hakupewa michoro yoyote kutoka kwa mshauri. Baada ya hapo, mkandarasi katika mpango wake na gharama aliamua kuendeleza michoro iliyojengwa ya muundo wa uwanja uliopo lakini mshauri hakuchukua hatua yoyote ya kuidhinisha kama michoro ya ujenzi.

Kwa mujibu wa mkataba, kuna baadhi mkataba ambayo inahitaji mkandarasi kujenga miundombinu mipya kama vile miundo ya ujenzi ikiwa ni pamoja na kuweka Transforma na jenereta, michoro kwa ajili ya chumba cha wachezaji na sehemu ya kupumzikia waheshimiwa na miundo ya ndani ya vyoo, na 3D na usanifu kuchora kwa benchi ya kiufundi.

Hata hivyo, mkandarasi amejenga miundo hii bila ya upatikanaji wa michoro iliyoidhinishwa na iliyopigwa muhuri na wataalamu kutoka kwa makampuni ya ushauri. Kazi hizo zilihitajika kutengenezwa vya kutosha na Mshauri wakati wa hatua za kubuni. Hii inamaanisha kuwa ikiwa kuna hatari yoyote kwenye mradi uliotekelezwa, sehemu ya uwajibikaji inaweza kuharibika.

### 3.7.10 Kuidhinisha malipo ya ziada kwa Mkandarasi, Wizara na Mshauri Elekezi

Katika mapitio zaidi ya Hati za Mkataba ukaguzi ulibainisha kuwa mbali ya Mkandarasi kuendelea kulipwa hadi ukaguzi unakamilika, mkandarasi huyo ameidhinisha malipo mengine kupitia barua yenye kumbukumbu namba DBL/P.1/2023 ya tarehe 6 Mei 2023 yenye thamani ya shilingi 658,790,839 (pamoja na VAT) ambayo hata Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imeridhia na sasa malipo yaliyoidhinishwa yapo Wizara ya Fedha tayari yanasubiri kulipwa kwa Mkandarasi. Maelezo yanawasilishwa katika jadweli hapa chini.

## Jadweli Nambari 24: Malipo kwa Mkandarasi Baada Wizara ya Fedha kutoa maombi ya Malipo yaliyoombwa na Mteja dhidi ya Kiasi cha Mkataba

| Namba | Aina ya Cheti | Malipo halisi kwa Mkandarasi (Tsh) | Kodi kwa ZRA (Tsh) | Kodi kwa TRA (Tsh) | Jumla ya Malipo ya Cheti kwa Mkandarasi (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyeti vya Malipo ya Awali | 507,895,652.17 | 36,521,739.13 | 15,582,608.70 | 560,000,000.00 |
| 2 | Cheti Namba 1 | 988,135,911.00 | 71,054,835.00 | 40,269,393.79 | 1,099,460,139.79 |
| 3 | Barua ya Mkopo iliyolipwa kwa mkandarasi | | | | 663,063,441.00 |
| 4 | Cheti cha malipo kilichoidhinishwa Namba 2 | | | | 658,790,839.00 |
| **Malipo ya jumla yaliyofanywa kwa mkandarasi hadi sasa** | | | | | **2,981,314,420** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Malipo na Cheti cha Malipo kilichoidhinishwa Namba 2 uliofanywa na Wakaguzi, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa mara baada ya Cheti kilichoidhinishwa Namba 2 chenye thamani ya shilingi 658,790,839 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kinalipwa na Wizara ya Fedha kwa Mkandarasi, jumla ya malipo yatakayofanyika kwa Mkandarasi yatakuwa shilingi 2,981,314,420 pamoja na VAT. Hii ina maana kwamba Mkandarasi amelipwa kiasi chote cha mkataba kiasi cha shilingi 2,800,000,000 Pamoja na VAT na ziada ya shilingi 181,314,420 pamoja na VAT na bila ya kurejesha malipo ya awali na pia bila ya makato yoyote ya fedha kwa ajili ya marejesho ya kazi zilizokwisha kutekelezwa.

Kutokana na hali hiyo kunaweza kujitokeza kuvuruga mtiririko wa malipo ya fedha kutoka kwa mlipaji jambo ambalo linaweza kusababisha utendaji duni wa kazi ambazo bado hazijatekelezwa, kukosekana kwa ubora wa kazi kutokana na kufanyika kwa malipo yote kabla ya kuthibitishwa kwa kazi iliyofanyika.

Aidha, uwepo wa usimamizi wa mkataba, usioridhisha kwa Wizara, Mshauri au Karani wa Kazi kumepelekea kufanyika kwa malipo ya hesabu ya kazi bila ya kuzingatia thamani halisi ya cheti cha malipo (IPC) au maandalizi ya ripoti za kifedha za mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kufanya hesabu ya kina ya kazi zilizotekelezwa na kulinganisha na malipo yaliyofanywa kuhusu kiasi cha mkataba ili kuwezesha usimamizi mzuri wa mikataba.

## 3.8 Vipengele vya Kiufundi (Ukaguzi wa Ubora, Upimaji wa Kazi, na upimaji wa vifaa) - Usimamizi wa Vipengele vya Ubora wa Mradi

Ukaguzi ulitathmini mambo ya kiufundi ya mradi na kubaini udhaifu katika utekelezaji wa mradi. Maelezo zaidi yanawasilishwa hapa chini: -

### 3.8.1 Uhamasishaji Hafifu wa Mkandarasi

Ukaguzi ulitathmini uhamasishaji wa wakandarasi na kubaini kuwa kulikuwa na udhaifu katika uhamasishaji kazi za Mkandarasi. Maelezo yanawasilishwa katika vifungu vifuatavyo: -

### (a) Ukosefu wa Idhini ya Uingizwaji wa Wafanyakazi muhimu wa Mkandarasi na Meneja wa Mradi

Kifungu nambari 10.1 cha GCC kinamtaka Mkandarasi kuajiri watumishi muhimu waliotajwa katika kipengele cha wafanyakazi muhimu, kama inavyotajwa katika masharti maalum ya mkataba, kutekeleza kazi zilizotajwa katika kipengele au watumishi wengine walioidhinishwa na Meneja wa Mradi. Zaidi ya hayo, meneja wa mradi ataidhinisha uingizwaji wowote uliopendekezwa wa wafanyakazi muhimu ikiwa tu sifa na uwezo wao husika ni sawa au bora kuliko wafanyakazi waliotajwa katika orodha.

Mnamo tarehe 20 hadi 23 Julai, 2023 ukaguzi ulipitia taarifa zilizomo katika Ripoti za Maendeleo ya kila mwezi, hati ya Mkataba na kubaini kuwa wafanyakazi wote muhimu wa mkandarasi walikuwa wamebadilishwa kwenye eneo la ujenzi ukilinganisha na wafanyakazi walioorodheshwa katika mkataba. Hali halisi wa wafanyakazi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 25: Wafanyakazi muhimu waliohamasishwa dhidi ya Wafanyakazi Waliopo kwenye eneo la mradi**

| Kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa | | Kama ilivyothibitishwa kwenye eneo la mradi mnamo tarehe 20 Julai 2023 | | Yupo/ Hayupo |
|---|---|---|---|---|
| **Nafasi** | **Wafanyakazi kama ilivyo kwa Mkataba** | **Nafasi** | **Wafanyakazi kama ilivyothibitishwa kwenye eneo** | |
| Meneja wa Mradi | Aziz Moiz Qurban | Meneja wa Eneo | Renson Kinyaha | Kapatikana |
| Mhandisi wa Mitambo | Abdul Fereji Muhogora | Mhandisi wa Eneo | Majid Yusuf | Hakupatikana [2] |
| | | Mhandisi wa Umeme | Ben Kihomwe | Kapatikana |
| | | Mhandisi wa Eneo(Mhandisi wa Kiraia) | Mohamed Hamad Shehe | Kapatikana (Kachukua nafasi ya Majid Yusuf) |

2 Aliondoka kwenye Eneo la mradi katikati ya Julai, 2023 kwa mradi mwingine wa Kampuni

| Kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa | | Kama ilivyothibitishwa kwenye eneo la mradi mnamo tarehe 20 Julai 2023 | | Yupo/ Hayupo |
|---|---|---|---|---|
| Nafasi | Wafanyakazi kama ilivyo kwa Mkataba | Nafasi | Wafanyakazi kama ilivyothibitishwa kwenye eneo | |
| Mhandisi wa Ufundi wa Kiraia | Malik Othman Bauji | Mtathmini wa gharama Quantity Surveyor | Renson Kinyaha | Kapatikana |
| Mhandisi wa Umeme | Charles Madoshi | Mwangalizi wa eneo site Foreman Technician | Ruthi & Sililo | Hakupatikana |
| Mhandisi wa TEHAMA | Jayesh Bhatt | - | - | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa zilizokusanywa kutoka Hati za Mkataba na Ripoti za Maendeleo ya Kila Mwezi, 2023*

Jadweli hapo juu inaonyesha kuwa, kulingana na Ripoti ya Maendeleo ya Kila mwezi ya Juni 2023, Mkandarasi alikuwa amebadilisha asilimia 100 ya wafanyakazi muhimu kama ilivyo katika hati za mkataba. Hata hivyo, hakuna ushahidi uliowasilishwa kwa ukaguzi na Mkandarasi kuonyesha kwamba mkandarasi alipata kibali cha uingizwaji wa wafanyakazi muhimu kutoka kwa Meneja wa Mradi.

Ukaguzi huo pia ulibaini kuwa, uingizwaji wa watumishi wote muhimu katika mradi kama inavyoonyeshwa katika mkataba wa kazi bila idhini kutoka kwa Meneja wa Mradi ulitokana na usimamizi duni wa Mshauri.

Ubadilishaji wa wafanyakazi wote muhimu waliowekwa katika mkataba bila ya idhini kutoka kwa Meneja wa Mradi hauhakikishi kuwa Mkandarasi ataweza kutekeleza mkataba kwa ufanisi, kwa weledi na kwa kufuata kikamilifu maelezo, michoro, maelekezo, na masharti ya mkataba.

### (b) Kukosekana kwa ushahidi juu ya sifa za wafanyakazi muhimu wa mkandarasi

Kifungu nambari 10.1 cha GCC kinamtaka Mkandarasi kuajiri watumishi muhimu waliotajwa katika orodha ya Wafanyakazi Muhimu, kama inavyotajwa katika Masharti Maalum ya Mkataba, kutekeleza kazi zilizotajwa katika orodha au watumishi wengine walioidhinishwa na Meneja wa Mradi.

Ukaguzi ulipitia majalada ya mradi ili kutathmini sifa za wafanyakazi muhimu walioajiriwa na mkandarasi na kubaini kuwa kulikuwa na ubadilishwaji wa wafanyakazi muhimu, hata hivyo, hakukuwa na ushahidi uliowasilishwa kwa ukaguzi kutathmini sifa zao. Maelezo ya wafanyakazi hao ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 26: Orodha ya Wafanyakazi Muhimu wa Mkandarasi na Sifa zinazohitajika**

| Jina la wafanyakazi | Nafasi ya Kazi | Ubadilishaji | Sifa | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Elimu | Mtaalamu |
| Aziz Moiz Qurban | Meneja wa Mradi | Renson Kinyaha | Hazikupatikana kwa ukaguzi | Hazikupatikana kwa ukaguzi |
| Abdul Fereji Muhogora | Mhandisi wa Mitambo | Majid Yusuf | Hazikupatikana kwa ukaguzi | Hazikupatikana kwa ukaguzi |
| Malik Othman Bauji | Mhandisi wa Ufundi wa Kiraia | Renson Kinyaha | Hazikupatikana kwa ukaguzi | Hazikupatikana kwa ukaguzi |
| Charles Madoshi | Mhandisi wa Umeme | Ruthi & Sililo | Hazikupatikana kwa ukaguzi | Hazikupatikana kwa ukaguzi |
| Jayesh Bhatt | Mhandisi wa TEHAMA | - | - | - |
| | Mhandisi wa Umeme | Ben Kihomwe | Hazikupatikana kwa ukaguzi | Hazikupatikana kwa ukaguzi |
| | Wakala wa Eneo (Mhandisi wa Kiraia) | Mohamed Hamad Shehe | Hazikupatikana kwa ukaguzi | Hazikupatikana kwa ukaguzi |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi juu ya Sifa za Wafanyakazi wa Mkandarasi, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa, kwa wafanyakazi wote muhimu waliobadilishwa, hakuna ushahidi wa sifa zao za elimu na sifa za usajili wa bodi ya kitaaluma kwa wafanyakazi muhimu waliobadilishwa.

Ukaguzi uliomba vyeti vya sifa za elimu na vyeti vya usajili wa Bodi ya Wakandarasi wakati wa ziara ya eneo la mradi kutoka tarehe 20 Julai, hadi 31 Julai, 2023 nyaraka hizo hazikupatikana kwa ajili ya ukaguzi jambo ambalo limetia shaka ya kwamba wafanyakazi hao wamekosa sifa kubalifu na vigezo vilivyowekwa na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi, hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa idhini ya meneja wa mradi kuhusu uingizwaji wa wafanyakazi jambo ambalo ni kwenda kinyume na matakwa ya masharti ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaongeza umakini katika kuipata timu ya Mshauri Elekezi wenye sifa na uwezo wa kusimamia miradi ya maendeleo pamoja na kuwasimamia kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa weledi, ufanisi na kwa mujibu wa taaluma zao.

### 3.8.2 Uhamasishaji mdogo (mobilization) wa wafanyakazi muhimu wa Mshauri

Ukaguzi ulitathmini uhamasishaji wa washauri na kutambua kuwa kulikuwa na uhamasishaji duni. Maelezo yanawasilishwa katika vifungu vifuatavyo: -

#### (a) Ukosefu wa ushahidi juu ya uthibitisho wa upatikanaji wa wataalam muhimu wa mshauri kwa mradi

Kifungu nambari 13.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba kilihitaji uthibitisho wa upatikanaji wa Wataalam muhimu ili kuanza kazi ya kuwasilishwa kwa Wizara kwa maandishi kama taarifa iliyoandikwa iliyosainiwa na kila Mtaalam muhimu na mshauri mkuu.

Mapitio ya kumbukumbu za Mradi yalibainisha kuwa hakukuwa na ushahidi unaoonyesha uwasilishaji wa uthibitisho wa wataalam muhimu wa mshauri kwa Wizara ili kuthibitisha upatikanaji wao. Hii ni kutokana na usimamizi duni wa mkataba na Mshauri wa Usimamizi.

Kushindwa kuwa na uthibitisho juu ya upatikanaji wa wataalam muhimu kunasababisha hatari ya kukosa wataalam ambao wako kwenye eneo la kazi kwa kufuata mahitaji ya mkataba jambo ambalo linaleta hatari ya kwamba wafanyakazi hao wana uwezekano wa kukosa sifa zinazofaa kwa usimamizi wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa Taasisi za Usimamizi wa Mashauri zinasimamia ipasavyo usimamizi wa mikataba na kwamba katika miradi ya baadae uthibitisho wa upatikanaji wa watumishi muhimu unafanyika kulingana na mahitaji ya mkataba.

#### (b) Kukosekana kwa sifa ya kutosha ya kampuni ya ushauri

Kwa mujibu wa Sehemu ya 7 na 7.1 ya Masharti ya Marejeo (ToR), Mkataba wa Huduma ya Ushauri unahitaji huduma ya ushauri kutolewa na kampuni inayostahiki ya taaluma nyingi au muungano na timu ya Wasanifu, Wahandisi, (Miundo, Umeme, TEHAMA, na Mitambo) na Watafiti wa kutosha kukidhi mahitaji ya kazi.

Ukaguzi ulibaini kuwa kampuni ya ushauri ya M/S Diamond Builders Limited inayohusika na utoaji wa huduma za ushauri kwa kudumisha Uwanja wa Gombani haikuwa na taaluma nyingi au muungano na timu ya Wasanifu, Wahandisi, (Miundo, Umeme, TEHAMA, na Mitambo) na Watafiti wa kutosha ili kuweza kukidhi mahitaji ya kazi. Muundo wa kampuni ni kinyume na mahitaji ya Masharti ya hadidu rejea za kazi hii. Mapitio zaidi ya majalada ya Mradi yalibaini kuwa kampuni hiyo inaundwa na wafanyakazi wafuatao kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 27: Muundo wa wafanyakazi wa kampuni ya Mshauri Elekezi**

| Namba | Nafasi | Jina | Upatikanaji katika Eneo kulingana na Ripoti ya Maendeleo ya Kila Mwezi | Maoni baada ya ziara ya eneo na ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mshauri Mkuu (Diamond Builders) | Victor B. Ndozero | Kapatikana | Anapatikana Dar es Salaam. Ofisi Kuu ipo Unguja na anahudhuria eneo la kazi kwa vipindi (periodically) |
| 2 | Mhandisi wa Kiraia | Ibrahim M. Salim | Kapatikana | Hakuwa kwenye eneo la mradi. Kulingana na mwakilishi wa mshauri huyo, mtu huyo alisafiri kwenda kwenye dharura |
| 3 | Watathmini wa gharama za mradi (Quantity Surveyor) | Mary Minja | Kapatikana | Alikuwepo kwenye eneo na ni mratibu wa mradi huo, anapatikana kwenye eneo wakati wote. Kwa mujibu wa mahojiano hayo, yeye ni mtaalamu wa manunuzi na usambazaji |

*Chanzo: Uchambuzi wa Takwimu zilizokusanywa na wakaguzi kutoka Eneo la mradi, 2023*

Aidha, ukaguzi uliomba vyeti vya usajili wa kampuni kwa mshauri, na nyaraka zifuatazo zilitolewa kwa ajili ya uhakiki kama inavyoonyeshwa kwenye Jadweli hapa chini:-

### Jadweli Nambari 28: Maelezo ya Mahitaji ya Usajili na Leseni

| Namba | Jina la Cheti | Namba | Jina la Taasisi lilitoa Cheti | Tarehe ya Kutolewa kwa Cheti |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Cheti cha Nambari ya Usajili wa Mlipakodi (VAT) | 07003544U | Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) | 1 Julai, 2022 |
| 2 | Cheti cha kuundwa kwa Kampuni | Z0000072798 | Msajili wa Makampuni | 29 Julai, 2020 |
| 3 | Cheti cha Usajili wa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi | 156-254-940 | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 24 Mei, 2022 |
| 4 | Cheti cha Usajili kama Mshauri katika Mkandarasi wa Ujenzi | C000808 | Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma -Zanzibar | 17 Juni, 2022 |
| 5 | Cheti cha Usajili wa Leseni ya Biashara kwa Ushauri | WBC00-AK-JB1496 | Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" | 19 Mei, 2022 |
| 6 | Cheti cha Usajili wa Kampuni ya Uhandisi wa Ushauri | 22/CEF-545 | Bodi ya Usajili ya Wasanifu, Wahandisi,na Watathmini wa gharama za mradi | 18 Juni, 2022 |

*Chanzo: Uchambuzi uliofanywa na Wakaguzi kwenye Vyeti vya Usajili, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa vyeti vitano kati ya sita vya usajili na bodi husika vilitolewa baada ya kupokea Taarifa ya Tuzo za tarehe 20 Aprili 2022 na baada ya Mkutano wa Majadiliano uliofanyika tarehe 29 Aprili 2022, ambapo cheti kimoja tu cha usajili (Certificate of Incorporation of the Company) kilitolewa tarehe 29 Julai 2020. Hii ina maana kwamba kampuni ya M/S Diamond Builders Limited ilifanya juhudi za kukamilisha usajili wa kampuni hiyo baada ya kupata hakikisho la kushiriki katika usimamizi wa mradi huo, ingawa, kampuni hiyo haikuzingatia mahitaji ya uzoefu wa angalau miaka saba.

Kukamilisha usajili baada ya mkutano wa mazungumzo kunaleta hatari kwamba, kampuni haikuhakikisha kutoa huduma kwa ufanisi kutokana na ukosefu wa kiwango cha kuridhisha cha uzoefu katika utoaji wa huduma za ushauri.

Uongozi wa Wizara unapaswa kuhakikisha kuwa miradi ya baadaye inahusisha Washauri tu wenye sifa zinazohitajika kama ilivyo kwa hadidu rejea ili kuhakikisha usawa na uwazi katika mchakato wa ununuzi.

### 3.8.3 Uzoefu usioridhisha wa kampuni katika ununuzi wa utoaji huduma za ushauri kwa uwanja wa Gombani

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Masharti ya Marejeleo (Qualifications) na 7.1 (Kampuni ya Ushauri), kampuni hiyo itakuwa na uzoefu wa miaka saba na imefanya angalau kazi tano zinazofanana, hasa katika Mkoa wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, na kuthibitisha kazi ya uzoefu uliofanywa. Kampuni hiyo inapaswa kuwa na angalau mmoja wa wafanyakazi wenye ujuzi wa lugha ya Kiswahili.

Mapitio ya Cheti cha usajili wa Kampuni yamebainisha kuwa Kampuni ya M/S Diamond Builders Limited ilisajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi, na Watathmini wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama kampuni ya uhandisi wa ushauri tarehe 18 Juni, 2022.

Itakumbukwa kuwa Wizara ilitoa Taarifa ya Tuzo za Huduma za ushauri kwa Kampuni ya M/S Diamond Builders Limited tarehe 18 Aprili, 2022 na Kampuni ya Diamond Builders Limited ilikubali zoezi hilo tarehe 20 Aprili, 2022, mkutano wa majadiliano kwa ajili ya kazi ya huduma ya ushauri ulifanyika tarehe 29 Aprili, 2022, na mkataba wa mradi huu ulisainiwa mnamo Julai, 2022. Hii inamaanisha kuwa Wizara ilianzisha mchakato wa ununuzi wa huduma za ushauri na kampuni isiyo na sifa kwa sababu, wakati kampuni hiyo iliwasilisha zabuni mnamo tarehe 1 Aprili, 2022, kampuni hiyo haikuwa na cheti cha usajili kama kampuni ya uhandisi wa ushauri; Pia inamaanisha kuwa, wakati mkataba ulisainiwa (Julai, 2023), kampuni hiyo ilikuwa na uanzishwaji wa mwezi mmoja tu ambao ni kinyume na mahitaji ya hadidu rejea ambayo ilihitaji uzoefu wa miaka saba.

Vivyo hivyo, mapitio ya ripoti ya tathmini ya zabuni iliyoambatanishwa na Mkataba wa Huduma ya Ushauri ilionyesha kuwa timu ya tathmini ilitoa alama ya wastani ya alama 8 kati ya 10 (sawa na asilimia 80) kwa uzoefu maalum wa mshauri kama kampuni, hata hivyo, mshauri wakati wa tathmini hakuwa na sifa ya usajili wa kampuni ya ushauri na Bodi ya Msanifu, Wahandisi, na Watathmini wa mradi. Kwa hivyo alama ya 8 kati ya 10 iliyotolewa na timu ya tathmini ya zabuni haikuwa sahihi kwa mujibu wa utaratibu.

Kwa mujibu wa Sehemu ya 7.2 ya Masharti ya Marejeo (ToR) na 7.2.1, timu ya Mshauri lazima iwe na wafanyakazi muhimu wenye sifa na uzoefu kama ilivyoelezwa katika Jadweli hapa chini: -

**Jadweli Nambari 29: Sifa za Wafanyakazi muhimu wa Mshauri aliyeorodheshwa katika Ripoti za Maendeleo ya Kila Mwezi (Januari hadi Juni, 2023)**

| Nafasi | Sifa | Idadi ya chini ya miaka | Sifa za wafanyakazi waliopo | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Sifa | Kiwango cha chini cha miaka |
| Kiongozi wa Timu / Mbunifu | Angalau shahada au Kozi inayoendana katika Usanifu | Miaka 9 ya uzoefu wa jumla na uzoefu wa miaka sita katika usimamizi wa mradi hasa katika Ujenzi wa Uwanja au Ubunifu wa Ujenzi wa Biashara na Usimamizi | Haijapatikana kwa ukaguzi | Haikupatikana kwa ukaguzi |
| Mhandisi wa Kiraia / Miundombinu | Angalau shahada au Kozi inayoendana na katika Uhandisi wa Miundo | Uzoefu wa miaka 5 katika kubuni na kusimamia kazi za ujenzi ikiwezekana katika nchi zinazoendelea | Haijapatikana kwa ukaguzi | Haikupatikana kwa ukaguzi |
| Mtathmini wa mradi | Angalau shahada au Kozi inayoendana katika Kutathmini mradi | Uzoefu wa miaka 7 katika ujenzi kabla ya kuanza kwa kazi | Haijapatikana kwa ukaguzi | Haikupatikana kwa ukaguzi |
| Mhandisi wa Umeme | Angalau shahada au Kozi inayoendana katika Uhandisi wa Umeme | Uzoefu wa miaka 5 katika hali kama hiyo ya mradi | Haijapatikana kwa ukaguzi | Haikupatikana kwa ukaguzi |
| Mhandisi wa Mitambo | Angalau shahada au Kozi inayoendana katika Uhandisi wa Mitambo | Angalau uzoefu wa miaka 5 katika hali kama hiyo ya mradi | Haijapatikana kwa ukaguzi | Haikupatikana kwa ukaguzi |

| Nafasi | Sifa | Idadi ya chini ya miaka | Sifa za wafanyakazi waliopo | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Sifa | Kiwango cha chini cha miaka |
| Mhandisi wa TEHAMA | Angalau shahada au Kozi inayoendana sawa katika TEHAMA | Angalau uzoefu wa miaka 7 katika hali kama hiyo ya mradi | Haijapatikana kwa ukaguzi | Haikupatikana kwa ukaguzi |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi juu ya Masharti ya Marejeo (ToR), 2023*

Aidha, ToR ilihitaji wafanyakazi wa mshauri kusajiliwa na bodi husika za kitaaluma. Mapitio ya majalada ya Mradi yalionyesha kuwa hakukuwa na ushahidi wa usajili wa wafanyakazi wa mshauri wanaosimamia mradi huo kwenye eneo la ujenzi. Vile vile, kupitia mapitio ya hati ya mkataba, ukaguzi ulibaini "Curriculum Vitae" ya wahandisi wawili tu ambao ni Mhandisi wa Mitambo (Ahmad H. Salum) na Mhandisi wa Umeme (Mohamed Mohamed), hata hivyo ukaguzi umebaini wahandisi hao hawakupatikana katika eneo la utekelezaji wa mradi.

Aidha, ukaguzi ulipewa vyeti vya usajili wa bodi ya elimu na kitaaluma kwa maafisa wa mshauri kwa wafanyakazi wa kiufundi ambao walitajwa kuwa sehemu ya wataalam muhimu kwenye timu ya mshauri, na maelezo juu ya sifa za wataalam huwasilishwa katika jadweli hapa chini.

## Jadweli Nambari 30: Maelezo kulingana na vyeti vya Elimu na Utaalamu

| Jina la Mtaalam | Nafasi | Sifa | | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|---|
| | | Elimu | Usajili wa kitaalamu | |
| Abdulla Omar Abbas | Mtathmini wa mradi | Shahada ya Pili katika Usimamizi wa Uhandisi | Amesajiiwa Mshauri Mtathmini wa mradi na Bodi ya Wasanifu, Wahandisi, na Watathmini Zanzibar | Ana sifa zinazofaa, hata hivyo, hajaorodheshwa katika hati za mradi kama vile ripoti za maendeleo ya kila mwezi |
| Salim S. Hamad | Umeme - Uhandisi wa Umeme | Shahada katika Umeme - Uhandisi wa Umeme | Cheti cha Uhitimu wa Kitaalamu hakijatolewa. | Kutozingatia mahitaji ya mkataba, hajaorodheshwa katika nyaraka za mradi kama vile ripoti za maendeleo ya kila mwezi |
| Celestine Rwehumbiza Kazoba | Kiongozi wa Timu -Mhandisi wa Kiraia / Miundombinu | Shahada ya Sayansi katika Uhandisi wa kiraia, Chuo Kikuu cha Dar- Es- salaam, Tanzania. Diploma ya kuhitimu katika Uhandisi wa Usafi, (Msc. Equivalent), Taasisi ya Uhandisi wa Hydraulic, Delft Uholanzi | Cheti cha Uhitimu wa Kitaalamu hakijatolewa, hata hivyo, kwa mujibu wa CV, yeye ni Mhandisi wa Ushauri wa ERB, Tanzania, Reg. no. 299, hakuna ushahidi juu ya usajili Zanzibar | Mkataba wa huduma ya ushauri haumtambui kama kiongozi wa timu. Kiongozi wa timu hiyo ni Victor B. Ndozero |
| Christian Safari | Mhandisi wa umeme | Haijatolewa | Mhandisi wa Kitaalamu aliyesajiliwa na ERB, Tanzania. Hakuna ushahidi wa usajili Zanzibar | Hakuna kifungu cha Cheti cha Shahada. Hajaorodheshwa katika nyaraka za mradi |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi juu ya Vyeti vya Uhitimu wa Elimu na Utaalam, 2023*

Jadweli hapo juu limeonyesha kuwa mshauri ametoa hati za kufuzu za elimu na taaluma, hata hivyo, wahandisi hawajaorodheshwa katika hati yoyote ya mradi hadi wakati ukaguzi huu unakamilika. Kwa kuongezea, hakuna ushahidi wa uthibitisho wa upatikanaji wao kwa mradi huu kulingana na kifungu cha 13.1 cha SCC. Hii inamaanisha kuwa hakuna uhakika katika ushiriki wa wahandisi kama hao kwa mradi huu.

### 3.8.4 Ukosefu wa ushahidi juu ya sifa za wataalam wa mshauri

Sehemu ya 7.2.1 ya Masharti ya Marejeo (ToR) inahitaji wafanyakazi muhimu wa mshauri kusajiliwa na bodi husika za kitaaluma. Ukaguzi ulipitia mawasiliano ya mradi na mkataba wa huduma ya ushauri na alibainisha hakukuwa na uwasilishaji wa ushahidi juu ya sifa za Wataalam muhimu wa Mshauri. Maelezo yanawasilishwa kwenye jadweli hapo juu.

Usimamizi wa mkataba usioridhisha na Mshauri na Mteja kuhusu idhini ya uingizwaji wa wafanyakazi muhimu na Meneja wa Mradi na utoaji wa sifa za wafanyakazi muhimu katika mradi wa uthibitishaji.

Ukosefu wa ushahidi wa kutathmini sifa za wafanyakazi wapya muhimu unaleta hatari kwamba, wafanyakazi muhimu wanaweza kukosa sifa zinazoendana na utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kumuelekeza Mshauri Elekezi kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa bidii, weledi na taaluma. Aidha, Wizara kuhakikisha inasimamia upatikanaji wa sifa za watumishi wa mshauri elekezi kwa miradi ijayo ili kuepuka kujitokeza kwa kasoro katika utekelezaji wa miradi.

### 3.8.5 Tathmini ya Ubora wa Vifaa vilivyotumika Kukidhi Vigezo

Kifungu cha 17.1 cha GCC kilimtaka Mkandarasi kujenga na kufanya kazi kulingana na Maelezo na Michoro.

Vigezo na michoro iliyoandaliwa ilieleza mahitaji tofauti ya ubora wa vifaa vya kutumika na ubora wa kazi itakayofanywa ambayo itahitaji idhini ya Mhandisi. Ukaguzi ulikagua nyaraka zote za mradi na kuangalia eneo la utekelezaji wa mradi na kufanya vipimo visivyo vya uharibifu kwenye miundo ya saruji iliyoimarishwa.

Uimara wa zege kutokana na utengenezwaji wake ulikaguliwa kwa kutumia Nyundo ya "Rebound" yenye Nambari ya utambuzi EL35-1480 ambayo ilithibitishwa na Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS) kwenye Maabara ya upimaji wa Mitambo tarehe 29 Agosti, 2022. Matokeo ya majaribio yaliyofanyika kwa kila sehemu kwenye miundo iliyojaribiwa imebainishwa katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 31: Matokeo ya majaribio yaliyofanyika juu ya Nguvu ya Zege ya Rebound Hammer

| Eneo/Aina ya Muundo | Mwanachama aliyejaribiwa / Alama | Sababu ya marekebisho Pembe ya matumizi | Nguvu iliyobainishwa (N/mm2) | Wastani wa Nguvu Iliyojaribiwa (N / mm2) | Maoni ya Wakaguzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Mnara wa 1 | A | 90 (Vertical) | 25 | 42 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | B | 90 (Vertical) | 25 | 41 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | C1 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 21 | Nguvu iliyobainishwa haikufikiwa |
| | C2 | 90 (Vertical) | 25 | 26 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | D | 90 (Vertical) | 25 | 41 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| Mnara wa 2 | A1 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 22 | Nguvu iliyobainishwa haikufikiwa |
| | A2 | 90 (Vertical) | 25 | 37 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | B1 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 25 | Nguvu iliyobainishwa haikufikiwa |
| | B2 | 90 (Vertical) | 25 | 37 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | C1 | 0 (njia ya kando) | 25 | 24 | Nguvu iliyobainishwa haikufikiwa |
| | C2 | 90 (Vertical) | 25 | 37 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | D1 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 26 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | D2 | 90 (Vertical) | 25 | 42 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |

| Eneo/Aina ya Muundo | Mwanachama aliyejaribiwa / Alama | Sababu ya marekebisho Pembe ya matumizi | Nguvu iliyobainishwa (N/mm2) | Wastani wa Nguvu Iliyojaribiwa (N / mm2) | Maoni ya Wakaguzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Mnara wa 3 | A | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 34 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | B | 90 (Vertical) | 25 | 44 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | C | 90 (Vertical) | 25 | 43 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | D | 90 (Vertical) | 25 | 42 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| Mnara wa 4 | A1 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 21 | Nguvu iliyobainishwa haikufikiwa |
| | A2 | 90 (Vertical) | 25 | 35 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | B1 | 90 (Vertical) | 25 | 36 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | B2 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 28 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | C1 | 90 (Vertical) | 25 | 33 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | C2 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 28 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | D1 | 90 (Vertical) | 25 | 33 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |
| | D2 | 0 (sideways/njia ya kando) | 25 | 28 | Nguvu iliyobainishwa ilitimizwa |

*Chanzo: Uchambuzi wa Matokeo ya Vipimo vya Hammer ya Rebound uliofanywa na Wakaguzi, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa matokeo ya majaribio yalipatikana kuwa mazuri na yalikidhi ubora wa chini ya kiwango halisi cha zege kilichoinishwa katika BoQ isipokuwa kwa vipimo vilivyochukuliwa kutoka pande za minara ya msingi. Hata hivyo, kwa pointi sawa zilizojaribiwa chini (-90 Degrees), alama zilipita vizuri. Hii inapelekea kutambulika kwamba saruji (zege) inaweza kuwa na tundu endelevu (honeycombs) wakati wa ujazaji wa zege jambo ambalo linaweza kupelekea kukosekana kwa uimara wa zege iliyowekwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa Mshauri Elekezi anamwelekeza Mkandarasi kwamba alama zote ambazo zilionyesha kuwa na kiwango cha chini katika matokeo ya vipimo vya zege katika mnara zijazwe na kuthibitishwa uimara wake ili kuweza kukidhi vigezo vinavyotakiwa.

### 3.8.6 Kufanyika kwa ukarabati wa Mnara bila ya kuwepo kwa Michoro ya Mnara na Ripoti ya Uchambuzi wa Miundo ya Mnara

Kwa mujibu wa Mkataba BoQ ukurasa 2/19, Bili Namba 2 (Main Building), Nambari ya kipengele 2 (Tower Renovation Works), na Nambari ya Bidhaa A ilimtaka Mkandarasi kufanya uchambuzi wa muundo na upakiaji wa mnara (kuanzisha mnara wa kuchora kwa minara iliyopo pamoja na vipimo vyote vya mnara kama vile vipimo kwa kila mnara), kuandaa na kuwasilisha ripoti ya uchambuzi wa Miundo ya Mnara na Michoro ya Mnara wa Taa za Uwanja zilizopo.

Kupitia ukaguzi wa nyaraka, ukaguzi ulibainisha kuwa Mkandarasi alianza ukarabati wa mnara bila kuangalia nguvu za uhimili wa minara iliyopo na kutoa ripoti kwa Mshauri na Wizara.

Ukosefu wa utoaji wa michoro ya mnara na ripoti ya uchambuzi wa muundo wa mnara na kuanza kwa ukarabati wa mnara bila kuangalia nguvu ya minara iliyopo inaweza kwa athari ambayo ikiwa mnara hautokuwa imara unaweza kuanguka, kuharibu miundombinu iliyopo, kusababisha vifo na kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa Mshauri Msimamizi anamwelekeza Mkandarasi kutoa michoro ya mnara na ripoti za uchambuzi wa miundo ya mnara.

## 3.9 Ukamilishaji na Ufungaji wa Mradi

### 3.9.1 Maandalizi ya Taarifa za Fedha za Mradi (Final Account)

Kwa mujibu wa Kifungu kidogo cha 60.1, Mkandarasi atampa Meneja wa Mradi akaunti ya kina ya jumla ya kiasi ambacho Mkandarasi anaona kuwa kinalipwa kabla ya mwisho wa Kipindi cha Dhima ya kasoro (Defects Liability). Meneja wa Mradi atatoa Cheti cha Dhima ya Kasoro na kuthibitisha malipo yoyote ya mwisho ambayo ni kutokana na Mkandarasi ndani ya siku 56 baada ya kupokea akaunti ya Mkandarasi ikiwa ni sahihi na imekamilika. Ikiwa sivyo, Meneja wa Mradi atatoa ndani ya siku 56 ratiba ambayo inasema upeo wa marekebisho au nyongeza ambazo ni muhimu. Ikiwa hesabu ya mwisho bado haijakidhi baada ya kuwasilishwa tena, Meneja wa Mradi ataamua juu ya kiasi kinacholipwa kwa Mkandarasi na kutoa cheti cha malipo. Mradi ulikuwa haujafikia hatua hii wakati wa ukaguzi huu mnamo Julai, 2023 kwa hivyo kipengele hiki hakikukaguliwa.

### 3.9.2 Usimamizi wa Mazingira (masuala ya usalama na kijamii), na Masuala ya Afya na Usalama wa Kazi

Ukaguzi ulitathmini kama mkandarasi alitekeleza ipasavyo hatari zinazohusiana na Mazingira, Usalama, na Athari za Jamii wakati wa utekelezaji wa mradi huo ikiwa zinaendana na matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na masharti ya Mkataba, na kubainisha udhaifu ufuatao:-

#### (i) Ukosefu wa vyeti vya EIA vya mradi

Kifungu cha 81 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 kinataka utafiti wa Tathmini ya Athari za Mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Aidha, kifungu cha 86 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 kinataka Baraza baada ya kuchunguza muhtasari wa mradi, kumtaka msimamizi wa mradi au kufanya utafiti wa Tathmini ya Athari za Mazingira na kuandaa Taarifa ya Athari za Mazingira ambayo itawasilishwa kwa Baraza kwa ajili ya ukaguzi.

Mapitio ya majalada ya Mradi yalibaini kuwa, hakukuwa na Cheti cha EIA cha mradi wa ukarabati na hakuna muhtasari wa mradi uliotayarishwa na uliowasilishwa kwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMC) ambalo linaweza kutoa fursa ya kuamua ikiwa mradi unahitaji EIA kamili au maandalizi tu ya Mpango wa Usimamizi wa Mazingira (EMP).

Ukosefu wa vyeti vya EIA ni kutokana na ukosefu wa mwongozo sahihi juu ya masuala ya mazingira na ukosefu wa kufanya muundo wa kina wa mradi ambao EIA inaweza kuwa kati ya masuala yaliyofunikwa.

Kukosekana kwa vyeti vya EIA au Muhtasari wa Mradi kumesababisha mradi kutokuwa na Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMP) au Mpango wa Usimamizi wa Afya na Usalama (HSMP) kama mikakati ya kutekeleza hatua za kupunguza hatari inayotokana na Ripoti ya EIA iliyoidhinishwa na Cheti cha EIA. Matokeo yake, Wizara haijahakikisha utekelezaji wa kutosha wa hatari zinazohusiana na mazingira, usalama, na athari za kijamii.

Kwa kuongezea, ukosefu wa Vyeti vya EIA umesababisha kuchelewa kupata eneo la utupaji kwa vifaa chakavu vilizoondolewa kama vile tartan zilzotolewa katika eneo la uwanja.

### 3.9.3 Ukosefu wa Utoaji wa Masuala ya Afya na Usalama

Ukaguzi huo ulibaini kuwa kulikuwa na ukosefu wa huduma za afya na usalama. Maelezo yanawasilishwa katika vifungu vifuatavyo:

#### (a) Utunzaji usiojitosheleza wa Afya na Usalama wa Wafanyakazi wa Mkandarasi

Kifungu kidogo cha 22.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kilimtaka Mkandarasi wakati wote kuchukua tahadhari zote za kutosha ili kudumisha afya na usalama wa wafanyakazi wake.

Mapitio ya Ripoti ya Maendeleo ya Kila Mwezi ya Januari hadi Juni, 2023 kwa utekelezaji wa mradi ilionyesha kuwa kulikuwa na utoaji wa vifaa vya usalama kama vile buti za usalama, miwani ya usalama, koti za kufanyia kazi, na kofia ngumu. Hata hivyo, wakati wa ziara hiyo ya kikazi katika eneo la mradi katika uwanja wa Gombani Julai, 2023 ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na wafanyakazi wakichanganya saruji na mchanga bila kuvaa barakoa za kujikinga na vumbi.

Sababu ya kutovaa barakoa ya kujikinga na vumbi ilitokana na kutotekelezwa kwa masuala ya afya na usalama. Hii ilichangiwa na ukosefu wa wafanyakazi wanaohusika na utekelezaji wa masuala ya afya na usalama.

Hii ilileta hatari ya kuwaweka wafanyakazi katika hatari ya kupata athari za kiafya kwenye mapafu ambayo yanaweza kusababisha kifo.

### (b) Kukosekana kwa Utoaji wa Vifaa vya Huduma ya Kwanza na Mahitaji ya vitu vya Usafi

Kifungu kidogo nambari 22.2 cha GCC inahitaji Mkandarasi kutoa vifaa vya huduma ya kwanza ambavyo vinapatikana wakati wote kwenye eneo la mradi na kwamba mipango inayofaa hufanywa kwa mahitaji yote muhimu ya ustawi na usafi kwa kuzuia magonjwa ya mripuko.

Vile vile, kifungu nambari 32 (1) cha Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa kazi ya 2005 kinahitaji kutoa na kudumisha sanduku la huduma ya kwanza au kabati kwa kiwango kilichoagizwa na sanduku la huduma ya kwanza au kabati kuwa na alama ya "FIRST AID" kuwa na vifaa au hifadhi ya vifaa vya huduma ya kwanza.

Mapitio ya Ripoti ya Maendeleo ya Kila Mwezi ya Januari hadi Juni, 2023 kwa mradi yalionyesha kuwa vifaa vya huduma ya kwanza vilipatikana wakati wote kwenye eneo la ujenzi, hata hivyo, kulingana na ziara ya eneo lililofanywa na ukaguzi, hakukuwa na utoaji wa vifaa vya huduma ya kwanza. Hii ilikuwa kinyume na kile kilichoripotiwa katika ripoti za maendeleo ya kila mwezi kwa kipindi kilichotajwa. Hii inaonyesha kuwa ripoti za maendeleo ya kila mwezi zimekuwa zikiripoti habari za uongo kuhusu upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza kwa kipindi chote cha miezi sita.

Pia, hakukuwa na taarifa juu ya uwepo wa mipango iliyofanywa kwa mahitaji yote muhimu ya ustawi na usafi kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya mripuko.

Ukaguzi huo ulibaini kuwa ukosefu wa mipangilio inayofaa kwa mahitaji yote muhimu ya ustawi na usafi kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya mripuko na ukosefu wa vifaa vya huduma ya kwanza ni kutokana na ukosefu/ kutokuwepo kwa afisa wa afya na usalama.

Ukosefu wa mipangilio inayofaa kwa mahitaji yote muhimu ya ustawi na usafi kwa kuzuia magonjwa ya mripuko inaweza kusababisha hatari ya magonjwa ya mripuko. Vile vile, ukosefu wa vifaa vya huduma ya kwanza hautoi uhakika utoaji wa huduma za afya za haraka kwa mfanyakazi ikiwa kuna dharura kama vile kuumia.

### (c) Ukosefu wa Taarifa ama Kumbukumbu juu ya Matukio ya Ajali

Kifungu kidogo cha 22.3 cha GCC kilimtaka Mkandarasi kumjulisha Mwajiri maelezo ya ajali yoyote mara tu inapowezekana baada ya kutokea kwake. Mkandarasi atatunza kumbukumbu na kutoa taarifa kuhusu afya, usalama, na ustawi wa watu, na uharibifu wa mali, kama Mwajiri anavyohitaji.

Mapitio ya Ripoti za Maendeleo za Kila Mwezi kuanzia Januari hadi Juni 2023 yamebaini kuwa hakukuwa na taarifa yoyote kuhusu masuala ya ajali ama kumbukumbu za matukio ya ajali. Ukosefu wa taarifa juu ya tukio la ajali inamaanisha kuwa hakuna ajali zilizowahi kutokea au ajali kutokea lakini hazijaripotiwa. Hii ni kutokana na ukosefu wa afisa wa afya na usalama katika mradi kwa kutotekeleza masuala ya afya na usalama.

### 3.9.4 Ukosefu wa Programu za Uhamasishaji juu ya VVU/UKIMWI

Mkandarasi ataendesha programu ya uhamasishaji wa VVU/ UKIMWI na atachukua hatua nyingine kama hizo ili kupunguza hatari za uhamisho wa VVU / UKIMWI au magonjwa mengine yoyote ya zinaa (STDs) kati ya wafanyakazi wa mkandarasi, wafanyakazi wa Mwajiri na jamii inayozunguka.

Mapitio ya Ripoti za Maendeleo ya Kila Mwezi za Januari hadi Juni, 2023 zilionyesha kuwa hakukuwa na taarifa juu ya masuala ya programu za uhamasishaji juu ya VVU/ UKIMWI zinazoonyesha kuwa mipango ya uhamasishaji juu ya VVU/ UKIMWI haifanywi.

Ukosefu wa programu za uhamasishaji wa VVU/UKIMWI kuna uwezekano wa kuwanyima wafanyakazi haki ya kupata elimu juu ya jinsi ya kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI. Hii inaweza kusababisha hatari ya kupata virusi vya HIV ambavyo vinaweza kusababisha vifo.

### 3.9.5 Utunzaji duni wa mazingira

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ulinzi duni wa mazingira katika utekelezaji wa mradi huo. Maelezo kamili yamefafanuliwa katika vifungu vifuatavyo:-

#### (a) Kukosekana kwa hatua muhimu za kulinda mazingira

Kifungu kidogo cha 20.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kilimtaka Mkandarasi kuchukua hatua zote za busara kulinda mazingira na kupunguza uharibifu na kero kwa watu na mali zinazotokana na uchafuzi wa mazingira, kelele, na mambo mengine yanayoweza kuharibu shughuli za mradi.

Mapitio ya Ripoti za Maendeleo za kila Mwezi kuanzia Januari hadi Juni, 2023 yalionyesha kuwa hakukuwa na taarifa yoyote kuhusu masuala ya kulinda mazingira na kupunguza uharibifu na kero kwa watu na mali zinazotokana na uchafuzi wa mazingira, kelele, na yanayoweza kuharibu shughuli za mradi.

Kushindwa kulinda mazingira na kupunguza uharibifu na kero kwa watu na mali zinazotokana na uchafuzi wa mazingira, kelele, na yanayoweza kuharibu shughuli za mradi ni kutokana na ukosefu wa maafisa wa afya na usalama kutotekeleza mahitaji ya usalama.

**(b) Kutokuchukuliwa hatua juu ya uondoaji wa takataka na maji taka kutoka katika shughuli zake**

Kifungu kidogo cha 20.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kilimtaka Mkandarasi kuhakikisha kwamba, uondoaji wa takataka na maji taka kutoka kwa shughuli zake hautazidi kiwango kilichowekwa katika sheria husika za mazingira.

Mapitio ya Mradi wa Waandishi wa Mradi yalibaini kuwa hakukuwa na Ripoti ya Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii ambayo Ukaguzi inaweza kutathmini ikiwa hatua zilichukuliwa juu ya takataka na maji taka kutoka katika shughuli zake ili kutozidi kiwango kilichowekwa katika sheria husika za mazingira.

**(c) Hatua zisizofaa za kuhakikisha kufuata kwa sheria za mahitaji ya Usalama na Afya ya Kazini (OHS)**

Kifungu kidogo cha 22.1 cha Masharti ya jumla ya Mkataba kilimtaka mkandarasi wakati wote kuchukua tahadhari zote za kutosha ili kudumisha afya na usalama wa wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kufuata vya kutosha mahitaji ya Afya na Usalama kazini.

Mapitio ya Ripoti za Maendeleo ya kila mwezi kutoka Januari hadi Juni, 2023 yalionyesha kuwa Mkandarasi alikuwa akichukua hatua nzuri kama vile utoaji wa vifaa vya usalama kwa mfano buti za usalama, miwani ya usalama, koti za kuakisika, na kofia ngumu kwa wafanyakazi wake. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mapungufu katika hatua zilizochukuliwa kwa kuhakikisha zinafuatwa taratibu za kutosha za mahitaji ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OHS). Hii ni kwa sababu, hakuna ushahidi wa upatikanaji wa mpango wa afya na usalama kazini, na hakuna ushahidi wa kuwepo kwa mpango wa dharura wa kukabiliana na dharura.

Kukosekana kwa hatua zinazofaa katika kuhakikisha Wizara zinafuatwa taratibu za kutosha na mahitaji ya afya na usalama kazini kunapelekea kutopatikana kwa uhakika usalama kazini na dhamana ya mahitaji ya afya.

### 3.9.6 Kukosekana kwa Maeneo Rasmi ya Utupaji wa Taka

Mahojiano na afisa wa mkandarasi yalionyesha kuwa kulikuwa na kibali cha maeneo ya kutupa taka kutoka kwenye msingi ulioondolewa kabla ya kuweka msingi mpya na barabara ya lami.

Afisa aliyehojiwa wa mkandarasi huyo alifahamisha zaidi ukaguzi kwamba, kulikuwa na mawasiliano kati ya mkandarasi na mwakilishi wa Wizara wa Pemba (Afisa Mdhamini) kuhusu kumuonyesha mkandarasi eneo kwa ajili ya kutupa taka zilizoondolewa, hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilika tarehe 20 hadi 23 Julai, 2023, hakukuwa na idhini iliyotolewa juu ya maeneo ya utupaji taka katika msingi ulioondolewa.

Ukosefu wa utoaji wa idhini katika eneo rasmi la utupaji wa taka umesababisha mkusanyiko wa taka zilizoondolewa kando ya barabara ya riadha (tartan road) ambayo itachelewesha utekelezaji wa shughuli kwenye njia ya riadha. Picha ifuatayo inaonyesha taka zilizokusanywa ambazo zimetoka kwenye barabara ya tartan.

**Picha Nambari 5: Mabaki ya uchafu kutoka Msingi ulioondolewa kwenye njia ya Riadha**



*Picha inayoonyesha mabaki yaliyoondolewa kutoka eneo ambalo njia za riadha itawekwa*

### 3.9.7 Ukosefu wa ushiriki wa wafanyakazi muhimu wa usalama na wataalam wa matibabu katika mradi

Kifungu nambari 58(1) cha Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazini, 2005 kinahitaji kufanyika kwa uchunguzi wa kina wa mara kwa mara wa afya kwa ajili ya uzima wa waajiriwa ambapo uchunguzi huo utafanywa na daktari mwenye sifa kama inavyoweza kuidhinishwa na Mkurugenzi.

Mapitio ya ripoti za Mradi na mahojiano na maafisa wa Mshauri Elekezi na Mkandarasi yalionyesha kuwa hakukuwa na wafanyakazi muhimu wa usalama na wataalam wa matibabu wanaohusika katika mradi huu. Hata hivyo, afisa aliyehojiwa wa mshauri huyo aliongeza kuwa masuala ya afya na usalama yanakumbushwa kila siku kabla ya kuanza kwa shughuli za kila siku.

Mnamo tarehe 20 hadi 23 Julai, 2023 ukaguzi umefanya ziara katika eneo la mradi na kubaini sababu ya kutoajiri wataalamu muhimu wa usalama na matibabu ni kutokana na ukosefu wa utambuzi wa umuhimu wa maafisa hao jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa utekelezaji duni wa afya na usalama kama vile kukosekana kwa vifaa vya huduma ya kwanza kwenye eneo la mradi licha ya uwepo wa ripoti za maendeleo ya kila mwezi zinazoelezea juu ya upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza.

### 3.9.8 Kumaliza kwa muda wa matumizi kwa vifaa vya kuzimia moto (fire extenguishers)

Kifungu nambari 85 cha Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazini ya 2005 kinataka kwamba maeneo yote ya kazi chini ya Sheria hii yatatoa na kudumisha, kupatikana kwa urahisi, njia za kuzima moto, ambazo zitakuwa za kutosha na zinazofaa kwa kuzingatia hali ya kila usalama kwa sehemu za kazi.

Mnamo tarehe 20 hadi 23 Julai, 2023 ukaguzi ulifanya ziara kwenye eneo la mradi na kubaini uwepo wa vifaa vya kuzimia moto ambavyo viliisha muda wa matumizi jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa hasara pindipo majanga ya moto yanapotokezea katika eneo la mradi au eneo jirani na vifaa hivyo kushindwa kufanya kazi kutokana na kumaliza muda wa matumizi.

Hata hivyo ukaguzi ulibaini kwa mara ya mwisho vifaa hivyo vilifanyiwa huduma za maboresho (services) mnamo mwezi wa Julai, 2021 hadi ukaguzi unakamilika hakuna hatua iliyochukuliwa ya kufanya maboresho kwa vifaa hivyo vya kuzimia moto na kupelekea uwepo wa zaidi ya miezi 11 iliyopita bila ya kufanyiwa huduma za maboresho (services) jambo ambalo huwenda likapelekea kutokufanya kazi kabisa au kuharibika kwa kukaa muda mrefu bila ya kufanyiwa maboresho. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini: -

**Picha Nambari 6: Kifaa cha kuzimia moto kilichokosa kufanyiwa service**





*Picha inayoonyesha kifaa cha kuzimia moto kilichomaliza muda wa matumizi (expired) ambacho bado hakijafanyiwa huduma za maboresho (services)*

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha kwamba:

(a) Unamuelekeza Mshauri wa Usimamizi kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi unaambatana na kufuata kikamilifu masuala ya afya, kijamii, usalama, na mazingira. Hii ni pamoja na kuwa na ripoti juu ya afya ya kazi, usalama, kijamii, na mazingira pamoja na rekodi juu ya tukio la ajali; kuwashirikisha maafisa wa afya na usalama kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya afya na usalama kazini, kuwashirikisha maafisa wa mazingira kutekeleza masuala ya mazingira na kijamii; kwa afisa wa afya kwa ajili ya uchunguzi na ufuatiliaji wa masuala ya afya ikiwa ni pamoja na utoaji wa programu za ufahamu juu ya VVU/UKIMWI kwa wafanyakazi; Kusajili mradi kwa ZEMC ili kuwezesha ZEMC kukagua mradi na kutoa uamuzi wa kuwa na Ukaguzi kamili wa Mazingira au kuwa na Mpango wa Usimamizi wa Mazingira ulioandaliwa kwa mradi;

(b) Kuhakikisha idhini ya eneo la utupaji taka inatolewa ili kuhakikisha kuwa vifaa vya msingi vilivyoondolewa ambapo mabaki yanatupwa sehemu husika.

(c) Kuhakikisha kuwa vifaa vya kuzima moto visivyotumika na vilivyokwisha muda wake katika eneo hilo vinafanyiwa marekebisho na kuweza kutumika ili viweze kutumika kwa ufanisi na kuweza kutoa huduma iliyokusudiwa katika eneo la mradi.

## 4.0 MAREJEO


1. Hati za Makisio ya Gharama za Ujenzi (BoQ).
2. BS EN 1997-1: 2004 [Ubunifu wa Kijioteknolojia].
3. Mkataba wa Huduma ya Ushauri - kwa ukarabati wa Uwanja wa Gombani.
4. Felista V. Chiragi (2017); ‘Kiwanda cha Ujenzi Tanzania’ Uchunguzi wa kielimu (Case Study): Kituo cha Michezo cha Vijana Complex Mwananyamala Dar es Salaam.
5. Masharti ya Jumla ya Mkataba.
6. Barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) yenye namba ya kumbukumbu MUUMU. BA.97/383/04/52 ya tarehe 14 Machi, 2022.
7. Barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar yenye kumbukumbu namba MUUMU. BA.97/383/04/52 ya tarehe 14 Machi, 2022.
8. Barua yenye nambari ya kumbukumbu WHVUM/MUUMU/22/16/ VOL.1/68 ya tarehe 9 Machi, 2022.
9. MEDS-044B1E.p65 (egyankosh.ac.in).
10. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (2016), Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma.
11. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (2020), Kanuni za Ununuzi wa Umma.
12. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (2021/22 na 2022/23), Mpango wa Ununuzi wa Mwaka.

13. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (2021/22 na 2022/23).
14. Ripoti za Maendeleo ya kila mwezi za Januari hadi Juni, 2023
15. Hadidu rejea za Mkutano wa Majadiliano kwa mkataba wa kazi wa Juni 7, 2022.
16. Masharti Maalum ya Mkataba.
17. Njia ya Kawaida ya Upimaji wa Ujenzi wa Kazi za Afrika Mashariki Toleo la 1970.
18. Ofisi ya Makamu wa Rais (2004), Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Dar es Salaam.
19. Mkataba wa Kazi – kwa ajili ya Ukarabati wa Uwanja wa Gombani
20. Gazeti la Zanzibar Leo la Alhamisi 21 Oktoba, 2021.
21. Mkataba wa Huduma ya Ushauri - kwa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani.

# KIAMBATISHO NAMBARI 1

## Kiambatisho Nambari 1: Orodha ya maafisa muhimu waliohojiwa

| Namba | Jina | Taasisi | Nafasi | Tarehe ya mahojiano |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fatma Hamad Rajab | MIYCS | Katibu Mkuu | 12/07/2023 |
| 2. | Ameir M. Makame | MIYCS | Kamishna, Idara ya Michezo | 12/07/2023 |
| 3. | Khamis Siasa Khamis | MIYCS | Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti wa Sera (DPPR) | 10/07/2023 |
| 4. | Juma S. Makame | MIYCS | Muhasibu Mkuu | 10/07/2023 |
| 5. | Maryam Abdallah Said | MIYCS | HPDMU | 11/07/2023 |
| 6. | Said Amrani Omar | MCGDEC | Mkuu wa M&E (Mstaafu HPDMU - MIYCS) | 12/07/2023 |
| 7. | Hassan Daud Mrisho | ZBA | Mhandisi wa Kiraia | 06/07/2023 |
| 8. | Salma Mussa Zaid | ZMOS | Afisa wa zamani wa Sheria wa MIYCS | 10/07/2023 |
| 9. | Mwanaidi Juma Suleiman | MIYCS | Afisa wa Sheria | 18/07/2023 |
| 10. | Salum Kh. Rashid | Vyombo vya habari vya serikali | Mshauri wa zamani wa Sheria wa MIYCS (Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala - Vyombo vya Habari vya Serikali) | 27/07/2023 |
| 11. | Mary Minja | Kampuni ya Ushauri ya M/S Diamond Builders Ltd | Mwakilishi wa Mshauri | 20/07/2023 |
| 12. | Victor B. Ndozero [3] | Kampuni ya Ushauri ya Diamond Builders Ltd | Meneja wa Mradi | Kutoka 20/07/2023 hadi 27/07/2023 |

3 Hakuwa kwenye eneo wakati wa ziara ya kukagua mradi, kwa hivyo timu ilimhoji kwa njia ya simu

| Namba | Jina | Taasisi | Nafasi | Tarehe ya mahojiano |
|---|---|---|---|---|
| 13. | Renson Kinyaha | Kampuni ya Ujenzi ya Salem Ltd | Mtathmini wa Mradi(Quantity Surveyor) | 20/07/2023 |
| 14. | Said Malik Said | Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), Pemba | Mhandisi Mkazi | 20/07/2023 |
| 15. | Mfamau Lali Mfamau | MIYCS, Pemba | Afisa Mdhamini | 26/07/2023 |
| 16. | Nassor Abdalla Mohamed | MIYCS, Pemba | Mkaguzi wa Ndani | 26/07/2023 |
| 17. | Nassor Salum Ali | MIYCS, Pemba | Kaimu Meneja wa Uwanja | 26/07/2023 |
| 18. | Abubakari Atik Suleiman | MIYCS, Pemba | Afisa wa Ununuzi na Ugavi | 26/07/2023 |
| 19. | Adam Abdalla Mohamed | MIYCS, Pemba | Ufuatiliaji na Tathmini | 20/07/2023 |
| 20. | Ben Kihomwe | Kampuni ya Ujenzi ya M/S Salem Limited JV Osaju Company Ltd | Mkandarasi | 20/07/2023 |
| 21. | Mohamed Hamad Shehe | Kampuni ya Ujenzi ya M/S Salem Limited JV M/S Osaju Company Ltd | Mkandarasi | 20/07/2023 |
| 22. | Asha Aboud Simai | MIYCS | Afisa wa Ununuzi | 05/07/2023 |
| 23. | Fereshi Juma | MIYCS | Afisa wa Ununuzi | 05/07/2023 |
| 24. | Salum Machano | MIYCS | Afisa wa Ununuzi | 05/07/2023 |

# KIAMBATISHO NAMBARI 2

## Kiambatisho Nambari 2: Orodha ya Hatua za Ufafanuzi zilizotolewa kwa Wakandarasi wote wa Zabuni

| Namba | Hati ya Zabuni (BoQ) | Hatua za Ufafanuzi |
|---|---|---|
| 1 | Kituo kidogo, Ufungaji na Kuagiza ikiwa ni pamoja na (loti 1) (Ukurasa wa 3 kati ya 19, Kipengele namba C) | Wajenzi watakuwa na jukumu la kunukuu au kuamua kiasi cha fedha |
| 2 | Usambazaji wa Jenereta aina ya Perking 400KVA, (Ukurasa wa 4 kati ya 19, Kipengele namba A) | Itakuwa ni;<br>Usambazaji wa jenereta aina ya Perking 400KVA inayojiwasha wenyewe (automatic) Caterpillar dizeli |
| 3 | Ukurasa wa ziada Kipengele (D) namba 4 kati ya 19 | Ondoa paneli moja ya ukuta isiyo na mzigo (safu hadi safu), Usambazaji na uwekaji mlango katika lango la ukubwa kamili ili kuruhusu transforma kuondolewa kupitia mlango huo. |
| 4 | Usambazaji na kuweka Mlango wa mbao kwa Vyoo vya Watazamaji (Ukurasa wa 11 kati ya 19, Kipengele H) | Usambazaji na kuweka Milango ya Vyoo 2.5x7 feet (Aluminium) |
| 5 | Ukurasa wa ziada wa Kipengele (J) no 11 kati ya 19 | Usambazaji na kufunga mlango wa mbao jiko la Mh.Rais (mita 2.1x1). |
| 6 | Usambazaji na kuweka sakafu taizi zilizong'aa za porcelain katika ukumbi wa mkutano 600x600x12mm nene hadi sakafu | Usambazaji na kuweka sakafu taizi zilizong'aa za porcelain katika ukumbi wa mkutano 600x600x12mm ikiwa ni pamoja na kuondoa vigae vilivyopo na kuandaa sakafu kwa ajili ya vigae vipya. |
| 7 | Kipengele A, ukurasa namba 15 kati ya 19 | • Upanuzi wa muundo wa paa la VIP kwa usawa (Kushoto na upande wa kulia) ikiwa ni pamoja na kifuniko cha paa la ALU ZINC kilichotengenezwa na ALAF<br>• Kuandaa na kufunga ngazi mpya za mbao (mbao ngumu; Mninga au kama; ukubwa 1x8 (horizontal and vertical), 2x4 kusaidia kuweka vifaa vyote muhimu ambavyo vimeidhinishwa. |

| Namba | Hati ya Zabuni (BoQ) | Hatua za Ufafanuzi |
|---|---|---|
| 8 | Kipengele B, ukurasa namba 15 kati ya 19 | Ubunifu mpya na kufunga jiko la Mh. Rais kwa;<br>• kuweka Makabati ya Ukutani<br>• Kufunga makabati ya chini yenye ukubwa wa mita 70cmx1 ikiwa ni pamoja na bakuli la kuoshea (washing basin) na vifaa vyote vya kufungia vya mabomba (Plumbing)<br>• kuweka vigae(tiles) katika sakafu na ukutani<br>• Feni la juu<br>• Soketi ya Swichi (Switch socket) 220V (1)<br>• Feni la umeme la kuingiza hewa la ventileta (1) |
| 9 | Kipengele D, ukurasa namba 15 kati ya 19 | Kukarabati Chumba cha Kudhibiti Matangazo kwa kusambaza na kufunga yafuatayo;<br>• Soketi ya njia mbili 2Nr<br>• Kujumuisha samani kama vile viti 3 vya ofisi (kava za ngozi, rangi nyeusi) na meza ya ukumbi wa mkutano 1 (yenye umbo la duara, Mbao za unga, ukubwa wa 80cmx3m rangi nyeusi)<br>• Patishani ya Aluminium (kuweka Ukuta kwa ukuta na urefu mpaka katika dari na mlango wa alumini)<br>• Kipoza hewa ya Tani 1 (1)<br>• Feni la juu ya dari (1)<br>• Mfumo Swichi 220V<br>• Kuandaa sakafu kwa ajili ya kuweka (tiles) 600x600mm |

| Namba | Hati ya Zabuni (BoQ) | Hatua za Ufafanuzi |
|---|---|---|
| 10 | Kipengele E, ukurasa no 15 kati ya 19 | Maelezo kuhusu vifaa vya chumba cha Matangazo (PA Sytem)<br>• Seti 2 za kipaza sauti za kitaalam (toner UHF Dual Cordless), yenye uwezo wa 200MT (TW-630)<br>• kifaa cha kitaalamu cha kuchanganya sauti(Alto) chenye uwezo wa chaneli 24 / BUS MIXER, 3band EQ, 1 USB port,<br>Njia ya 4groung<br>• Kikuza sauti (7) cha kitaalamu (Amplifier) (Behringer EX300) Chenye Uwezo wa chaneli 2 @3000WT<br>• Feni la kutoa baridi (Samson) uwezo wa bidhaa Power Amp / Server Trea ya feni la kupoza Rack Mount Vero 28-238 120J<br>• Vichakataji Sauti (Sound Processors) (Track DS) uwezo wa bidhaa input 2 na output 4 ((2x2 way, 3way, 4way, 2way sub). 3x24<br>bits / 48KHZ DSPs)<br>• Vifaa vya ufungaji na waya<br>• Uwezo wa bidhaa ya Amprack 23.5 (27.5 na casters) x20x18 Uzito 36.4lbs (kilo 16.6) makisio. uzito 300lb /kilo 135.<br>• Vipaza sauti vya nje vya VIP vilivyokua haviingii maji 3000WT (10pcs) |

| Namba | Hati ya Zabuni (BoQ) | Hatua za Ufafanuzi |
|---|---|---|
| 11 | Kipengele A, ukurasa namba 16 kati ya 19 | • Vyoo 4 vyenye ukubwa wa mita 1.2x1.8<br>• Viingilizi vya hewa (2)<br>• Bideti za haja ndogo (bidet Urinals) -4<br>• Milango ya Alumini- 4p<br>• Feni la dari 2 na Kipoza hewa Tani 1 (1) katika Chumba cha kubadilishia nguo wachezaji<br>• Kuondoa mlango uliopo na utumie ukuta wa matofali 150mm kwa kuweka ukubwa wa ufunguzi mita 1x2.5 |
| 12 | Kipengele C, ukurasa namba 16 kati ya 19 | Uanishaji wa lami; KIWANGO CHA FIFA |
| 13 | Ongeza asilimia 2 kwa ajili ya mambo ya dharura | Itakuwa ni; Kuongeza kwa ajili ya dharura Shilingi 300,000,000/- |

*Chanzo: Hadidu rejea za mkutano wa kabla ya mkutano na ziara ya eneo ambayo ilifanyika tarehe 22 Aprili, 2022 na tarehe 23 Aprili, 2022 katika Wizara na eneo la mradi mtawaliwa*

# KIAMBATISHO NAMBARI 3

## Kiambatisho Nambari 3: Kuingizwa kwa Maoni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| Namba | Rasimu ya Maoni ya Mwanasheria Mkuu | Kuingizwa kwa maoni na Afisa wa Uhasibu kulingana na mkataba wa sasa wa kazi uliosainiwa | Maoni ya Wakaguzi |
|---|---|---|---|
| 1 | Bei ya Mkataba: Bei ya mkataba iliyotajwa katika rasimu ni Tsh 2,975,000,000/- Pamoja na VAT na asilimia 2 ya dharura na ada ya ushauri. Mkataba huu ni kati ya Wizara na Mkandarasi. Kwa hiyo, ada ya ushauri haihitajiki katika mkataba huu. | Bei ya mkataba ni Tsh 2,800,000,000/- PAMOJA NA VAT. Kwa hivyo, ada ya ushauri imetengwa | |
| 2 | **Kusainiwa kwa mkataba:** Utiaji saini wa mkataba (Contractor) uliotajwa katika rasimu ni kampuni mbili ambazo zitafanya ubia wa pamoja.<br><br>**Mipaka ambayo ilitokea** | | |

